



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI



HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI

MHESHIMIWA JANUARY YUSUF MAKAMBA (MB.),

**AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA
MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA
NISHATI KWA MWAKA**

2022/23







VIONGOZI WAKUU WA WIZARA YA NISHATI



**Mhe. January Y. Makamba (Mb.)
Waziri wa Nishati**



**Mhe. Wakili. Stephen L. Byabato
(Mb.)
Naibu Waziri wa Nishati**



**Mha. Felchesmi J. Mramba
Katibu Mkuu**



**Bw. Kheri A. Mahimbali
Naibu Katibu Mkuu**

**HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA
JANUARY YUSUF MAKAMBA (MB.), AKIWASILISHA
BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA
WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2022/23**

A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2021/22 na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa mwaka 2022/23.
2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na fursa ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2022/23. Aidha, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama kama Waziri wa Nishati katika Serikali ya Awamu ya Sita (6) na kuwasilisha Hotuba hii, kwa namna ya kipekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, kwa kuniamini na kunitfea kuwa Waziri wa Nishati tarehe 12 Septemba, 2021. Uteuzi huu ni dhamana na heshima kubwa kwangu katika kuhakikisha kuwa Sekta ya Nishati inakidhi matarajio ya Watanzania ya kupata umeme wa uhakika pamoja na kuendeleza rasilimali za mafuta na gesi kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Naahidi kwa neema ya Mwenyezi Mungu nitayatekeleza majukumu yangu kwa uadilifu kwa kushirikiana na Bunge lako Tukufu pamoja na wadau wengine katika Sekta ya Nishati.
3. **Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri mkubwa anaouonesha katika kuiongoza nchi yetu tangu alipoingia madarakani mwezi Machi, 2021. Ni dhahiri kuwa miongozo, dira na maelekezo anayotoa yamekuwa chachu kwangu katika kusimamia Sekta ya Nishati na kwa maendeleo ya Taifa letu kwa ujumla katika nyanja mbalimbali.
4. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuwashukuru Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo mbalimbali wanayonipatia katika kusimamia Sekta ya Nishati. Vilevile, nampongeza Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea na usimamizi mahiri wa shughuli za maendeleo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
5. **Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii pia kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kwa kishindo na Waheshimiwa Wabunge ili muweze kuliongoza Bunge letu Tukufu. Aidha, nimpongeze pia Bi. Nenelwa Mwihambi kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Katibu wa Bunge. Ni wazi kuwa chini ya uongozi wenu Bunge letu limeendelea kuwa mahiri zaidi katika kusimamia na kuishauri Serikali kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali na hatimae kuboresha maisha ya wananchi wetu.
6. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. Dunstan Luka Kitandula (Mb.), Makamu Mwenyekiti Mhe. Seif Khamis Gulamali (Mb.), na Wajumbe wote wa Kamati kwa michango na ushauri wao wakati wa kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2021/22 na uchambuzi wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/23. Napenda kuahidi kuwa, Wizara ya Nishati itazingatia ushauri wa Kamati wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Nishati kwa mwaka 2022/23.

7. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuungana na waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapongeza Mhe. Emmanuel Lekishon Shangai, Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro; Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Jimbo la Ushetu; na Mhe. Mohamed Said Issa, Mbunge wa Jimbo la Konde Pemba kwa kuchaguliwa kuwa wawakilishi wa wananchi katika Majimbo hayo. Pia, nampongeza Mhe. Shamsi Vuai Nahodha kwa kuteuliwa na Mhe. Rais kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, napenda kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu, familia, ndugu, jamaa, na wananchi kwa kuondokewa na wapendwa wetu, Mhe. Elias John Kwandikwa aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu; Mhe. William Tate Ole Nasha aliyekuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji na Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Mhe. Irene Alex Ndyamkama aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Rukwa. Tunaomba Mwenyeze Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.
8. **Mheshimiwa Spika**, Hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui ya Hotuba ya Mhe. Kassim M. Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2022/2023.
9. **Mheshimiwa Spika**, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2021/22 pamoja na Mpango wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2022/23.

**B. UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA
KWA MWAKA 2021/22**

10. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2021/22, Wizara iliendelea na utekelezaji wa mipango yake ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Nishati inachangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi na Pato la Taifa. Maeneo ya kipaumbele yaliyozingatiwa yalikuwa ni: kuendelea kutekeleza miradi ya uzalishaji umeme nchini ili kufikia lengo la kuwa na MW 5,000 ifikapo mwaka 2025; kuimarisha mifumo ya usafirishaji umeme nchini; kuendelea na utekelezaji wa Miradi ya Kupeleka Umeme Vijiji kuititia Wakala wa Nishati Vijiji (REA); kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (*East African Crude Oil Pipeline - EACOP*) kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania; utekelezaji wa Mradi wa Kusindika Gesi Asilia (LNG); kuimarisha shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia hususan katika vitalu vya kimkakati vikiwemo Mnazi Bay Kaskazini na Eyasi Wembere; kuongeza kasi ya usambazaji wa gesi asilia; kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Nishati; na kuendelea kuimarisha utendaji wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara ili kuongeza ufanisi katika usimamizi na uendelezaji wa Sekta ya Nishati.

**Bajeti ya Matumizi ya Wizara na Mtiririko
wa Fedha kwa Mwaka 2021/22**

11. **Mheshimiwa Spika**, Bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2021/22 ilikuwa **Shilingi trilioni 2.386**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi trilioni 2.359** sawa na **asilimia 98.89** zilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na **Shilingi bilioni 27.22** sawa na **asilimia 1.11** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.
12. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Mei, 2022 Wizara ya Nishati ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi trilioni 1.820**, sawa na **asilimia 76.29** ya Bajeti yote ya Wizara kwa

Mwaka 2021/22. Kati ya fedha hizo **Shilingi trilioni 1,797** zilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na Shilingi **bilion 22.83** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

13. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika mwaka 2021/22 pamoja na mambo mengine, uliongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III) 2021/22 – 2025/26; Sera, Mikakati na Programu mbalimbali za Kisekta na Kitaifa pamoja na Malengo ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030 kuhusu upatikanaji wa nishati.

SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU


B 1: UZALISHAJI, USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI UMEME NCHINI

Uzalishaji Umeme

14. ***Mheshimiwa Spika***, Hadi kufikia mwezi **Mei 2022**, uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa ni **MW 1,694.55** ambapo **MW 574.60** sawa na asilimia 33.91 ni kutokana na nguvu ya maji, **MW 1,021.32** sawa na **asilimia 60.27** gesi asilia, **MW 88.13** sawa na **asilimia 5.20** mafuta (yanayotumiwa kwa nyakati za dharura) na **MW 10.50** sawa na **asilimia 0.62** umeme unaozalishwa kutokana na Tungamotaka (Biomass). Uwezo wa mitambo hiyo unajumuisha mitambo inayomilikiwa na TANESCO ambayo huchangia **MW 1,482.29** sawa na **asilimia 87.47** na mitambo ya wazalishaji binafsi (IPPs/SPPs) ambayo huchangia **MW 212.26** sawa na **asilimia 12.53**. **Kielelezo Na. 1** kinaonesha mchanganuo wa uwezo wa mitambo ya kufua umeme katika Gridi ya Taifa.

Kielelezo Na. 1: Mchanganuo wa Uwezo wa Mitambo ya Kufua Umeme Katika Gridi ya Taifa

Chanzo	Uwezo	
	MW	%
Maji	574.60	33.91%
Gesi Asilia	1,021.32	60.27%
Tungamotaka	10.50	0.62%
Jumla	1,694.55	100.00%




15. ***Mheshimiwa Spika***, uwezo wa kuzalisha umeme kwa mitambo ambayo haijunganishwa katika Gridi ya Taifa umefikia MW 38.83 ambazo zinajumuisha mitambo inayomilikiwa na TANESCO yenye uwezo wa kufua MW 33.83 na **MW 5** zitokanazo na nguvu ya juu kutoka kwa mzalishaji binafsi NextGen Solawazi na hivyo kufanya jumla ya uwezo wa mitambo ya kufua umeme nchini kufikia **MW 1,733.38** ikilinganishwa na **MW 1,605.86** zilizokuwepo mwaka 2020/21, sawa na ongezeko la **asilimia 7.94**. Ongezeko hili limetokana na utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo Ubungo III wenye kuzalisha **MW 120** kwa kutumia gesi asilia. Mchanganuo wa uwezo wa mitambo hiyo ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 1**.

Hotuba ya Waziri wa Nishati

16. **Mheshimiwa Spika**, mahitaji ya juu ya umeme katika mfumo wa Gridi ya Taifa yameendelea kukua na kufikia **MW 1,335.01** yaliyofikiwa tarehe 25 Machi, 2022 saa 2:00 usiku ikilinganishwa na **MW 1,201.02** zilizokuwa zimefikiwa mwaka 2020/21, sawa na ongezeko la **asilimia 11.16. Kielelezo Na. 2** kinaonesha Mwenendo wa Ukuaji wa Mahitaji ya Juu ya Umeme katika Gridi ya Taifa kwa Miaka 10 kuanzia mwaka 2013 hadi Mwezi Mei, 2022.

Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa Ukuaji wa Mahitaji ya Juu ya Umeme katika Gridi ya Taifa



Usafirishaji Umeme

17. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutayarisha na kutekeleza miradi mbalimbali ya njia za kusafirisha umeme ambayo inalenga kuboresha upatikanaji wa umeme, hususan kwenye mikoa ambayo bado haijafikiwa na Gridi ya Taifa na uhakika wa umeme kwa kujenga njia za mzunguko pete (*ring circuit*) ili kuwezesha umeme kupita njia mbadala pale miundombinu ya usafirishaji inapopata hitifaluu. Miradi hiyo ni pamoja na: Iringa – Sumbawanga **kV 400**; Sumbawanga – Kigoma **kV 400**; Nyakanazi – Kigoma **kV 400**; Singida – Arusha – Namanga **kV 400**; Julius Nyerere – Kinyerezi **kV 400**; Chalinze – Dodoma **kV 400**; Iganga – Mbeya – Kasumulu – Kyela **kV 400**; Sumbawanga – Katanga **kV 400**; Mutukula – Kyaka – Nyakanazi – Geita – Mabuki **kV 400**; Geita – Nyakanazi **kV 220**; na Rusumo – Nyakanazi **kV 220**. Miradi hiyo itakapokamilika itawezesha mauziano ya umeme kati ya Tanzania na nchi jirani

ikiwemo Kenya, Uganda, Rwanda, DRC na Burundi kupitia *Eastern African Power Pool (EAPP)*; na Msumbiji na Malawi kupitia *Southern African Power Pool (SAPP)*.

18. **Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia mwezi Mei, 2022 jumla ya urefu wa njia za kusafirisha umeme imefikia kilomita **6,111.27** ambapo kati ya hizo, njia za msongo wa **kV 400** ni kilomita **670**; **kV 220** ni kilomita **3,225.7**; **kV 132** ni kilomita **1,672.57** na **kV 66** ni kilomita **543**. Aidha, ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa KV 220 kutoka Geita hadi Nyakanazi yenye urefu wa kilomita 144 ambayo kwa sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 99 unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2022. Kukamilika kwa njia hii kutafanya jumla ya njia za kusafirisha umeme kufikia kilomita **6,255.27**. **Kiambatisho Na. 2** kinaonesha mtandao wa njia za kusafirisha umeme nchini (*National Grid Network*).

Usambazaji Umeme

19. **Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na changamoto ya kukatika kwa umeme nchini kutokana na miundombinu kuzidiwa kutokana na kuongezeka kwa mahitaji kwa kasi, uchakavu wa miundombinu na shughuli za kibinadamu kama vile magari kugonga nguzo, nguzo kuchomwa moto na hujuma katika miundombinu. Aidha, ili kuimarisha miundombinu ya usambazaji umeme, Serikali imeendelea kutayarisha na kutekeleza miradi mbalimbali ya kusambaza umeme katika mikoa mbalimbali ikiwemo Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Dodoma na Pwani itakayowezesha kuondokana na changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara na hivyo kuwa na umeme wa uhakika. Miradi hiyo inaenda sambamba na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme na ufungaji wa mashineumba kwa kuzingatia mahitaji ya sasa na ya baadae katika eneo husika.
20. **Mheshimiwa Spika**, njia za usambazaji umeme zimefikia jumla ya kilomita **153,988.49**, ambapo kati ya hizo, njia za msongo wa **kV 33** ni kilomita **48,965.73**, msongo wa **kV 11** ni kilomita **12,648.73** na msongo wa **kV 0.4** ni kilomita **92,374.03**. Hii ni sawa na ongezeko la **asilimia 3.67** ikilinganishwa na kilomita **148,544.23** zilizokuwepo hadi mwezi Juni, 2021. Aidha, jumla ya mashineumba za usambazaji umeme zimefikia **27,863** ikilinganishwa na mashineumba **26,438** mwezi Juni, 2021 sawa na ongezeko la **asilimia 5.40**. Miundombinu hii imewezesha jumla ya wateja waliouanganishiwa umeme nchini kufikia **3,735,886** ikilinganishwa na wateja **3,290,490** waliokuwepo kufikia mwezi Juni, 2021 sawa na ongezeko la **asilimia 13.54**. **Kielelezo Na. 3** kinaonesha Miundombinu ya Usafirishaji, Usambazaji Umeme na Vituo vya Kupoza Umeme hadi Kufikia mwezi Mei, 2022.

Kielelezo Na. 3: Miundombinu ya Usafirishaji, Usambazaji Umeme na Vituo vya Kupoza Umeme hadi Kufikia mwezi Mei, 2022

Na	Njia za Usafirishaji Umeme	Urefu (km)
1	Njia za msongo wa kV 400	670
2	Njia za msongo wa kV 220	3,225.70
3	Njia za msongo wa kV 132	1,672.57
4	Njia za msongo wa kV 66	543
Jumla		6,111.27

Na	Njia za Usambazaji Umeme	
1	Njia za msongo wa kV 33	48,965.73
2	Njia za msongo wa kV 11	12,648.73
3	Njia za msongo wa kV 0.4	92,374.03
Jumla		153,988.49

Na	Vituo vya Kupoza Umeme	Idadi
1	Vituo vya Msongo wa kV 220	23
2	Vituo vya Msongo wa kV 132	30
3	Vituo vya Msongo wa kV 66	7
4	Vituo vya Msongo wa kV 33/11	67
Jumla		127

Na	Njia za Usafirishaji Umeme	Urefu (km)
1	Mkongo wa Mawasiliano	4,368

B 2: MIRADI YA KUZALISHA UMEME

B 2.1: MIRADI ILIYOPO KATIKA HATUA ZA UTEKELEZAJI

- (i) *Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Julius Nyerere Hydro Power Project (JNHPP) – MW 2,115*
21. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 2,115** kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rufiji. Gharama ya mradi huu ni **Shilingi trilioni 6.55** ambazo zinatolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa **asilimia 100**. Hadi kufikia mwezi Mei, 2022 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilika kwa uchimbaji na ujenzi wa handaki la kuchepusha maji (*diversion tunnel*) na kuendelea na ujenzi wa: bwawa (*main dam and spillways*); njia kuu za kupitisha maji (*tunnels*); kituo cha kuzalisha umeme (power house); na kituo cha kuongeza nguvu ya umeme (*switchyard*).
22. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa mradi wa Julius Nyerere katika maeneo yote kwa ujumla umefikia **asilimia 60.22**. Malipo kwa mkandarasi hadi kufikia mwezi Mei, 2022 ni jumla ya Shilingi **trilioni 3.84** ambayo ni sawa na **asilimia 100** ya fedha zilizotakiwa kuwa zimelipwa kulingana na hatua ya utekelezaji wa mradi iliyofikiwa, kiwango hicho ni sawa na **asilimia 58.63** ya gharama zote za mradi.
- (ii) *Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension – MW 185*
23. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahu upanuzi wa kituo cha Kinyerezi I – **MW 150** kwa kuongeza mitambo itakayozalisha MW 185 na hivyo kufanya kituo hicho kuzalisha jumla ya **MW 335**. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa **asilimia 100** kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 188** sawa na

takriban **Shilingi bilioni 437.31**. Utekelezaji wa mradi huu ulisimama mwezi Mei, 2020 kutokana na kufilisika kwa aliyekuwa Mkandarasi wa mradi *M/s Jacobsen Electro As* wa Norway. Hata hivyo, ili kuhakikisha mradi huu unakamilika, Serikali kupitia TANESCO imempata Mkandarasi mwingine Kampuni ya *CSI Energy Group (Tanzania) Limited* kwa ajili ya kukamilisha kazi ya ujenzi wa mradi.

24. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia mwezi Mei, 2022 ujenzi wa misingi ya kufunga mitambo umekamilika; mitambo minne (4) ya kuzalisha umeme ipo tayari katika eneo la mradi; na ufungaji wa mitambo miwili (2) kati ya minne (4) ukiwa umeanza na inatarajiwa kuwashwa kabla ya mwezi Juni, 2022 na mingine miwili (2) itawashwa mwezi Agosti, 2022. Aidha, upanuzi wa kituo cha kupokea umeme umekamilika. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 88** na unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2022.
- (iii) *Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rusumo – MW 80*
25. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 80** kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Kagera na unahusisha nchi tatu (3) za Tanzania, Burundi na Rwanda kwa mgawanyo sawa kwa kila nchi. Kwa upande wa Tanzania mradi unahu pia ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme yenye msongo wa **KV 220** kutoka Rusumo hadi Nyakanazi. Gharama za mradi kwa upande wa Tanzania ni **Dola za Marekani milioni 113** sawa na takriban **Shilingi bilioni 262.85** kwa ufadhili wa Benki ya Dunia.

26. ***Mheshimiwa Spika***, kazi zilizokamilika hadi kufikia mwezi Mei, 2022 ni: ujenzi wa eneo la kusimika mitambo (*power house*); na milango ya kuingiza na kuchepusha maji (*spillway and intake gates*). Aidha, usimikaji wa mitambo umefikia **asilimia 88** na ujenzi wa handaki la kupitishia maji unaendelea. Vilevile, miradi yote ya kijamii ya awamu ya kwanza kwa upande wa Tanzania imekamilika. Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia **asilimia 91.6** na unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2022.
- (iv) ***Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Malagarasi – MW 49.5***
27. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 49.5** kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Malagarasi, mkoani Kigoma. Aidha, mradi utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 132** yenye urefu wa kilomita **54** kutoka Malagarasi hadi Kidahwe, mkoani Kigoma. Gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 144.14** sawa na takriban Shilingi bilioni 335.28 na unatekelezwa kwa ufadhilli wa Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) kwa takriban **Shilingi bilioni 325.65** na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inachangia **Shilingi bilioni 9.63**. Kazi zilizofanyika katika kipindi cha mwaka 2021/22 ni kuanza taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi na Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

B 2.2: MIRADI ILIYOPO KATIKA HATUA ZA UTAYARISHAJI

- (i) ***Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Ruhudji – MW 358***
28. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 358** kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhudji mkoani Njombe na unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita **170** kutoka Ruhudji hadi kituo cha kupoza umeme cha Kisada mkoani Iringa. Gharama za ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 407.4** sawa na takriban **Shilingi bilioni 947.65** na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 53.2** sawa na takriban **Shilingi bilioni 123.75**. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakinifu ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2022.
- (ii) ***Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kakono – MW 87***
29. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 87** kwa kutumia maji ya Mto Kagera na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** kutoka Kakono hadi Kyaka yenye urefu wa kilomita **38.5** pamoja na ukarabati wa kituo cha kupoza umeme cha Kyaka. Gharama za ujenzi wa mradi ni **Dola za Marekani milioni 287.6** sawa na takriban **Shilingi bilioni 668.99** ambazo zitatolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Umoja wa Ulaya (EU) na Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD).

Hotuba ya Waziri wa Nishati

30. Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kufuatia misheni ya kufanya tathmini ya mradi (Kakono HPP Appraisal Mission) iliyofanyika tarehe 30 Machi, 2022 ilijojumuisha Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Nishati pamoja na TANESCO ilibainika kuwa kutokana na mabadiliko ya hali ya uchumi na kupanda kwa gharama za chuma duniani gharama ya mradi inakadiriwa kufika **Dola za Marekani 310.8**. Katika mwaka 2021/22 Serikali kuitia TANESCO iliendelea na taratibu za kuhuisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii kulingana na matakwa ya kimataifa ili kukidhi taratibu za ufadhili wa mradi.

(iii) **Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rumakali – MW 222**

31. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 222** kwa kutumia maji ya Mto Rumakali mkoani Njombe na njia ya kusafirisha umeme yenye msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 150 kutoka kwenye mitambo hadi kituo cha kupoza umeme cha Iganjo mkoani Mbeya. Gharama za mradi huu kwa pamoja zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 388.22** sawa na takriban **Shilingi bilioni 903.04**. Kwa kipindi cha mwaka 2021/22 kazi zilizofanyika ni pamoja na kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakinifu.

(iv) **Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kikonge – MW 300**

32. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 300** kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhuhu mkoani Njombe na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita **53** kutoka

Kikonge hadi kituo cha kupoza umeme cha Madaba. Mradi huu unahusisha pia ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji. Jumla ya gharama za mradi zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 795.4** sawa na takriban **Shilingi trilioni 1.85** ambapo kati ya fedha hizo gharama ya kuzalisha na kusafirisha umeme ni **Shilingi trilioni 1.65** na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ni **Shilingi bilioni 202.37**. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilika kwa Upembuzi Yakinifu; na kuanza kwa taratibu za kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii.

(v) **Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Mtwara – MW 300**

33. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 300** kwa kutumia gesi asilia katika Mkoa wa Mtwara. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 421.1** sawa na takriban **Shilingi bilioni 979.52**. Mradi huu unatekelezwa sambamba na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita 268 kutoka Mtwara hadi Somanga Fungu. Kazi zilizotekelizwa hadi sasa ni pamoja na kukamilika kwa Upembuzi Yakinifu wa kituo cha kuzalisha umeme na njia ya kusafirisha umeme; na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii ya mradi pamoja na miundombinu wezeshi ya maji, barabara na bomba la gesi. Aidha, majadiliano ya ufadhili wa mradi kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Japan kuitia JICA yameanza.

(vi) *Mradi wa Kuzalisha Umeme Jua Shinyanga – MW 150*

34. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia jua eneo la Kishapu mkoani Shinyanga wenyewe uwezo wa kuzalisha **MW 150**. Gharama ya mradi huu ni **Euro milioni 115.30** sawa na takriban **Shilingi bilioni 296.4**. Mradi huu unatekelezwa katika awamu mbili, awamu ya kwanza itahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme **MW 50** utakaogharimu kiasi cha **Euro milioni 42.32** sawa na takriban **Shilingi bilioni 109.1**. Awamu hii itaenda sambamba na uboreshaji wa miundombinu ya gridi (*grid modernization*) ili kuruhusu gridi kuweza kubeba umeme wa nishati jadidifu. Uboreshaji huu utakagharimu **Euro milioni 87** sawa na takriban **Shilingi bilioni 224.2**. Awamu ya kwanza ya mradi huu inafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD).
35. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa awamu ya pili utahusu upanuzi wa kituo cha kuzalisha umeme kwa kuongeza **MW 100** utakaogharimu kiasi cha **Euro milioni 72.98** sawa na takriban **Shilingi bilioni 188.1** ambapo taratibu za ufadhili zinaendelea. Kwa kipindi cha mwaka 2021/22, kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha taratibu za ufadhili wa awamu ya kwanza ambapo mkataba wa mkopo ulisainiwa mwezi Julai 2021; kukamilisha zabuni za mradi; na kuanza taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi.

B 3: MIRADI YA KUSAFIRISHA NA KUSAMBAZA UMEME

B 3.1: MIRADI ILIYOPO KATIKA HATUA ZA UTEKELEZAJI

- (i) *Julius Nyerere Hydro Power Plant hadi Chalinze – KV 400 na Kituo cha Kupoza Umeme, Chalinze*
36. ***Mheshimiwa Spika***, sehemu hii inahu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** yenye urefu wa **kilomita 162** kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Julius Nyerere hadi Chalinze mkoani Pwani unaogharimu kiasi cha **Dola za Marekani milioni 51.4** na **Shilingi bilioni 31.9**; na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Chalinze unaogharimu kiasi cha **Dola za Marekani milioni 42.5** na **Shilingi bilioni 29.8**. Kwa kipindi cha mwaka 2021/22, kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha usanifu wa mradi; kulipa fidia kwa wananchi walipisha eneo la mradi; kuanza ujenzi ambapo ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme umefikia **asilimia 44** na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme umefikia **asilimia 3.59**.
- (ii) *Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Geita hadi Nyakanazi na Kituo cha Kupoza Umeme, Nyakanazi*
37. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa **kilomita 144** kutoka Geita hadi Nyakanazi; ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi; na kusambaza umeme katika vijiji 32 vinavyopitiwa na mradi. Gharama za utekelezaji wa mradi huu ni **Euro milioni 45** sawa na takriban Shilingi bilioni 127. Kazi zilizofanyika hadi mwezi Machi, 2022 ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ambao umekamilika kwa **asilimia 99**; ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi na upanuzi

Hotuba ya Waziri wa Nishati

- wa kituo cha Geita ambao umefikia **asilimia 98**; na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji umeme katika vijiji vinavyopitiwa na mradi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2022.
- (iii) **Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Singida – Arusha – Namanga na Kituo cha Kupoza Umeme, Lemugur**
38. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita **414** kutoka Singida hadi Namanga kuititia Babati na Arusha. Mradi huu pia unahusisha ujenzi wa kituo kipywa cha kupoza umeme cha Lemugur katika eneo la Kisongo mkoani Arusha na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Singida na usambazaji wa umeme katika vijiji 19 vilivyo jirani na mkuza wa njia ya umeme katika mikoa ya Singida, Manyara na Arusha. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo gharama ya mradi ni **Dola za Marekani milioni 258.82** sawa na takriban **Shilingi bilioni 602.04**.
39. **Mheshimiwa Spika**, hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Singida hadi Babati na Babati hadi Arusha kwa **asilimia 100**; Arusha hadi Namanga kwa **asilimia 77**; na kuendelea na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Lemugur ambao umefikia **asilimia 62.9**. Kwa ujumla mradi umefikia **asilimia 79.3** na mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2022.
- (iv) **Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma na Kituo cha Kupoza Umeme, Kidahwe**
40. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma yenye urefu wa kilomita **280**, ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Kidahwe Mkoani Kigoma, upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi na usambazaji umeme katika vijiji 18 vilivyo katika eneo la mradi. Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 187** sawa na takriban **Shilingi bilioni 434.98** na zinatolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Exim ya Korea Kusini (EDCF) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kazi zilizotekelawa ni pamoja na kukamilisha ulipaji wa fidia katika eneo la Kidahwe na eneo la mkuza wa njia ya kusafirisha umeme; kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa njia ya usafirishaji umeme; na ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme.
- (v) **Mradi wa Backbone Transmission Investment Project (BTIP) - Phase II**
41. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu ni wa awamu ya pili ya mradi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** kutoka Iringa hadi Shinyanga kuititia Dodoma na Singida yenye urefu wa kilomita **670**. Mradi unalenga kuongeza uwezo (upgrade) wa vituo vinne (4) vya kupoza umeme vya Iringa, Shinyanga, Singida na Dodoma kutoka **kV 220** hadi **kV 400**. Gharama ya mradi wa awamu ya pili ni **Dola za Marekani milioni 120** sawa na takriban **Shilingi bilioni 279.13**. Kazi zilizotekelawa ni pamoja na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Singida na Dodoma ambavyo vimekamilika kwa **asilimia 100** mwezi Januari, 2022; na kuendelea na taratibu za kumpata mfadili kwa ajili ya upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Iringa na Shinyanga.

- (vi) *Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi*
42. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita **94** kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Rusumo hadi Nyakanazi. Gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 35** sawa na takriban **Shilingi bilioni 81.41** na unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kazi zilizoteklezwa ni pamoja na ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi; na kuendelea na ujenzi wa mradi. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 79**.
- (vii) *Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (Standard Gauge Railway – SGR II, Lot I)*
43. ***Mheshimiwa Spika***, awamu ya kwanza ya mradi huu ilihusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita **160** kutoka Kinyerezi, Dar es Salaam hadi Kingolwira, Morogoro kwa gharama ya **Shilingi bilioni 76.23** na ulikamilika mwezi Januari, 2021. Awamu ya pili ya mradi huu inahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 410 kutoka Msamvu, Morogoro hadi Kintinku, Singida kwa ajili ya kuendesha Treni ya Umeme (*Standard Gauge Railway – SGR*). Gharama za mradi ni **Shilingi bilioni 164.3** na unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa **asilimia 100**. Ujenzi wa mradi huu ulianza mwezi Novemba, 2020 na hadi mwezi Mei, 2022 umefikia **asilimia 88**.
- (viii) *Mradi wa Ujenzi wa kituo Kipycha cha Kupoza Umeme Luguruni*
44. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahu ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Luguruni kitakachohusisha ufungaji wa mashineumba mbili (2) zenyе uwezo wa **MVA 90** kila moja. Mradi huu utakuwa na matoleo (outgoing feeders) sita (6) ya msongo wa **kV 33** ambayo yataboresha upatikanaji wa umeme katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Gharama ya mradi ni **Shilingi bilioni 15.2** na unagharamiwa na Serikali kupitia TANESCO. Kazi zilizoteklezwa ni pamoja na ujenzi wa misingi ya mashineumba na vifaa vya kudhibiti mfumo wa umeme. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 92**.
- ### B 3.2: MIRADI AMBAYO IPO KWENYE UTAYARISHAJI
- (i) *Chalinze - Kinyerezi kV 400*
45. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita **93** kutoka kituo cha kupoza umeme cha Chalinze hadi kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi. Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 42.882** sawa na takriban **Shilingi bilioni 99.74**. Aidha, mradi huu unahuishwa upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi utakaogharimu kiasi cha **Dola za Marekani milioni 71.4** sawa na takriban **Shilingi bilioni 166.08**. Kazi zilizofanyika ni pamoja na: kulipa fidia kwa wananchi watakoopisha mradi; kukamilisha Upembuzi Yakinifu; usanifu wa mradi; na kuendelea kukamilisha taratibu za ufadhili.

(ii) *Chalinze - Dodoma kV 400*

46. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita 345 kutoka kituo cha kupoza umeme cha Chalinze hadi Dodoma. Mradi huu utahusisha pia upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Dodoma. Gharama za mradi huu kwa upande wa njia ya kusafirisha umeme ni **Dola za Marekani milioni 159.98** sawa na takriban **Shilingi bilioni 372.13**, na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Dodoma ni **Dola za Marekani milioni 13.2** sawa na takriban **Shilingi bilioni 30.70**. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha Upembuzi Yakinifu; usanifu wa mradi; na kuendelea kukamilisha taratibu za ufadhili.

(iii) *Kinyerezi - Somanga Fungu kV 400 na Vituo vya Kupoza Umeme, Somanga Fungu na Mkuranga*

47. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita 198 kutoka kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi hadi ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Somanga Fungu na Mkuranga. Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 150** sawa na takriban **Shilingi bilioni 348.92**. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; kukamilisha Upembuzi Yakinifu; usanifu wa mradi; na kuendelea kukamilisha taratibu za ufadhili.

(iv) *Chalinze - Segera kV 400 na Kituo cha Kupoza Umeme, Segera*

48. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita 181 kutoka kituo cha kupoza umeme cha Chalinze hadi kituo cha kupoza umeme cha Segera. Gharama za mradi huu katika njia ya kusafirisha umeme ni **Dola za Marekani milioni 65.87** sawa na takriban **Shilingi**

bilioni 153.22 na kituo cha kupoza umeme cha Segera ni **Dola za Marekani milioni 45.97** sawa na takriban **Shilingi bilioni 106.93**. Kazi zilizofanyika ni pamoja na: kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; kukamilisha Upembuzi Yakinifu; usanifu wa mradi; na kuendelea kukamilisha taratibu za ufadhili.

(v) *Segera - Tanga kV 220 na Kituo cha Kupoza Umeme, Tanga*

49. **Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 64 kutoka kituo cha kupoza umeme cha Segera hadi Tanga. Mradi huu utahusisha pia ujenzi wa kituo kipyä cha kupoza umeme cha Tanga. Gharama za mradi kwa upande wa njia ya kusafirisha umeme ni **Dola za Marekani milioni 19.77** sawa na takriban **Shilingi bilioni 45.99**, na upande wa kituo cha kupoza umeme ni **Dola za Marekani milioni 31.6** sawa na takriban **Shilingi bilioni 73.50**. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha Upembuzi Yakinifu; usanifu wa mradi; na kuendelea na taratibu za kupata fedha za utekelezaji wa mradi.

(vi) *Chalinze - Bagamoyo kV 220 na Kituo cha Kupoza Umeme, Bagamoyo*

50. **Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 90 kutoka kituo cha kupoza umeme cha Chalinze hadi Bagamoyo. Mradi huu utahusisha pia ujenzi wa kituo kipyä cha kupoza umeme cha Bagamoyo. Gharama za mradi kwa upande wa njia ya kusafirisha umeme ni Dola za Marekani milioni 27 sawa na takriban **Shilingi bilioni 62.8**, na upande wa kituo cha kupoza umeme ni **Dola za Marekani milioni 32** sawa na takriban **Shilingi bilioni 74.44**. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha Upembuzi Yakinifu; usanifu wa mradi; na kuendelea na taratibu za kupata fedha za utekelezaji wa mradi.

**(vii) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme
Msongo wa kV 400 kutoka Somanga Fungu
hadi Kinyerezi**

51. **Mheshimwa Spika**, gharama za mradi huu zinakadirwa kuwa **Dola za Marekani milioni 150** sawa na takriban **Shilingi bilioni 348.92**. Kazi zilizofanyika hadi sasa ni pamoja na: kuhuisha taarifa ya Upembuzi Yakinifu ili kujumuisha njia ya kusafirisha umeme kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha JNHPP kwenda Mkuranga kupitia Kibiti; na kuendelea na malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha mradi.

**(viii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme
Msongo wa kV 400 kutoka Sumbawanga
hadi Kigoma kupitia Mpanda, na Kituo cha
Kupoza Umeme Mpanda**

52. **Mheshimwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** kutoka Sumbawanga hadi Kigoma kupitia Mpanda yenyeye urefu wa kilometra 480. Gharama za mradi huu zinakadirwa kuwa **Dola za Marekani milioni 200.4** sawa na takriban **Shilingi bilioni 466.15** kwa upande wa njia ya kusafirisha umeme, na **Dola za Marekani milioni 50** kwa upande wa kituo cha kupoza umeme. Kwa sasa Serikali inaendelea na taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mshauri Mwelekezi wa kudurusu taarifa ya Upembuzi Yakinifu (*Upgrade of Feasibility Study*).

**(ix) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme
Msongo wa kV 400 kutoka Iringa hadi
Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma
na Vituo vya Kupoza Umeme vya Kisada,
Iganjo na Tunduma**

53. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** kutoka Iringa kupitia Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga yenyeye urefu wa kilomita 624. Mradi huu unahusisha pia ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Kisada (Iringa), Iganjo (Mbeya), Tunduma

na Sumbawanga. Mradi huu pia unalenga kuunganisha Gridi ya Taifa na nchi za kusini mwa Afrika (*Southern African Power Pool – SAPP*). Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 595** sawa na takriban **Shilingi trilioni 1.38** ambazo zitatolewa na Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Umoja wa Ulaya (EU) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mikataba ya ufadhili wa mradi huu imesainiwa. Kazi zilizotekelawa ni pamoja na kuhuisha taarifa za Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii; kuandaa nyaraka za malipo ya fidia katika maeneo ya Iringa hadi Mbeya; na kutangaza zabuni za awali (*pre-qualification*) kwa ajii ya kuwapata Wakandarasi wa mradi.

- (x) **Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme
Msongo wa kV 220 kutoka Shinyanga
hadi Simiyu na Kituo cha Kupoza Umeme,
Imalilo**
54. **Mheshimwa Spika**, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenyeye urefu wa kilomita 109 kutoka Ibadakuli Mkoani Shinyanga hadi Imalilo Mkoani Simiyu pamoja na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Imalilo na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Ibadakuli. Gharama ya mradi inakadirwa kuwa **Shilingi bilioni 75** na unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa **asilimia 100**. Kazi zilizotekelawa kwa mwaka 2021/22 ni pamoja na kukamilisha usanifu wa awali wa kituo cha kupoza umeme cha Imalilo na upimaji wa njia kutoka Shinyanga hadi Simiyu; kuanza taratibu za manunuzi ya vifaa vya ujenzi wa jengo la kuongozea mitambo na uzio; na kukamilisha hatua za awali za kufanya Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii.

**(xi) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme
Msongo wa kV 220 kutoka Benaco hadi
Kyaka na Ujenzi wa Kituo cha Kupoza
Umeme cha Benaco na Upanuzi wa Kituo
cha Kupoza Umeme cha Kyaka**

Hotuba ya Waziri wa Nishati

55. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 166.17 kutoka Benaco hadi Kyaka Mkoani Kagera. Mradi huu pia unahusisha ujenzi wa kituo kipywa cha kupoza umeme cha Benaco na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kyaka. Gharama ya mradi inakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 119.4**. Katika mwaka 2021/22 kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha Upembusi Yakinifu; na kuanza kufanya Tathmini ya Mazingira na Jamii.

(xii) **Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 132 kutoka Urambo mkoani Tabora hadi Kidahwe mkoani Kigoma na Ujenzi wa Vituo vya Kupoza Umeme; Urambo, Nguruka na Kidahwe**

56. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 132** yenye urefu wa kilomita 395 kutoka Tabora hadi Kigoma na ujenzi wa vituo vitatu (3) vya kupoza umeme msongo wa **kV 132/33** vya Urambo, Nguruka na Kidahwe pamoja na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Tabora. Gharama za mradi huu ni **Shilingi bilioni 69.7** na unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa **asilimia 100**. Kazi zilizotekelawa hadi sasa ni pamoja na: kukamilisha uwekaji wa mipaka ya mkuza wa njia ya kusafirisha umeme; kukamilisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii; kukamilisha kazi ya uthamini kwa kipande cha Tabora hadi Urambo na kuendelea na kazi ya uthamini kwa kipande cha Urambo hadi Kaliua; kukamilisha ujenzi wa jengo la kuongozea vituo vya kupoza umeme vya Urambo na Nguruka na ujenzi wa uzio; na kuendelea na kazi ya usanifu wa vituo vya kupoza umeme.

(xiii) **Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 132 kutoka Tabora hadi Katavi kuititia Ipole na Inyonga na Vituo vya Kupoza Umeme vya Ipole, Inyonga na Mpanda**

57. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 132** kutoka Tabora hadi Katavi yenye urefu wa kilomita 381 pamoja na ujenzi wa vituo vitatu (3) vya kupoza umeme msongo wa **kV 132/33** vya Ipole, Inyonga na Mpanda. Gharama za mradi huu ni **Shilingi bilioni 64.5** na unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa **asilimia 100**. Kazi zilizotekelawa ni pamoja na kukamilisha uwekaji wa mipaka ya mkuza wa njia ya kusafirisha umeme; kukamilisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii; kuendelea na kazi ya uthamini; kuendelea kusafisha eneo la mradi; kuendelea na usimikaji wa nguzo; kukamilisha ujenzi wa jengo la kuongozea vituo vya kupoza umeme na ujenzi wa uzio; na kuendelea na usanifu wa vituo vya kupoza umeme.

(xiv) **Mradi wa Kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme katika Jiji la Dodoma**

58. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** kutoka Zuzu kwenda Msalato na kutoka Zuzu kwenda Kikombo pamoja na ujenzi wa vituo viwili (2) vinya vya kupoza umeme katika maeneo ya Msalato na Ihumwa Jijini Dodoma. Gharama ya mradi ni **Dola za Marekani milioni 167.7** sawa na takriban **Shilingi bilioni 390.09**. Kazi iliyofanyika ni pamoja na kuhuisha Upembusi Yakinifu; na kuendelea na taratibu za kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

Uwekezaji wa Sekta Binafsi katika Sekta Ndogo ya Umeme

59. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kuititia TANESCO imeendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuendeleza miradi ya umemekama ifuatavyo: kukamilisha majadiliano ya mikataba ya kuuziana umeme na makampuni binafsi yaliyokidhi vigezo vya zabuni iliyotangazwa mwaka 2018, itakayozalisha jumla ya **MW 650** inayotokana na makaa ya mawe (MW 300), upopo (MW 150) na sua (MW 200).

60. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kuitia TANESCO imesaini Hati ya Makubaliano ya Awali (*Memorandum of Understanding - MoU*) na kampuni binafsi ya *Masdar Abu Dhabi Company* ili kuzalisha umeme wa nishati jadidifu kiasi cha **MW 597**. Aidha, TANESCO ipo kwenye mazungumzo ya kukamilisha taratibu za Makubaliano ya Awali na kampuni ya Total-Eren kwa ajili ya kuzalisha umeme wa nishati jadidifu **MW 200** na kampuni ya *Kibo Mining* kwa ajili ya kuzalisha umeme wa makaa ya mawe MW 300. Miradi hii itakapokamilika itaongeza jumla ya **MW 1,747** katika Gridi ya Taifa. Gharama ya miradi hii inakadirwa kuwa takriban **Dola za Marekani milioni 800** sawa na takriban **Shilingi trilioni 1.86**.
61. **Mheshimiwa Spika**, Serikali pia iliendelea kuvutia uwekezaji kwa wazalishaji wadogo wa umeme ambapo wawekezaji wawili (2) wameanza uzalishaji na wanauza umeme kwa TANESCO. Wazalishaji hao ni: Nextgen Solawazi, Kigoma (MW 5 - Umeme Jua); na Luponde Hydro Ltd, Njombe (MW 0.9 - Maji). Aidha, wazalishaji watatu (3) wameshaanza ujenzi amba ni Lung'ali Natural Resources Co. Ltd, Kilolo (MW 1.28 – Maji); Nishati Lutheran DKK Investment Ltd, Makete (MW 0.36 – Maji); na Madope Hydro Co. Ltd, Ludewa (MW 1.7 – Maji). Aidha, wawekezaji watatu (3) amba ni SSI Energy Tanzania Ltd, Kahama (MW 10 – Umeme Jua); Turiani Hydropower Co. Ltd, Mvomero (MW 5 – Maji); na Ninety – Two Limited, Ngorongoro (MW 2 – Maji) wapo katika hatua mbalimbali za kuanza ujenzi. Vilevile, mwekezaji Mapembas (MW 10 – Maji) wa mkoani Njombe yupo katika majadiliano ya mkataba wa kuuziana umeme.

B 4: MIRADI YA KUSAMBAZA UMEME VIJIJINI

62. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kuitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) imeendelea na utekelezaji wa miradi ya nishati vijijini katika mikoa yote ya Tanzania Bara, ikiwa ni pamoja na kuongeza wigo wa Gridi ya Taifa (grid extension); miradi ya kuzalisha umeme ya nje ya gridi ya Taifa (off-grid), inayojumuisha mifumo midogo ya kuzalisha na kusambaza umeme (mini-grids) katika maeneo yenye vyanzo vyta nishati jadidifu (renewable energy sources). Wakala wa Nishati Vijijini pia unatekeleza mradi wa Kupeleka Umeme katika Vijiji-Miji Pembezoni mwa Majiji (Peri-Urban) pamoja na Miradi ya Ujazilizi (*Densification*).
- (i) **Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu (REA III)**
63. **Mheshimiwa Spika**, mradi mkubwa wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu ulilenga kufikisha umeme katika vijiji 7,476 kwa mizunguko miwili (*Round I & II*). Mradi wa Awamu ya Tatu Mzunguko wa Kwanza amba utekelezaji wake ulianza mwaka 2018 ulilenga kupeleka umeme katika maeneo 3,978 ikiwa ni vijiji 3,559 na vitongoji 419 kwa ujenzi wa njia za umeme wa msongo wa kati zenye urefu wa kilomita 15,473, njia za msongo mdogo za usambazaji zenye urefu wa kilomita 15,050.6, kufunga mashineumba 6,155. Mradi uligharimu **Shilingi trilioni 1.157** na kukamilika mwezi Machi, 2022 ambapo jumla ya wateja wa awali 227,561 wameunganishiwa umeme.
64. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili unalenga kupeleka umeme katika vijiji 3,448 vilivysalia katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Lengo la mradi huu ni kujenga miundombinu ya msongo wa kati yenye urefu wa kilomita 28,297, msongo mdogo yenye urefu wa kilomita 3,450, kufunga mashineumba 3,452 na kuunganisha wateja wa awali wapatao 75,622. Gharama

Hotuba ya Waziri wa Nishati

- ya mradi huu ni **Shilingi trilioni 1.24**. Mradi utakapokamilika utawezesha kutimiza azma ya Serikali ya kuvunganishia umeme vijiji vyote vya Tanzania Bara.
65. **Mheshimiwa Spika**, hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu hadi kufikia mwezi Mei, 2022 ni pamoja na: kufanya upimaji na usanifu wa kina katika maeneo yote ya mradi; ununuzi wa vifaa na kuvisafirisha kwenda maeneo ya mradi; na kuanza ujenzi wa miundombinu. Mradi huu awali ulitarajiwा kukamilika mwezi Desemba, 2022 lakini utekelezaji wake umekabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ucheleweshaji wa vifaa kutokana na kuendelea kuwepo kwa masharti ya kudhibiti kusambaa kwa UVIKO 19 katika nchi wakandarasi wanakoagiza vifaa. Aidha, kumekuwa na ongezeko kubwa la bei ya vifaa vya ujenzi wa mradi ikiwemo nyaya na mashineumba ambavyo hutengenezwa kutokana na alumini, chuma na shaba.
66. **Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, Serikali inaendelea na jitihada za kutatua changamoto hizo ili kutimiza azma ya kufikisha umeme katika kila kijiji, ambapo kwa sasa inapitia upya mikataba ya utekelezaji ili kuendana na upandaji wa bei za vifaa.
- (ii) **Mradi wa Peri-Urban katika Mkoa wa Pwani na Wilaya ya Kigamboni, Dar es Salaam (Peri-Urban I)**
67. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulihuisha usambazaji wa umeme katika vijiji - miji vilivyoko katika Mkoa wa Pwani na Wilaya ya Kigamboni - Dar es Salaam, ambao ulinufaisha maeneo 227 ikiwa ni vijiji 36, mitaa 50, vitongoji 76 na maeneo mengine 65. Aidha, utekelezaji wa mradi huu ulihuisha ujenzi wa kilomita 595 za msongo wa kati, kilomita 1,517 za msongo mdogo, ufungaji mashineumba 455 na kuunga wateja wa awali 37,713 kwa gharama ya **Shilingi bilioni 80.5**. Mradi umekamilika na kufanikiwa kufikisha umeme katika maeneo yote yaliyolengwa na mradi.
- (iii) **Mradi wa Peri-Urban katika Mikoa ya Arusha, Dodoma na Mwanza (Peri-Urban II)**
68. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa pili wa Peri-Urban unatekelezwa pembezoni mwa majiji ya Arusha, Dodoma na Mwanza kwa kupeleka umeme katika maeneo 153. Mradi huu unahuisha ujenzi wa kilomita 207 za msongo wa kati, kilomita 544 za msongo mdogo, ufungaji mashineumba 143 na kuunga wateja wa awali 16,328 kwa gharama ya **Shilingi bilioni 31.33**. Hadi kufikia mwezi Mei, 2022, usimikaji wa nguzo umefikia **asilimia 84.4**. na mradi unatarajiwা kukamilika mwezi Desemba, 2022.
- (iv) **Mradi wa Peri-Urban katika Mikoa ya Kagera, Geita, Kigoma, Mbeya, Singida, Tabora na Tanga (Peri-Urban III)**
69. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa Peri-Urban III utatekelezwa pembezoni mwa miji ya Bukoba, Geita, Kigoma, Mbeya, Singida, Tabora na Tanga kwa kupeleka umeme katika maeneo 416. Mradi huu unahuisha ujenzi wa kilomita 447 za msongo wa kati, kilomita 1,020 za msongo mdogo, ufungaji mashineumba 417 na kuunganisha wateja wa awali 22,105 kwa gharama ya **Shilingi bilioni 60**. Kazi iliyofanyika ni kuendelea na taratibu za kuwapata wakandarasi watakaotekaleta mradi.
- (v) **Mradi ya Ujazilizi (Densification)**
70. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unalenga kusambaza umeme katika vitongoji ambavyo vimepitija na njia za umeme msongo wa kati kwa kufunga mashineumba na kujenga njia za umeme msongo mdogo pamoja na kuunga wateja na unatekelezwa kwa mizunguko mitatu (3) ambayo ni 2A, 2B na 2C.
71. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa 2A unahuisha kusambaza umeme katika vitongoji 1,371, ujenzi wa kilomita 5,109.3 za msongo mdogo, ufungaji mashineumba 1,004 na kuunganisha jumla

- ya wateja wa awali 107,215 katika mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Kilimanjaro, Mbeya, Pwani na Tanga. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Machi, 2021 baada ya ufunguzi wa Hati za Muamana (LCs) kwa gharama ya **Shilingi bilioni 117.02**. Hadi kufikia mwezi Mei, 2022, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 84.7** na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Agosti, 2022. Aidha, hadi kufikia mwezi Mei, 2022 vitongoji 913 vilifikasiwa na umeme ambapo wateja wa awali 31,956 wameunganishiwa umeme na mashineumba 714 kati ya 1,004 zimefungwa.
72. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa 2B unahusisha ujenzi wa njia za msongo mdogo wenyе urefu wa kilomita 4,246, kufunga mashineumba 1,277 katika vitongoji 1,686 na kuunganisha jumla ya wateja wa awali 95,334. Mradi huu utatekelezwa katika mikoa 10 ya Arusha, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Morogoro, Njombe, Simiyu na Songwe. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa **Shilingi bilioni 227**. Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na taratibu za ununuzi ili kuwapata wakandarasi watakaotekeliza mradi.
73. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa 2C utahusisha ujenzi wa msongo mdogo wenyе urefu wa kilomita 6,562, kufunga mashineumba 1,932 na kuunganisha wateja wa awali 131,719. Mradi huu utatekelezwa katika vitongoji 1,752 katika mikoa ya Iringa, Manyara, Mara, Mtwara, Rukwa na Ruvuma. Gharama za mradi ni **Shilingi bilioni 381.8**. Katika Mwaka 2022/23, kiasi kitakachotumika ni **Shilingi Bilioni 31.10**, ambapo **Shilingi 14.81** ni kutoka Serikali ya Norway na **Shilingi 16.29** kutoka Serikali ya Tanzania. Mradi huu upo katika hatua za ununuzi ili kuwapata wakandarasi watakaotekeliza mradi
- (vi) **Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha kupoza Umeme cha Ifakara na Kusambaza Umeme Vijijini katika Wilaya za Kilombero na Ulanga**
74. **Mheshimiwa Spika**, mradi unalenga kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme katika wilaya za Kilombero na Ulanga kwa kupanua miundombinu ya kusambaza umeme na kuunganisha wateja. Mradi huu pia utawezesha uendelezaji na uimarishaji wa shughuli za kilimo cha umwagiliaji katika eneo la Southern Agriculture Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT) hivyo kuimarisha kilimo cha kisasa na kuongeza thamani ya mazao. Mradi unahusisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme chenyе ukubwa wa MVA 20 (lot 1) na ujenzi wa njia ya msongo wa kati zenye urefu wa kilomita 82, njia za msongo mdogo zenye urefu wa kilomita 78, kufunga mashineumba 26 na kuunga wateja wa awali 1,350 katika vijiji nane (8) na vitongoji saba (7) katika wilaya za Kilombero na Ulanga (lot 2). Gharama za mradi ni **Shilingi bilioni 23.62** kwa fedha za Serikali na ufadhili wa Umoja wa Ulaya.
75. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Mei, 2022 utekelezaji wa mradi huu umefikia **asilimia 77**. Kazi ambazo zimefanyika katika Lot 1 ni kujenga misingi ya kuwekea mitambo na tayari sehemu kubwa ya mitambo hiyo imeshafika eneo la mradi. Kazi ambazo zimefanyika katika Lot 2 ni kukamilika kwa ufungaji wa mashineumba zote, ujenzi wa msongo mdogo wenyе kilomita 78 na ujenzi wa msongo wa kati wa kilomita 75. Kazi iliyobaki ni kufunga mitambo na ujenzi wa kituo cha kuongozea mitambo (control room).
- (vii) **Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vituo vya Afya na Pampu za Maji ili Kukabiliana na Magonjwa ya Kuambukiza na UVIKO-19**
76. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu kusambaza umeme kwenye vituo vya afya na visima vya maji kwenye Mikoa 23 ya Tanzania

Hotuba ya Waziri wa Nishati

Bara ambapo inatarajiwa vituo vya afya 57, hospitali sita (6) na visima vya maji 363 vitaungwa na huduma ya umeme. Serikali inatekeleza mradi huu ili kuongeza jitihada za kupambana na magonjwa ya kuambukiza ukiwemo UVIKO-19. Gharama za mradi zinakadirwa kuwa **Shilingi bilioni 34.50** na zinatolewa na Umoja wa Ulaya. Katika mwaka 2021/22 kazi iliyofanyika ni kufanya usanifu wa kina wa mradi. Aidha, utekelezaji wa miradi mingine ya kusambaza umeme vijijini umewezesha jumla ya Taasisi 40,408 kuunganishiwa umeme kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 3.**

(viii) **Mradi wa Kupeleka Umeme Vijijini, katika Migodi Midogo, Maeneo ya Viwanda na Maeneo ya Kilimo**

77. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha kupeleka umeme katika maeneo 336 ya uchimbaji madini hususani wachimbaji wadogo, viwanda vidogo na mashamba ya kilimo, lengo likiwa ni kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza thamani ya bidhaa. Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia za msongo wa kati zenye urefu wa kilomita 1,019, njia za msongo mdogo za urefu wa kilomita 382, kufunga mashineumba 271 na kuunganisha wateja wa awali 3,591. Gharama za mradi ni takriban Shilingi bilioni 100 na unagharamiwa na Serikali. Taratibu za ununuzi zinaendelea ili kuwapata Wakandarasi watakaotekeleza mradi huu.

- (ix) **Mradi wa Kusambaza Umeme Maeneo Yaliyo Nje ya Gridi (Off-Grid Projects)**
78. **Mheshimiwa Spika**, Serikali pia inasimamia utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme vijijini katika maeneo yaliyo nje ya Gridi ya Taifa ikiwemo visiwa vyote ambavyo havijafikiwa na huduma za umeme. Mradi unatekelezwa kwa utaratibu wa Ufadhilli wa Malipo kwa Matokeo (Results Based Financing - RBF) na unalenga kukuza Sekta Binafsi katika kutekeleza miradi ya nishati jadidifu kwa maeneo yaliyo nje ya Gridi ya Taifa. Mradi unafadhiliwa na Serikali za Sweden na Uingereza. Jumla ya fedha zilizopangwa kama ruzuku ni **Dola za Marekani milioni 10.80** sawa na **Shilingi bilioni 25.13**.
79. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha awamu ya kwanza (mwaka 2018 hadi 2022), mradi huu ulifadhili miradi 13 yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa jumla ya **MW 9.64** na ulilenga kuunganisha wateja wa awali 20,020. Hadi kufikia mwezi Mei, 2022 wateja walioungwa ni 17,764 sawa na **asilimia 88.73**. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2022.

B 5: UENDELEZAJI WA RASILIMALI YA JOTOARDHI

80. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya Jotoardhi ikiwa ni hatua ya kuhakikisha nchi inakuwa na vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme (Energy Mix). Mpango wa Serikali ni kuzalisha umeme MW 200 ifikapo mwaka 2025 kama ilivyoainishwa katika **Kielelezo Na. 4.**

Kielelezo Na. 4: Mpango wa Uzalishaji Umeme wa Jotoardhi kwa Miradi ya Kipaumbele

Na.	Jina la Mradi	Mwaka wa Kuanza Uzalishaji	Kiwango cha Uzalishaji
1.	Ngozi (Mbeya)	Awamu ya kwanza mwaka 2023	MW 30
		Awamu ya pilli mwaka 2025	MW 40
2.	Songwe (Songwe)	Mwaka 2023	MW 5
3.	Kiejo-Mbaka (Mbeya)	Mwaka 2024	MW 60
4.	Luhoi (Pwani)	Mwaka 2025	MW 5
5.	Natron (Arusha)	Mwaka 2025	MW 60
	Jumla		MW 200

Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

- (i) ***Mradi wa Jotoardhi Ngozi (Mbeya) - MW 70***
81. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unalenga kuzalisha **MW 70** kwa kutumia jotoardhi katika eneo la Ngozi, Mbeya. Kwa sasa, mradi umefikia katika hatua ya uhakiki ambayo inahusisha uchorongaji wa visima vitatu vya uhakiki. Kwa mwaka 2021/22, kazi zilizofanyika ni kukamilisha mkataba wa

ununuzi wa mtambo wa kuchoronga visima hivyo pamoja na taratibu za kuwapata wakandarasi kwa ajili ya kuchoronga visima vya uhakiki na ujenzi wa miundombinu ya barabara na maji.

- (ii) ***Mradi wa Jotoardhi Songwe (Songwe) - MW 5***
82. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu upo mkoani Songwe na unahusu uzalishaji wa umeme (**MW 5**) na matumizi mengine. Hadi kufikia mwezi Mei, 2022, kazi zilizotekelawa ni: kuanza kutumia teknolojia ya Jotoardhi katika utotoleshaji wa vifaranga vya kuku; kukusanya taarifa za kijiolojia kuhusu uendelezaji wa Jotoardhi; kukamilika kwa ujenzi wa bwawa la kuogelea na burudani la majimoto ambalo limeanza kuvutia utalii wa ndani na nje; na kuanza matumizi ya Jotoardhi katika kilimo. Aidha, Serikali inaendelea na taratibu za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya uchorongaji ambazo zinatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2022.
- (iii) ***Mradi wa Jotoardhi Kiejo-Mbaka (Mbeya) - MW 60***
83. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu upo katika Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya na ni mahsus kwa ajili ya uzalishaji wa umeme na matumizi mengine. Utekelezaji wa mradi huu ulianza kwa hatua za utafiti wa awali na unatarajiwa kuanza na uzalishaji wa **MW 10**. Katika mwaka 2021/22, kazi zilizofanyika ni pamoja na kuendelea na ukusanyaji na uchakataji wa taarifa za kisayansi katika visima vya utafiti vilivyo-chorongwa na kuendelea na taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kuandaa na kusimamia kazi ya uchorongaji wa visima vya uhakiki. Aidha, taarifa za awali za kisayansi zilizochakatwa kutoka katika kisima kifupi kimoja cha utafiti ((**KMB-01**) zimeonyesha uwepo wa rasilimali ya Jotoardhi katika eneo la mradi kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 5.**

Kielelezo Na. 5: Kisima Kifupi cha Utafiti cha Jotoardhi (KMB-01) Kilichochorongwa katika Eneo la Mradi wa Kiejo-Mbaka, Wilaya ya Busekelo, Mkoani Mbeya



(iv) **Mradi wa Jotoardhi Natron (Arusha)**

84. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha uzalishaji wa umeme na matumizi mengine. Utekelezaji wa mradi huu umeanza kwa hatua za utafiti wa awali na mradi unatarajiwa kuanza na uzalishaji wa **MW 60**. Kwa sasa mradi huu upo katika hatua ya utafiti. Katika mwaka 2021/22, kazi zilizofanyika ni pamoja na kuendelea kukamilisha taratibu za ufadhili wa mradi kutoka Geothermal Risk Mitigation Facility - GRMF; na kukamilika kwa taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kufanya utafiti.
85. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TGDC inaendelea kufanya tafiti katika maeneo mbalimbali nchini ili kubaini maeneo mapya yenye viashiria vya uwepo wa rasilimali ya jotoardhi, lengo likiwa ni kuongeza mchango wa rasilimali hiyo katika kuzalisha umeme na matumizi mengine. **Kiambatisho Na. 4** kinaonesha Ramani ya Maeneo Mbalimbali yenye Viashiria vya Uwepo wa Rasilimali ya Jotoardhi Nchini.

B 6: KURATIBU, KUSIMAMIA NA KUFUATILIA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIKAKATI MBALIMBALI KATIKA SEKTA NDOGO YA UMEME

Mradi wa Nishati Endelevu kwa Wote (Sustainable Energy for ALL – SE4ALL)

86. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na TANESCO iliendelea na utekelezaji wa Mradi wa Nishati Endelevu kwa Wote (*Sustainable Energy for ALL – SE4ALL*) ambapo zoezi la Upembuzi Yakinifu wa Awali (*Pre-Feasibility Study*) kwa ajili ya eneo la kuzalisha umeme wa jua wa **MW 100** Mkwese, Manyoni, Singida lilikamilika. Aidha, Andiko la kuomba ufadhili kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakinifu wa Kina (*Detailed Feasibility Study*) lilikamilika na Jumuiya ya Ulaya imekubali kufadhili zoezi hilo ambapo maandalizi ya kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kazi hiyo yameanza. Vilevile, upembuzi yakinifu wa awali katika eneo la Kandoto, Wilaya ya Same kwa ajili ya mradi wa **MW 50** umekamilika.

SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

87. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22 Serikali kupitia Wizara ya Nishati, iliendelea kuimarisha na kusimamia Sekta Ndogo ya mafuta na gesi asilia katika maeneo ya utafutaji, uendelezaji, uzalishaji, uchakataji, usafirishaji na usambazaji wa rasilimali hiyo.

B 7: UDHIBITI WA SHUGHULI ZA MKONDO WA JUU WA MAFUTA NA GESI ASILIA

88. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (*Petroleum Upstream Regulatory Authority -PURA*) imeendelea kusimamia shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa gesi asilia kupitia mikataba

- 11 ya Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (*Production Sharing Agreement - PSAs*) kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 5**. Hadi kufikia mwezi Mei, 2022 kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa nchini ni takriban **Futi za Ujazo Triliioni 57.54**. Kati ya kiasi hicho, gesi iliyogunduliwa nchi kavu (*onshore*) ni **Futi za Ujazo Triliioni 10.41** na kwa upande wa bahari kuu (*offshore*) ni **Futi za Ujazo Triliioni 47.13 (Kiambatisho Na. 6)**. Aidha, ramani inayoonesha shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa gesi asilia nchini ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 7**. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2021 hadi mwezi Mei, 2022, uzalishaji wa gesi asilia umeongezeka hadi kufikia **Futi za Ujazo Bilioni 64.42** ikilinganishwa na **Futi za Ujazo Bilioni 53.82** kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2020/21 sawa na ongezeko la **asilimia 20**. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa mahitaji ya gesi asilia katika uzalishaji wa umeme, viwandani, katika taasisi, magari na majumbani hapa nchini. **Kiambatisho Na. 8** kinaonesha uwezo wa uzalishaji wa gesi asilia katika vitalu vya Mnazi Bay na Songo Songo.
89. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, Serikali kupitia PURA imekamilisha uhakiki na ukaguzi wa gharama za Mikataba ya Uzalishaji wa Pamoja na Ugawanaji wa Mapato (PSA) kwa mwaka 2020 na kuanza uhakiki wa gharama na mapato ya Mikataba ya PSA kwa mwaka 2021 ili kuhakikisha Serikali inaendelea kupata stahiki yake kama ilivyokubaliwa katika mikataba iliyopo. Kupitia kaguzi zilizofanyika mwaka 2021/22, **Shilingi bilioni 113.72** zimeokolewa.
90. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia PURA imesimamia kikamilifu ukarabati wa visima vitatu (SS3, SS4 na SS10) vya uzalishaji gesi asilia katika Kitalu cha Songo Songo baada ya visima hivyo kupunguza kiwango cha uzalishaji kutokana na uwepo wa kutu na takataka. Ukarabati wa visima hivyo umekamilika na kwa sasa vinafanyiwa

majaribio kabla ya kuanza uzalishaji wa gesi. Kufuatia ukarabati huo, uzalishaji wa gesi unatarajiwa kuongezeka kwa **Futi za Ujazo Milioni 30** kwa siku.

91. **Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha mwaka 2021/22, PURA imesimamia zoezi la uchukuaji wa data za mitetemo za 3D katika Kitalu cha Ruvu, zoezi ambalo limekamilika mwezi Desemba, 2021. Lengo la ukusanyaaji wa data hizi ni kupata uhakika wa eneo la kuchoronga kisima cha utafutaji wa mafuta na gesi asilia. Shughuli inayoendelea kwa sasa ni kutafsiri na kuhakiki data zilizokusanywa ili kubaini eneo sahihi la kuchimba kisima cha utafutaji. Aidha, PURA inaendelea na usimamizi wa maandalizi ya uchukuaji wa data za mitetemo za 3D katika Kitalu cha Ruvuma ambapo kazi zinazofanyika kwa sasa ni kuandaa mazingira pamoja na kutoa elimu kwa wananchi wanaoishi pembezoni mwa eneo la mradi.

B 8: MIRADI YA UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA KATIKA VITALU VYA KIMKAKATI

- (i) **Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini**
92. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahu utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini kilichopu bahari ya kina kifupi Kusini Mashariki mwa Tanzania. Katika mwaka 2021/22, shughuli zilizotekelzwu katika Kitalu hiki ni pamoja na kusainiwa kwa mkataba kati ya TPDC na Mtaalamu Msimamizi wa Uchorongaji wa visima viwili (2) vya utafutaji na uendelezaji; Mtaalamu Msimamizi kuhuishwa taarifa za kijiolojia na kijifizikia za uchorongaji wa visima, kuandaa taarifa za visima; na kusanifu na kuandaa mpango wa uchimbaji wa visima, kuandaa nyaraka za manunu ya vifaa vya uchorongaji wa visima tajwa. Hatua ya kwanza ya uhuishaji wa taarifa za kijiolojia na kijifizikia imekamilika. Aidha,

Serikali imeshiriki kwenye makongamano mbalimbali ya kimataifa ambapo imenadi kitalu hiki kwa lengo la kupata mbia.

(ii) *Kitalu cha Eyasi – Wembere*

93. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unalenga utafutaji wa mafuta katika kitalu cha Eyasi – Wembere kilichopo kwenye Bonde la Ufa la Afrika Mashariki, Kaskazini Mashariki mwa Tanzania. Hadi kufikia mwezi Mei, 2022 hatua iliyofikiwa ni pamoja na kukamilika kwa Moduli ya mfumo wa 3D iliyotumia data za kijiofizikia iliyowezesha maandalizi ya mpango wa kukusanya taarifa za mitetemo za mfumo wa 2D; kukamilisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira; na kumpata Mkandarasi wa kukusanya na kutafsiri taarifa za kijokemia zitakazoonesha maeneo yanayoweza kupatikana mafuta au gesi asilia.

(iii) *Kitalu cha Songo Songo Magharibi*

94. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika kitalu cha Songo Songo Magharibi. Hadi kufikia mwezi Mei, 2022 kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha ukusanyaji wa data za kijiolojia na kukamilisha tafsiri za data za mitetemo za mfumo wa 2D. Aidha, kazi nyingine iliyofanyika ni kufanya manunuzi ya mshauri mwelekezi wa kuititia taarifa za mfumo wa 2D na kuandaa mpango wa uchorongaji.

(iv) *Vitalu namba 4/1B na 4/1C*

95. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unalenga kufanya utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu namba 4/1B na 4/1C vilivyopo katika bahari kuu kwenye kina kirefu cha maji. Katika mwaka 2021/22, TPDC imefanya tafsiri za data za kijiolojia na kijiofizikia za mfumo wa 2D. Kwa kuwa vitalu hivi vinahitaji uwekezaji mkubwa, Serikali imeshiriki kwenye makongamano mbalimbali ya kimataifa ambapo imevinadi kwa lengo la kupata wabia.

(v) *Kitalu cha Ziwa Tanganyika*

96. **Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kufanya utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika Ziwa Tanganyika (Eneo la Kaskazini) ambapo Kitalu hiki kipo kwenye Bonde la Ufa la Afrika Mashariki, Tanzania. Hadi kufikia mwezi Mei, 2022 kazi zilizotekelawa ni pamoja na kukamilisha kutafsiri data za mitetemo za mfumo wa 2D, kufanya manunuzi ya mkandarasi kwa ajili ya kutengeneza moduli ya mfumo wa 3D kwa kutumia taarifa za uvutano na usumaku (3D modelling of Full Tensor Gravity (FTG) data) pamoja na kuandaa programu na gharama ya kukusanya data za mitetemo za mfumo wa 2D (2D seismic plan and design). Kazi za kutengeneza moduli za 2D za data za FTG imeanza. Kwa kuwa kitalu hiki kinahitaji uwekezaji mkubwa, Serikali imekinadi katika makongamano mbalimbali ya kimataifa kwa lengo la kupata mbia.

(vi) *Kitalu cha Ruvu*

97. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unalenga kufanya utafutaji wa gesi asilia katika kitalu cha Ruu kilichopo Mkao wa Pwani. Hadi kufikia mwezi Mei, 2022 hatua iliyofikiwa ni pamoja na kukamilika kwa ukusanyaji, uchakataji na tafsiri za data za mitetemo za mfumo wa 3D, kwa sasa Mkandarasi yupo kwenye maandalizi ya uchorongaji wa Kisima cha utafiti katika kitalu hicho.

(vii) *Kitalu cha Ruvuma*

98. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unalenga katika utafutaji wa mafuta katika kitalu cha Ruvuma kilichopo Mtwara. Katika kitalu hiki, gesi imegunduliwa katika kisima cha Ntorya 1 na Ntorya 2. Kwa mwaka wa Fedha 2021/22 Mkandarasi anaendelea na ukusanyaji wa data za mitetemo za mfumo wa 3D ili kuhakiki ukubwa wa mashapo yaliyogundulika gesi asilia maeneo mengine na kuandaa taratibu za kuweza kuzalisha gesi iliyogundulika kwa ajili ya mahitaji ya

nchi. Aidha, Mkandarasi pamoja na TPDC wanaandaa mpango wa uzalishaji gesi asilia iliyogundulika.

(viii) Kitalu cha Kilosa-Kilombero

99. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unalenga kufanya utafutaji wa mafuta na gesi katika kitalu cha Kilosa-Kilombero kilichopo Morogoro. Kazi zinazoendelea kwa sasa ni pamoja na kupitia taarifa za mitetemo na maandalizi ya uchorongaji wa Kisima cha utafutaji.

(ix) Kitalu Namba 1 & 4 na Kitalu Namba 2

100. **Mheshimiwa Spika**, vitalu hivi viro baharini katika maji ya kina kirefu na kwa sasa viro katika hatua ya uendelezaji na uzalishaji (Development and Production) wa gesi asilia. Katika vitalu hivi kiasi kikubwa cha gesi asilia kimegundulika kiasi cha takriban Futi za Ujazo Trillion 47.13. Aidha, gesi hiyo ndiyo itakayotumika katika mradi wa kusindika gesi asilia (LNG) utakaojengwa Likong'o, mkoani Lindi. Katika mwaka 2021/22 Serikali, TPDC na Wakandarasi wameendelea na majadiliano ya Mkatuba ya Nchi Hodhi (HGA).

(x) Kitalu cha Songo Songo

101. **Mheshimiwa Spika**, kitalu cha Songo Songo kina leseni ya uendelezaji na uzalishaji wa gesi asilia. Kitalu hiki kimeanza uzalishaji wa gesi asilia mwaka 2004 kutoka katika visima nane (8); SS3, SS4, SS5, SS7, SS9, SS10, SS11 na SS12. Kwa sasa wastani wa futi za ujazo milioni mia moja na thelathini (130mmscfd) kwa siku zinazalishwa. Gesi hii inatumika kwa ajili ya uzalishaji wa umeme, nishati ya uendeshaji wa viwanda, matumizi ya kupikia majumbani na kwenye magari. Kwa mwaka 2021/22, TPDC na Mkandarasi wamekamilisha ufungaji wa komresa na ukarabati wa Visima SS3, SS4 & SS10 ambao umeongeza uzalishaji wa gesi asilia kutoka 105mmscfd mpaka 130mmscfd.

(xi) Kitalu cha Mnazi Bay

102. **Mheshimiwa Spika**, kitalu cha Mnazi Bay kina leseni ya uendelezaji na uzalishaji wa gesi asilia. Kitalu hiki kimeanza uzalishaji wa gesi asilia mwaka 2006 kutoka katika visima vitano (5), Mnazi Bay 1, Mnazi Bay 2, Mnazi Bay 3, Mnazi Bay 4 na MSX 1. Kwa sasa wastani wa futi za ujazo milioni 95 kwa siku (95 mmscfd) zinazalishwa. Gesi hii inatumika kwa ajili ya uzalishaji wa umeme, nishati ya uendeshaji wa viwanda, matumizi ya kupikia majumbani na kwenye magari. Kwa mwaka 2021/22, TPDC na Mkandarasi wamekamilisha ukarabati wa kisima cha MSX 1 na kwa sasa TPDC inatarajia kufanya ukarabati katika Kisima cha Mnazi Bay1 na kutoboa ukanda mpya wa gesi (new zone) kwenye visima MB2, MB3 na MSX1. Ukarababti huu unalenga kuongeza uzalishaji wa gesi asilia kwa matumizi ya umeme, viwandani, majumbani na kwenye magari. **Kielelezo Na. 6** kinabainisha kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa nchini hadi kufikia Mwezi Mei, 2022 kupitia miradi ya utafutaji.

Kielelezo Na. 6: Kiasi cha Gesi Asilia Kilichogunduliwa Nchini hadi Kufikia Mwezi Mei, 2022 kupitia miradi ya utafutaji



Chanzo: **TPDC**

B 9: MRADI WA KUCHAKATA NA KUSINDIKA GESI ASILIA KUWA KIMIMINIKA (LIQUEFIED NATURAL GAS – LNG)

103. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatekelezwa katika eneo la Likong'o mkoani Lindi na unahusu usindikaji wa gesi asilia iliyogunduliwa katika Vitalu Na. 1, 2 na 4 katika kina kirefu cha bahari. Kazi zilizotekelzeza hadi kufikia mwezi Mei, 2022 ni pamoja na uwekaji nguzo za alama katika eneo la mradi; ujenzi wa barabara kuzunguka eneo la mradi; kuendelea na stadi za kisayansi (geoscience) na stadi za mitambo itakayosimikwa katika eneo la mradi; kuendelea kuboreshwa kwa nyenzo zinazotumika katika majadiliano ya Mkataba wa Nchi Hodhi (HGA) kati ya Serikali na wawekezaji; kupatikana kwa Mshauri Mwelekezi ambaye anaishauri Serikali kuhusu masuala ya ufundi, sheria, fedha, biashara na uchumi; na kuendelea na majadiliano ya Mkataba wa HGA kati ya Serikali na Wawekezaji. **Kiambatisho Na. 9** kinaonesha eneo la mradi wa LNG.

B 10: MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI WA GESI ASILIA

(i) *Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani*

104. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kwa njia ya mabomba pamoja na vituo vya kugandamiza gesi asilia (CNG). Kazi zilizotekelzeza ni pamoja na: uunganishwaji wa nyumba 670 katika Mkoa wa Dar es Salaam (Sinza - 225, Police Barracks Kurasini - 345 na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - 100); na kuunganisha kiwanda cha Raddy Fiber Manufacturing Tanzania Ltd kilichopo Mkuranga

mkoani Pwani. Aidha, Serikali iliendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika miradi ya CNG ambapo leseni imetolewa kwa Kampuni ya ANRIC Gas Technologies Company. **Kiambatisho Na. 10** kinaonesha shughuli za usambazaji gesi asilia katika Mkoa wa Dar es Salaam.

(ii) *Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa ya Lindi na Mtwara*

105. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia kwa njia ya mabomba katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Katika mwaka 2021/22 Serikali kupitia TPDC ilikamilisha ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia majumbani yenye urefu wa kilomita 18.3 iliyounganisha nyumba za awali 209 katika Kata za Mnazi Mmoja na Mingoyo mkoani Lindi. **Kiambatisho Na. 11** kinaonesha shughuli za usambazaji gesi asilia katika Mkoa wa Lindi.

106. **Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla urefu wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia nchini umeongezeka kutoka kilomita 129.64 mwaka 2020/21 hadi kufikia kilomita 154.79 mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la **asilimia 19.40. Kiambatisho Na. 12** kinaonesha mchangano wa urefu wa miundombinu hiyo.

(iii) *Mradi wa Usambazaji wa Gesi Asilia nchini kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini Unaosimamiwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA)*

107. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unalenga kusambaza nishati ya gesi asilia katika maeneo ya vijijini. Kutokana na ukubwa wa gharama za miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia, TPDC na REA wamekubaliana kutumia Mfuko wa Nishati Vijijini kuwekeza kwenye ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi kwa kuanza na vijiji vilivyo karibu na miundombinu iliyopo katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani. **Napenda**

- kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, pamoja na jukumu kubwa la kuharakisha upatikanaji wa umeme vijijini na vitongojini, REA imeanza usambazaji wa gesi asilia vijijini, kwa lengo la kuhakikisha wananchi wa maeneo hayo wanakuwa na vyanzo mbadala vya nishati na hivyo kupunguza matumizi ya nishati isiyo rafiki kwa mazingira.** Katika mwaka 2021/22 kazi zilizofanyika ni kukamilisha tafiti za masoko kwa maeneo ya Kisemvule (Mkuranga - Pwani) na Mnazi Mmoja (Lindi) ili kubaini wateja wa gesi walipo na kuandaa usanifu wa kihandisi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia.
- (iv) **Mradi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia Kutoka Tanzania hadi Uganda**
108. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahu unahu ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Tanzania hadi Uganda. Mradi unalenga pia kusambaza gesi asilia katika maeneo yatakayopitiwa na bomba hilo. Kufuatia kusainiwa kwa Makubaliano ya Awali (*Memorandum of Understanding – MoU*) kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda mwezi Agosti 2018, Serikali zote mbili ziliunda Kamati ya Pamoja ya Wataalamu (*Joint Technical Committee - JTC*), Kamati ya Pamoja ya Uongozi (*Joint Steering Committee*) na Kamati ya Mradi ya Mawaziri (*Joint Project Committee*). Mwezi Mei, 2022, Kamati hizi zilikutana, zikapitia na kuidhinisha nyaraka mbalimbali ambazo ni pamoja na Rasimu ya Mkataba Mahsus (*Draft Bilateral Agreement*) ambao utakaposainiwa utatoa mwongozo wa utekelezaji wa mradi hususani namna ya kumpata mshauri elekezi wa kufanya upembuzi yakinifu wa mradi.
- (v) ***Mradi wa Kusafirisha Gesi Asilia Kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Mombasa (Kenya)***
109. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahu unahu kusafirisha gesi asilia kutoka Dar es Salaam kwenda Mombasa na utekelezaji wake unatarajiwa kunufaisha pia Mikoa ya Pwani, Tanga, Arusha na Kilimanjaro kwa kuwezesha upatikanaji wa gesi asilia katika mikoa hiyo ambayo itapitiwa na bomba la kusafirisha gesi na mikoa mingine ya jirani. Makubaliano ya Awali kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kenya yalisainiwa tarehe 4 Mei, 2021 na tayari Serikali zote mbili zimeunda Kamati ya Pamoja ya Wataalam; Kamati ya Pamoja ya Uongozi na Kamati ya Pamoja ya Mawaziri ili kusimamia na kuharakisha utekelezaji wa mradi.
110. ***Mheshimiwa Spika***, Timu ya Pamoja ya Wataalam kutoka nchi hizo mbili imeshakutana na kuandaa Mpango Kazi wa Mradi pamoja na kufanya maandalizi ya Upembuzi Yakinifu. Kukamilika kwa mradi huu kunatarajiwa kuwa na manufaa makubwa kwa Taifa letu ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa mapato ya Serikali pamoja na ajira. Aidha, mradi utachochea uendelezaji wa gesi asilia iliyogunduliwa nchini na vilevile kutoa fursa kwa tafiti zaidi kufanyika kutokana na kupatikana kwa soko la uhakika.

Hotuba ya Waziri wa Nishati

B 11: MIRADI YA KUHIFADHI NA KUSAFIRISHA MAFUTA

Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima - Uganda hadi Tanga - Tanzania (East African Crude Oil Pipeline - EACOP)

111. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) likiwa na urefu wa kilomita 1,443 ambapo kati ya hizo kilomita 306 zitakuwa Uganda na kilomita 1,137 zitakuwa Tanzania. Katika mwaka 2021/22 kazi zilizotekelzwa ni pamoja na: kutoa elimu kwa wananchi hususan katika maeneo yanayopitiwa na mradi kuhusu utekelezaji na fursa za mradi; kukamilika kwa malipo ya fidia katika maeneo 14 ya kipaumbele yatakayojengwa kambi za wafanyakazi, hifadhi za vifaa vya ujenzi wa mradi na karakana ya kupokea na kupaka rangi mabomba (*coating yard*).

112. **Mheshimiwa Spika**, kazi nyingine zilizotekelzwa ni kuanza kwa shughuli za awali za ujenzi katika eneo kitakapojengwa kiwanda cha kuwekea plastiki kwenye mabomba katika eneo la Sojo Wilayani Nzega; na kufikiwa kwa uamuzi wa mwisho wa uwekezaji na Kampuni ya EACOP mwezi Februari, 2022. Aidha, Serikali tayari imetoa jumla ya **Shilingi Biliioni 259.96** ikiwa ni sehemu ya malipo ya umiliki wa Serikali wa **asilimia 15** katika mradi kupitia TPDC. **Kiambatisho Na. 13** kinaonesha Ramani ya Njia ya Bomba la Mafuta la Mradi wa EACOP.

113. **Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine, maandalizi ya ulipaji fidia kwa wananchi wanaopisha mkuza wa ujenzi wa bomba yamekamilika ambapo zoezi la kutoa elimu ya mikataba ya fidia limeanza kwa mikoa yote itakayopitiwa na bomba (Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Manyara, Singida, Dodoma na Tanga). Jumla ya wananchi 9,122 wanatarajiwa kupatiwa elimu, kusaini mikataba ya fidia na kulipwa fidia kwa mujibu wa Sheria.

B 12: SHUGHULI ZA UAGIZAJI NA UPATIKANAJI WA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI NCHINI

- (i) *Ushiriki wa TPDC katika Biashara ya Mafuta kupitia TANOIL*
114. **Mheshimiwa Spika**, kuanzia mwezi Machi, 2021 TPDC kupitia kampuni yake tanzu ya TANOIL imekuwa ikishiriki katika biashara ya mafuta kwa kununua na kuuza mafuta kwa wateja mbalimbali nchini. Hadi kufikia mwezi Mei, 2022, kiasi cha **lita milioni 113.20** na **138.10** za petroli na dizeli mtawalia ziliuzwa. Aidha, kutokana na mwenendo mzuri wa biashara, mtaji wa **Shilingi biliioni 76.21** uliotolewa na TPDC kwa TANOIL kwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari, 2021 hadi mwezi Machi, 2022 umeimarika na kufikia **Shilingi biliioni 596.83**.
- (ii) *Ushiriki wa TPDC katika Biashara ya Mafuta kupitia Mfumo wa Uagizaji kwa Pamoja (Bulk Procurement System - BPS)*
115. **Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta nchini, kuanzia mwezi Oktoba, 2021 Serikali kupitia TPDC ilianza kushiriki katika zabuni za uagizaji wa bidhaa za mafuta kupitia Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (BPS). Kupitia mfumo huo, hadi kufikia mwezi Machi, 2022 TPDC imeweza kushiriki na kushinda zabuni tatu (3) za uagizaji wa mafuta ya dizeli pekee. Kati ya zabuni hizo, mbili ni za mwezi Oktoba, 2021 zilizowezesha uagizwaji wa tani 202,789 ambazo zilipokelewa mwezi Desemba, 2021 na zabuni moja ya mwezi Februari, 2022 imeweza uagizwaji wa tani 111,762 zilizopokelewa mwishoni mwa mwezi Aprili, 2022.

B13: USHIRIKIANO WA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA (SMT) NA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR (SMZ) KATIKA UENDELEZAJI WA SEKTA YA NISHATI

116. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kuimarisha Muungano kati ya Tanzania Bara na Zanzibar, Wizara zenye dhamana ya masuala ya nishati za pande zote mbili zimeendelea kufanya vikao mbalimbali vya mashirikiano vinavyolenga kuendeleza Sekta ya Nishati katika pande mbili za Muungano. Katika kutekeleza azma hiyo, mwezi Februari, 2022 Taasisi za TPDC na ZPDC, PURA na ZPRA pamoja na EWURA na ZURA zilisaini Hati za Makubaliano ya Mashirikiano (Memorandum of Understanding - MoU) kuhusu ushirikiano wa kitaalamu katika tasnia ya umeme, mafuta na gesi, hususan katika kujengeana uwezo wa kitaalam, utunzaji wa data na ubadilishanaji wa maarifa na taarifa mbalimbali. Utekelezaji wa makubaliano hayo unaendelea.

B 14: MRADI WA KUJENGA UWEZO WA KUSIMAMIA NA KUENDELEZA RASILIMALI ZA NDANI NA UTAWALA WA RASILIMALI ZA ASILI TANZANIA

117. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu ulianza kutekelezwa mwezi Juni, 2017 kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB). Gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 29.54** ambapo Mfuko wa Maendeleo wa Afrika unachangia **Dola za Marekani milioni 26.59** sawa na takriban **Shilingi bilioni 61.85** na Serikali ya Tanzania inachangia **Dola za Marekani milioni 2.95** sawa na takriban **Shilingi bilioni 6.86**. Lengo la mradi ni kuzijengea uwezo taasisi za Serikali zinazosimamia rasilimali ya gesi asilia pamoja na ukusanyaji wa mapato. Taasisi

zinazonufaika na mradi huu ni pamoja na Wizara ya Nishati, TPDC, PURA, ZURA, EWURA, TRA, TRA-Zanzibar, ZRB na NEEC.

118. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2021/22, Wizara na Taasisi nufaika za mradi zimeendelea kupata ufadhili wa mradi katika mafunzo ya muda mfupi ambapo jumla ya watumishi 220 walipata mafunzo ikijumuisha watumishi 40 wa TPDC, Watumishi 29 wa Wizara ya Nishati, Watumishi 21 wa PURA na Watumishi 130 wa TRA. Aidha, mradi umeweza kununuliwa kwa vitendea kazi mbalimbali kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa taasisi nufaika za mradi. Vifaa hivyo vinahusisha kituo cha kutunza takwimu za utafiti na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia chini ya PURA, vifaa vya kuhodhi mfumo wa uondoshaji shehena mipakani (*Tanzania Eletronic Single Window System*) na midaki (*scanner*) miwili iliyofungwa ndani ya Bandari ya Dar es Salaam chini ya TRA. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2023.

B 15: HALI YA UAGIZAJI NA UPATIKANAJI WA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI NCHINI

119. ***Mheshimiwa Spika***, uagizaji wa mafuta nchini umepitia hatua mbalimbali ambapo hadi kufikia mwaka 1977, kampuni za kigeni zilizokuwa zinafanya biashara ya mafuta nchini zilikuwa zinaagiza mafuta kujazia kiasi kilichopungua katika mafuta yaliyosafishwa kwenye mtambo (*refinery*) wa TIPER. Ilipofika mwaka 1982 Serikali ilielekeza TPDC pekee iagize mafuta yote (safi na ghafi) kutohana na udanganyifu uliobainika. Hivyo, kati ya mwaka 1982 hadi mwaka 1997, Sekta Ndogo ya Mafuta ilidhibitiwa na Serikali kuitia TPDC ambapo Serikali ilikuwa ikipitia na kupanga bei ya mafuta kulingana na gharama halisi.

120. **Mheshimiwa Spika**, katika miaka ya 1990 Serikali ilianzisha Sera ya Uchumi Huria na hivyo kutunga Kanuni za Mpito za Mafuta (*Interim Petroleum Regulations*) kwa lengo la kuboresha hali ya upatikanaji wa mafuta nchini kwa bei nafuu pamoja na kuvutia uwekezaji katika sekta ya mafuta. Utekelezaji wa Sera hii ulianza kwa kuruhusu TPDC kuendelea kuagiza mafuta ghafi, kuyasafisha katika kiwanda cha TIPER kisha kuuza kwa Kampuni za Biashara ya Mafuta (OMCs) na pia kuruhusu OMCs kujaziliza upungufu kwa kuagiza mafuta kutoka nje ya nchi. Kuanzia mwezi Januari, 2000 Kampuni za Mafuta ziliruhusiwa kuagiza mafuta ya kutosheleza mahitaji ya nchi na kupanga bei za mafuta hayo kulingana na hali ya ugavi na uhitaji (*demand and supply*).

121. **Mheshimiwa Spika**, sera ya Soko Huria ilihamasisha uwekezaji katika miundombinu lakini zilijitokeza changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na: miundombinu iliyojengwa kutokidhi viwango vilivyowekwa; ukwepaji kodi kuitia udanganyifu wa kiasi na aina ya mafuta pamoja na kuuza mafuta ya transit katika soko la ndani; uchakachua ji dizeli kwa kutumia mafuta ya taa; Kampuni za Mafuta kuuza mafuta kwa bei ya juu kuliko għarama halisi; għarama kubwa za uagizaji (*premium*) zilizokuwa na wastani wa **Dola za Marekani 83 kwa tani**; na kuongezeka muda wa meli kusubiri kupakua mafuta (*demurrage*) kutokana na shehena ndogo ndogo za kuanzia tani 5,000 hadi tani 10,000 kwa meli zilizopeleka għarama za *demurrage* kufikia wastani wa **Dola za Marekani 45 kwa tani**.

122. **Mheshimiwa Spika**, kati ya mwaka 2004 na mwaka 2008, Serikali ilifanya marekebisho ya sheria ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katia Sekta Ndogo ya Mafuta kwa lengo la kumlinda mlaji na kudhibiti ukwepaji kodi. Sheria hii iliekeleza kuwa mafuta yote yatakayotumika nchini lazima ununuzi wake ufanyike kwa ufanisi (*Efficient Procurement of Petroleum Products*). Katika utekelezaji wa Sheria hiyo, Kanuni ya The


Petroleum (Bulk Procurement), Regulations 2011 ilitungwa na hivyo kuruhusu Mfumo wa Uagizaji wa Pamoja (*Bulk Procurement System - BPS*) wa Mafuta kuanza kutumika mwezi Januari, 2012.

123. **Mheshimiwa Spika**, mfumo wa BPS umekuwa na manufaa kadhaa kwa nchi yetu ikiwa ni pamoja na kupungua kwa għarama za uagizaji (*premium*) na għarama za meli kusubiri kushusha mafuta (*demurrage costs*) ambapo kabla ya kuanza mfumo huu għarama hizo zilikuwa ni wastani wa **Dola za Marekani 83 kwa tani** (*premium*) na **Dola za Marekani 45 kwa tani** (*demurrage costs*). Katika kipindi cha mwezi Julai, 2021 hadi mwezi Aprili, 2022 wastani wa għarama za uagizaji ilikuwa ni **Dola za Marekani 32.06 kwa tani** na meli kusubiri **Dola za Marekani 2.69 kwa tani**, hivyo katika kipindi hiki cha miezi kumi (10) mfumo wa BPS umeokoa jumla ya **Dola za Marekani milioni 413.20** sawa na takriban **Shilingi bilioni 961.15**. Għarama hizi huongeza bei ya mafuta kwa mlaji wa mwisho. Aidha, mfumo huu pia unawezesha uhakika wa upatikanaji wa mafuta yanayotosheleza mahitaji ya nchi wakati wote; udhibiti wa ubora wa mafuta; kuondoa vikwazo vyā kibiashara na kuweka usawa wa mazingira ya kufanya biashara ya mafuta; na upatikanaji wa takwimu sahihi za mafuta kwa ajili ya ukokotoaji wa kodi na tozo mbalimbali.

124. **Mheshimiwa Spika**, usimamizi mzuri wa BPS unaofanywa na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) umeendelea kuimarisha udhibiti wa upotevu wa mafuta wakati wa upokeaji kutoka kwenye meli kwa kuendelea kuboresha taratibu za ukaguzi na usimamizi. Hatua hii imewzesha kupunguza kiwango cha upotevu wa mafuta wakati wa upakuaji kutoka wastani wa **asilimia 0.3** hapo awali hadi kufikia wastani wa **asilimia 0.09** kwa sasa. Ufanisi huu unawezesha **kuokolewa kila mwezi wastani wa tani 966 za mafuta yenye thamani ya takriban shilingi bilioni 2.25. Kielezezo Na. 7** kinaonesha mwenendo

wa udhibiti wa upotevu wa mafuta wakati wa upakuaji mafuta kutoka kwenye meli kuanzia mwaka 2012 hadi mwaka 2021. Vilevile, katika uboreshaji udhibiti wa upakuaji mafuta kutoka kwenye meli, Serikali kuitia TPA imenunua na kusimika mita za kupima mafuta za teknolojia ya kisasa katika bandari za Tanga, Mtwara na Dar es Salaam - KOJ. Aidha, Serikali kuitia EWURA imezielekeza kampuni zinazomiliki maghala ya mafuta kufunga mita za kupima mafuta katika mabomba yote yanayoingia kwenye maghala yao ili kuhakikisha mafuta yanapokelewa sehemu iliyokusudiwa.

Kielelezo Na. 7: Mwenendo wa Udhibiti wa Upotevu wa Mafuta Wakati wa Upakuaji Mafuta Kuanzia mwaka 2012 hadi mwaka 2021



125. **Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha mwezi Julai, 2021 hadi Aprili, 2022, jumla ya **lita bilioni 6.43** za bidhaa za petroli ziliingizwa nchini ikilinganishwa na **lita bilioni 5.37** zilizoingizwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2020/21 sawa na ongezeko la **asilimia 19.70** linalotokana na kukua kwa mahitaji ya mafuta ndani ya nchi pamoja na nchi jirani kuongeza uagizaji wa mafuta kuitia mfumo wa BPS. Kiasi cha mafuta kilichoingizwa kwa ajili ya matumizi ya ndani ni **lita bilioni 3.45** sawa na **asilimia 53.6** ya kiasi chote kilichoingizwa nchini na **lita bilioni 2.98** sawa na **asilimia 46.4** zilipitishwa kwenda nchi jirani kama inavyoonekana katika **Vielelezo Na. 8 na 9**.
126. **Mheshimiwa Spika**, japokuwa ni hiari kisheria kwa mafuta yapitayo nchini kwenda nchi jirani kuitishwa katika Mfumo wa Uagizaji wa Pamoja, lakini zaidi ya asilimia 95 ya mafuta yaliyopita kwenda katika nchi hizo yalitumia mfumo huu kutokana na ufanisi mzuri. Mwenendo wa uagizaji wa bidhaa za mafuta kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 ni kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 10**. Aidha, **Kielelezo Na. 11** kinaonesha jumla ya kiasi cha mafuta kilichoagizwa kwa kila aina ya bidhaa katika kipindi hicho. Vilevile, **Kielelezo Na. 12** kinaonesha mwenendo wa mafuta yaliyoingizwa nchini katika kipindi cha miaka saba (7) iliyopita, yaani mwaka 2015 hadi mwaka 2021.

Hotuba ya Waziri wa Nishati

Kielelezo Na. 8: Mafuta Yaliyoingizwa Mwezi Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 kwa Matumizi ya Ndani

Mwezi	Dizeli (Lita)	Petroli (Lita)	Mafuta ya Taa (Lita)	Mafuta ya Ndege (Lita)	Mafuta Mazito (Lita)	Jumla (Lita)
Jul-2021	225,611,919	80,670,818	2,799,742	12,187,114	-	321,269,592
Ago-2021	203,334,489	143,327,449	1,697,750	6,644,374	-	355,004,062
Sep-2021	194,972,502	173,155,261	255,025	6,614,649	-	374,997,438
Okt-2021	134,979,622	124,829,777	1,943,757	29,275,695	-	291,028,851
Nov-2021	179,115,883	66,188,599	975,000	19,249,162	-	265,528,643
Des-2021	150,406,955	171,194,399	1,160,413	18,677,605	-	341,439,372
Jan-2022	207,605,458	141,983,154	1,254,896	15,994,338	-	366,837,846
Feb-2022	159,633,557	131,201,034	1,268,976	11,229,485	-	303,333,052
Mac-2022	143,821,348	109,475,813	825,781	13,349,603	-	267,472,545
Apr-2022	196,346,364	108,737,235	195,000	11,206,000	-	316,484,598
Jumla Mafuta Yaliyoagizwa	1,795,828,097	1,250,763,539	12,376,340	144,428,025	-	3,203,396,001
Mafuta yaliyobadilishwa matumizi (Localized)	150,877,021	88,413,292	1,826,527	1,336,395	-	242,453,235
Jumla ya Mafuta kwa Matumizi ya Ndani	1,946,705,118	1,339,176,831	14,202,867	145,764,420	-	3,445,849,236


Chanzo: **PBPA na TRA**

Kielelezo Na. 9: Mafuta Yaliyoingizwa Kuanzia Mwezi Julai, 2021 Hadi Aprili, 2022 Kwenda Nchi Jirani

Mwezi	Dizeli	Petroli	Mafuta ya Ndege/Taa	Mafuta Mazito	Jumla
Jul-2021	256,912,770	96,469,310	11,590,107	8,397,797	373,369,984
Aug-2021	209,628,005	110,784,584	10,523,234	-	330,935,824
Sep-2021	217,898,941	145,037,388	8,894,057	-	371,830,387
Okt-2021	148,973,780	94,087,337	38,517,330	-	281,578,447
Nov-2021	201,839,329	85,193,248	17,582,500	-	304,615,077
Des-2021	138,350,650	110,775,552	17,310,552	-	266,436,754
Jan-2022	196,682,996	131,653,546	15,678,724	-	344,015,265
Feb-2022	154,216,641	131,201,034	12,498,461	-	297,916,136
Mar-2022	160,049,318	110,427,222	20,028,419	-	290,504,959
Apr-2022	235,098,826	113,456,701	14,831,700	-	363,387,226
Jumla mafuta yaliyoingizwa (Transit)	1,919,651,256	1,129,085,922	167,455,085	8,397,797	3,224,590,059
Mafuta yaliyobadilishwa matumizi (Localized)	150,877,021	88,413,292	3,162,922	-	242,453,235.13
Jumla ya Mafuta ya Kwenda Nchi Jirani	1,768,774,235	1,040,672,631	164,292,162	8,397,797	2,982,136,824


Chanzo: **PBPA na TRA**

Kielelezo Na. 10: Mwenendo wa Uagizaji wa Bidhaa za Mafuta kwa Kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022



Kielelezo Na. 11: Jumla ya Kiasi cha Bidhaa za Mafuta Kilichoagizwa kwa Kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022

AINA YA MAFUTA	KIASI KILICHOAGIZWA (TANI)
DIZELI	2,880,150
PETROLI	1,603,937
MAFUTA YA NDEGE / TAA	202,936
JUMLA	4,687,023



Hotuba ya Waziri wa Nishati

Kielelezo Na. 12: Mwenendo wa Uagizaji wa Mafuta Kuanzia 2015 Hadi 2021

Mwaka	Mafuta Yaliyoagizwa kwa Matumizi ya Ndani	Mafuta Yaliyoagizwa kwenda Nchi Jirani	JUMLA
2015	3,338,097,164	1,825,467,870	5,163,565,034
2016	3,302,298,898	2,185,151,066	5,487,449,964
2017	3,193,252,759	2,168,192,874	5,361,445,632
2018	3,264,785,479	2,440,025,165	5,704,810,644
2019	3,537,891,891	2,615,679,703	6,153,571,595
2020	3,532,619,144	2,287,292,015	5,819,911,159
2021	3,781,254,741	3,149,225,882	6,930,480,623



Chanzo: **PBPA na TRA**

127. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwezi Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 jumla ya zabuni 90 zilitolewa kupitia zabuni shindanishi za kimataifa zinazofanyika kila mwezi ambazo ni wastani wa zabuni 9 kwa mwezi. Jumla ya wazabuni 13 walishiriki katika zabuni hizo na kushinda kwa nyakati tofauti. Kati ya wazabuni hao watano (5) ni kampuni zilizosajiliwa ndani ya nchi.

128. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwezi Julai, 2021 hadi mwezi Aprili, 2022 wastani wa gharama za kuleta mafuta nchini (*weighted average premium*) zilikuwa ni **Dola za Marekani 32.06** kwa tani ambayo ni sawa na ongezeko la **asilimia 8.1** ikilinganishwa na **Dola za Marekani 29.46** kwa tani katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2020/21. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji wa mafuta. Aidha, katika kipindi hicho gharama za meli kusubiri kushusha mafuta (*demurrage charges*) zilikuwa ni **Dola za Marekani 2.69** kwa tani sawa na unaifuu wa **asilimia 24.2** ikilinganishwa na **Dola**

za Marekani 3.34 kwa tani katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2020/21. Kupungua kwa gharama hizi kunatokana na mpangilio makini wa meli zinazoleta mafuta pamoja na usimamizi mzuri wakati wa upakuaji mafuta kutoka melini.

129. **Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua umuhimu wa matumizi ya teknolojia katika shughuli za upakuaji mafuta kutoka kwenye meli, Serikali kupitia PBPA imekamilisha taratibu za ununuzi wa **Mfumo wa Kusoma Mita Zote za Kupima Mafuta Wakati Wote (24/7)**. Mfumo huo ujulikanao kwa jina la *Supervisory Control and Data Acquisition (SCADA)* utasoma mita zote zinazomilikiwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania pamoja na mita zote zinazopima mafuta yanayoingia katika maghala ya Kampuni za Mafuta (OMCs). Kuwepo kwa mfumo huu kutawezesha ufuutiliaji mubashara wa upakuaji mafuta kutoka kwenye meli kwenda katika maghala ya mafuta na kugundua/kutahadharisha kwa haraka panapotokea ukiukwaji wa taratibu za upakuaji mafuta

kutoka kwenye meli. Hivyo, mfumo huu utahakikisha kuwa mafuta yanapokelewa katika maghala yaliyokusudiwa kwa wakati wote. Wakandarasi wa kutekeleza mradi huu wamepatikana na ufungaji wa mfumo huo unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2023.


130. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) ipo katika mpango wa maboresho ya miundombinu ya kuhudumia meli na shehena zote ikijumuisha bidhaa za mafuta ya petroli ambapo katika mpango wa muda mfupi TPA inakamilisha ununuizi wa mkandarasi atakayefanya kazi ya ukarabati wa gati la kupokelea mafuta la Kurasini (KOJ) katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023. Aidha, katika mpango wa muda mrefu, TPA inatarajia kukamilisha Upembuzi Yakinifu na Tathmini ya Athari kwa Mazingira ya mradi wa ujenzi wa kituo cha kupokelea mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam (*Single Receiving Terminal – SRT*) kabla ya kumalizika kwa mwaka 2021/22. Utekelezaji wa mpango huu utaongeza uwezo wa miundombinu ya bandari wa kupokea mafuta mengi kwa wakati mmoja.

B 16: MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA

131. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2021 hadi mwezi Aprili, 2022, wastani wa bei ya mafuta ghafi katika soko la dunia ilikuwa **Dola za Marekani 85.68** kwa pipa ikilinganishwa na wastani wa **Dola za Marekani 51.58 (Kielelezo Na.13)** kwa pipa kwa kipindi kama hicho mwaka 2020/21, sawa na ongezeko la **asilimia 66**. Kuongezeka kwa bei kulitokana na kuongezeka kwa kasi ya mahitaji ya mafuta kulikosababishwa na kurejea kwa shughuli za kiuchumi katika nchi mbalimbali duniani ambazo zilisitishwa kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19. Vilevile, pamoja na kuendelea kuongezeka kwa mahitaji ya mafuta duniani, mgogoro wa kivita kati ya Urusi na Ukraine umefanya upungufu wa mafuta uongezeke baada ya nchi za Ulaya na Marekani kuweka vikwazo vya kiuchumi dhidi ya Urusi ambayo huchangia takriban **asilimia 12** ya uzalishaji wa mafuta duniani. **Kielelezo Na.14** kinaonesha Mwenendo wa Bei ya Mafuta Ghafi mwaka 2020/21 na 2021/22.

Hotuba ya Waziri wa Nishati

Kielelezo Na. 13: Wastani wa Bei ya Mafuta Ghafi katika Soko la Dunia Mwaka 2020/21 na Mwaka 2021/22




Kielelezo Na. 14: Mwenendo wa Bei ya Mafuta Ghafi mwaka 2020/21 na 2021/22

Mwezi	Bei za Mafuta Ghafi (Dola/Pipa)	
	2020/21	2021/22
Julai	43.22	74.25
Agosti	45.02	70.38
Septemba	43.36	74.88
Oktoba	41.52	83.71
Novemba	43.98	80.85
Desemba	50.22	74.80
Januari	55.28	85.57
Februari	62.20	94.10
Machi	65.70	112.46
Aprili	65.31	105.81
Wastani wa Bei katika Mwaka	51.58	85.68
Asilimia ya Ongezeko la Bei (%)	66%	

132. Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa bei ya mafuta ghafi katika soko la Dunia kwa mwaka 2021/22 kulipelekea kuongezeka kwa bei ya mafuta yaliyosafishwa ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2022, wastani wa bei ya mafuta yaliyosafishwa katika soko la dunia ilikuwa **Dola za Marekani 825, 751**, na 748 kwa tani kwa mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa/ndege mtawalia, ikilinganishwa na wastani wa **Dola za Marekani 452,400** na 386 kwa tani kwa kipindi kama hicho mwaka 2020/21. Hii ni sawa na ongezeko la **asilimia 83, 88** na **94** kwa mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa/ndege mtawalia. **Kielelezo Na.15** kinaonesha Mwenendo wa Bei za Mafuta yaliyosafishwa katika Soko la Dunia kwa Mwaka 2021/22.

Kielelezo Na.15: Mwenendo wa Bei za Mafuta yaliyosafishwa katika Soko la Dunia



133. **Mheshimiwa Spika**, kama ilivyokuwa kwa bei ya mafuta ghafi na yaliyosafishwa, bei za mafuta katika soko la ndani kwa mafuta yaliyopokelewa kupitia Bandari ya Dar es Salaam nazo ziliongezeka kwa mwaka 2021/22. Wastani wa bei za mafuta kwa Mkoa wa Dar es Salaam kuanzia mwezi Julai, 2021 hadi mwezi Mei, 2022 kwa lita moja ilikuwa kama ifuatavyo: petroli Shilingi 2,562, dizeli Shilingi 2,421 na mafuta ya taa Shilingi 2,337 ikilinganishwa na wastani wa bei za mafuta hayo kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2020/21 ambazo zilikuwa petroli Shilingi 1,910, dizeli Shilingi 1,815 na mafuta ya taa Shilingi 1,723 sawa na ongezeko la asilimia 34, 33 na 36 mtawalia. Kielelezo Na.16 kinaonesha wastani wa Mwenendo wa Bei za Mafuta katika Soko la Ndani kwa Mwaka 2021/22.

Kielelezo Na.16: Wastani wa Mwenendo wa Bei za Mafuta katika Soko la Ndani kwa Mwaka 2021/22

134. **Mheshimiwa Spika**, kama ilivyobainishwa hapo juu, bei za mafuta hapa nchini zinatokana na bei zilizopo katika soko la dunia ambazo nchi yetu haina uwezo wa kudhibiti mwenendo wake. Bei hizo huchangia wastani wa asilimia 45 ya bei ya mafuta katika soko la ndani. Itakumbukwa kuwa, pamoja na Serikali kuchukua hatua ya kupunguza/kuondoa baadhi ya tozo za mafuta mwezi Oktoba, 2021, bado bei ya bidhaa hiyo imeendelea kuongezeka kutoptaka na kupanda kwa bei katika soko la dunia. Kwa mantiki hiyo, ni dhahiri kuwa mabadiliko ya bei ya mafuta katika soko la dunia huathiri bei za bidhaa hiyo hapa nchini. Ili kukabiliana na changamoto hiyo na kwa kuzingatia uzoefu katika nchi nyingine, imeonekana ipo haja ya kufanya tathmini ya kina ya kuanzisha Mfuko wa Kudhibiti Mabadiliko ya Bei za Mafuta (*Fuel Price Stabilization Fund - FPSF*). Kupitia Mfuko huo, makali ya ongezeko la bei za mafuta hapa nchini yanaweza kupungua kwa kuwa fedha zitakazokusanywa zitatumika kufidia ongezeko la bei ya mafuta iliyokokotolewa kwa kuzingatia gharama halisi na bei kikomo itakayopangwa kudhibiti ongezeko la bei hapa nchini. Tathmini hiyo inatarajiwa kufanyaika mwaka 2022/23.

B 17: UDHIBITI WA MASUALA YA NISHATI KUPITIA EWURA

135. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, Wizara ya Nishati kupitia EWURA ilifanya shughuli mbalimbali za kiudhibiti kama ifuatavyo:

- (i) Kuendelea kuandaa na kuhuisha Kanuni na Miongozo mbalimbali ya udhibiti na uendelezaji wa masuala ya nishati sambamba na utoaji wa bei elekezi kwa bidhaa za mafuta nchini. Kanuni na miongozo hiyo ni: Kanuni za Umeme (Huduma za Ufungaji Mifumo ya Umeme) za Mwaka 2021; The Petroleum (Products Price Setting)(Amendment) Rules, za Mwaka 2022; The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Petroleum Product Price Setting) Rules, 2022; The Electricity (Licensing and Registration Fees) Rules, 2022; The Electricity (Electrical Installation Services) Rules, 2022; The Petroleum (Liquefied Petroleum Gas Operations) (Amendment) Rules, 2022; The Petroleum (Lubricants Operations) Rules, 2022; na The Wholesale, Storage, Retail and Consumer Installation) Rules, 2022. Ufanuzi wa Kanuni na Miongozo iliyoolewa ni kama inavyoonekana kwenye Kiambatisho Na. 14.
- (ii) Kutoa leseni 902 kwa Mafundi wa Ufungaji wa Mifumo ya Umeme (*electrical installations personnel*), ambapo daraja A ni 26, Daraja B 81, Daraja C 400, Daraja D 349, Daraja W 41, Daraja S1 mmoja (1), Daraja S2 mmoja (1) na Daraja S3 watatu (3). Kutoa leseni moja (1) ya muda (*provisional licence*) kwa Kampuni ya Ninety – Two Limited, Ngorongoro inayotegemewa kuzalisha megawati mibili (2) kwa kutumia nguvu za maji. Vilevile, EWURA imeendelea kufuatilia utekelezaji wa matumizi ya leseni hizo, ikiwemo kuhamasisha wananchi, taasisi za umma na binafsi kutumia mafundi umeme wenye leseni zitolewazo na EWURA. Kiambatisho Na. 15 kinafanua kwa kina kuhusu leseni zilizotolewa na wigo wa majukumu kwa kila daraja.

- (iii) Kuboresha mfumo wa utoaji wa leseni za Mafundi Umeme kwa kuititia Kanuni za ufungaji wa mifumo ya umeme na ulipaji wa ada za leseni ambazo zilitangazwa tarehe 4 Machi 2022 kuititia Gazeti la Serikali, GN Na.112 na Na.113; na kuongezwa kwa muda wa leseni hizo kutoka miaka mitatu (3) hadi mitano (5). Maboresho haya ambayo yanapatikana kuititia tovuti ya EWURA (www.ewura.go.tz) yatapunguza ghamama za maombi ya leseni kwa mafundi umeme na hivyo kuvutia mafundi wengi zaidi kujisajili na kurahisisha upatikanaji wa huduma; na
- (iv) Kuidhinisha mikataba ya kuuza umeme (*Standardized Power Purchase Agreement - SPPA*) kwa wazalishaji wawili (2) kwa Kampuni ya Ninety – Two Limited, Ngorongoro inayotegemewa kuzalisha megawati mbili (2) kwa kutumia nguvu ya maji na Jumeme Rural Power Co. Limited inayotegemea kuzalisha umeme kwa nguvu ya jua wenye kilowati 990 katika eneo la Mpanda na kilowati nyingine 990 katika eneo la Sumbawanga. Aidha, jumla ya leseni 12 za wazalishaji wadogo wa umeme zenye jumla ya MW 32.33 zimetolewa kama inavyoonekana katika Kiambatisho Na. 16.
136. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwezi Julai, 2021 hadi mwezi Machi, 2022, katika mkondo wa kati na wa chini wa sekta ya petroli, Serikali kuititia EWURA ilitoa jumla ya leseni 394 ambapo kati ya hizo, leseni 258 ni mpya na leseni 136 zimehuishwa muda wake. Kati ya leseni hizo, 320 ni za vituo vya mafuta; 25 ni za Wauzaji wa Mafuta kwa Jumla; tano (5) ni za Maghala ya Kuhifadhi Mafuta; 20 ni za Vituo vya Mafuta kwa ajili ya Matumizi Binafsi; tatu (3) ni za Viwanda vya Kuzalisha Vilainishi; nne (4) ni za Wauzaji wa Vilainishi kwa Jumla; 12 ni za Wasambazaji wa Gesi ya LPG; moja (1) ni ya Kutoa Huduma ya Kujaza Mafuta kwenye Meli (Bunkering Operations); moja

(1) ni ya kiwanda cha utengenezaji vilainishi, moja (1) ni ya usambazaji wa vilainishi, moja (1) ya kiwanda cha kuchakata gesi asilia na mbili (2) za vituo vya kujaza gesi asilia kwenye magari. Vilevile, EWURA ilihiusha leseni moja (1) ya Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA). Kiambatisho Na. 17 kinaonesha mchanganuo wa leseni zilizotolewa. Aidha, Kiambatisho Na. 18 ni wastani wa matumizi ya mafuta na mauzo kwa Kituo kwa Mwaka 2021.

137. **Mheshimiwa Spika**, EWURA imetoa jumla ya vibali 238 vya ujenzi wa vituo vya mafuta; vibali viwili (2) vya ujenzi wa Maghala ya kuhifadhi na kujaza kwenye mitungi gesi itokanayo na petroli (LPG); na kibali kimoja (1) kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kuunganisha gesi asilia katika kiwanda cha madawa.

B 18: USHIRIKISHWAJI WA WAZAWA KATIKA SEKTA YA MAFUTA NA GESI

138. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22 Serikali kuititia EWURA iliendelea na utekelezaji wa Kanuni za Ushirikishaji Wazawa kwenye mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia. Kwa ujumla ushirikishwaji wa wazawa umeendelea kuimarika ambapo kwa sasa uendeshaji wa mitambo ya uchakataji, usafirishaji na usambazaji wa gesi asilia unafanywa na Watanzania. Aidha, Taasisi za EWURA kwa kushirikiana na PURA zimeanzisha mfumo wa pamoja wa uratibu, ufuatiliaji, usimamizi na uwasilishaji wa taarifa mbalimbali kuhusu masuala ya ushirikishwaji wazawa (Common Qualification System-CQS). Mfumo huo kwa sasa ndio unaotumika kusajili watoa huduma wa ndani katika kanzi data (The Local Suppliers and Service Providers Database - LSSP). Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 jumla ya kampuni za ndani 1,286 zilikuwa zimejisajili kwenye Kanzi Data ya LSSP ikilinganishwa na Kampuni 608

zilizokuwa zimesajiliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22.

139. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia EWURA na PURA imeanzisha Kanzi Data ya Wataalam wa ndani (*Tanzania Professionals Database - TPD*). Lengo la Kanzi Data hiyo ni kuwezesha Kampuni za Kimataifa za Mafuta (International Oil Companies - IOCs) kuwapata kwa urahisi Watanzania wenyе sifa na uwezo wa kufanya kazi katika tasnia ya mafuta na gesi. Nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuhimiza wataalam wetu kujisajili katika Kanzi Data hiyo ili kuongeza wigo wa fursa za ajira kwa wataalam wa ndani. Kanzi Data hizi mbili (LSSP na TPD) zinapatikana katika tovuti za EWURA na PURA kupitia viunganishi "cqs. ewura.go.tz" na "cqs.pura.go.tz" mtawalia.
140. **Mheshimiwa Spika**, PURA iliendelea kuhakikisha Watanzania wanashiriki kikamilifu katika kutumia fursa zinazotokana na uwekezaji katika shughuli zinazohusu utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia. Kupitia kazi ya ukusanyaji wa taarifa za mitetemo katika Kitalu cha utafutaji wa mafuta na gesi asilia cha Ruvu, jumla ya Watanzania 530 walipata ajira za muda mfupi katika nafasi mbalimbali. Aidha, bidhaa na huduma zilizonunuliwa nchini wakati wa utekelezaji wa kazi hii zilikuwa na thamani ya Dola za Marekani milioni 39.41 sawa na takriban Shilingi bilioni 91.67.

C. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA KUKABILIANA NAZO

141. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana mwaka 2021/22, changamoto katika utekelezaji wa majukumu hazikosekani. Changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa na Wizara ili kuzipatia ufumbuzi ni pamoja na zifuatazo:
- a) Kupanda kwa bei ya mafuta kunakotokana na ongezeko la bei za mafuta katika soko la dunia na ongezeko la gharama za uagizaji wa mafuta. Hatua zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kutoa ruzuku ya Shilingi bilioni mia moja (**Shilingi 100,000,000,000**) kwa ajili ya kupunguza bei za mafuta hapa nchini kuanzia mwezi Juni, 2022.
- Hatua nyiningine ni kuanza zoezi la kuanzisha Mfuko wa Kudhibiti Mabadiliko ya Bei za Mafuta (*Fuel Price Stabilization Fund – FPSF*) pamoja na kuanzisha Hifadhi ya Mafuta ya Kimkakati (National Strategic Petroleum Reserve). Serikali pia itaendelea kuimarisha uwezo wa TPDC kuagiza mafuta nje ya nchi pamoja na EWURA na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja ili zitekeleze majukumu yao kwa tija na weledi zaidi.
- b) Kupanda kwa bei ya alumini, chuma na shaba duniani kunakoongeza gharama ya utekelezaji wa miradi ya umeme. Wizara inakamilisha uchambuzi wa athari hizo katika miradi ya umeme inayoendelea kutekelezwa ili kubainisha gharama zitaka-zoongezeka na kuchukua hatua stahiki za kukabiliana na athari hizo.
- c) Uhitaji mkubwa wa umeme ukilinganisha na uzalishaji. Kukamilika kwa miradi mikubwa ya uzalishaji na usafirishaji umeme inayoendelea kutekelezwa kama ilivyobainishwa katika Hotuba kutawezesha kutatuliwa kwa changamoto hii.

- d) Kuongezeka kwa mahitaji ya gesi asilia kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo kuzalisha umeme. Wizara inaendelea kutekeleza miradi ya utafutaji, uendelezaji, uzalishaji, ukarabati, usafirishaji na usambazaji wa gesi asilia, ikiwa ni hatua ya kukabiliana na changamoto hii.

D. MPANGO WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2022/23

- 142. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, Serikali itaendelea kuchukua hatua za kuimarishe na kuendeleza Sekta ya Nishati kwa kutekeleza vipaumbele mbalimbali kwa kushirikiana na wadau ikiwemo Sekta Binafsi. Mkazo utaendelea kuelekezwa katika kukamilisha miradi ya kimkakati ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme; kuimarishe upatikanaji wa nishati vijiji pamoja na kusimamia shughuli za utafutaji, uendelezaji, uzalishaji, uchakataji, usafirishaji na usambazaji wa mafuta na gesi asilia. Aidha, mikakati mbalimbali itatekelezwa ili kuimarishe upatikanaji wa rasilimali fedha za kugharamia uendelezaji wa Sekta ya Nishati pamoja na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.
- 143. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali itaendelea kuimarishe Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati ili ziweze kusimamia kwa ufanisi na tija uendelezaji wa Sekta ya Nishati katika maeneo yao, pamoja na kuimarishe nguvukazi ya Wizara ya kusimamia na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Taasisi, miradi na programu mbalimbali za Wizara.
- 144. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2022/23, Wizara itaongozwa na vipambele vifuatavyo:-

1. Kutekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme, ikiwemo kupeleka umeme

- wa Gridi ya Taifa kwenye mikoa ya Katavi, Kigoma na Kagera na mradi mkubwa wa Kuimarishe Gridi ya Taifa (*National Grid Stabilization Project*);
- 2. Kutekeleza Miradi ya Nishati Vijiji pamoja na kuanza utaratibu wa kupeleka umeme katika Vitongoji vyote nchini;
- 3. Kukamilisha mazungumzo ya mradi wa LNG Lindi na kuanza maandalizi ya utekelezaji wake;
- 4. Kutekeleza miradi ya nishati jadidifu ikiwemo jotoardhi, tungamotaka, upepo na jua pamoja na matumizi bora ya Nishati (*Energy Efficiency and Conservation*);
- 5. Kuhakikisha upatikanaji wa mafuta ya kutosha nchini, ikiwemo uanzishwaji wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta (*Strategic Petroleum Reserve*) na Mfuko wa Kudhibiti Mabadiliko ya Bei za Mafuta (*Fuel Price Stabilization Fund - FPSF*);
- 6. Kuiimarishe TPDC na Kampuni zake Tanzu za TANOIL na GASCO;
- 7. Kuboresha miundombinu ya kupokea, kushusha, kuhifadhi na kutoa mafuta katika Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara na Ghala za dhamana ya forodha (*Customs Bonded Warehouse*) na Kituo cha Pamoja cha kupokelea Mafuta kutoka Melini (*Single Receiving Terminal*);
- 8. Kuimarishe utendaji wa taasisi za Wizara, hasa TANESCO, EWURA na PBPA, na huduma zinazotelewa na taasisi hizo;
- 9. Kuongeza ushiriki na uwekezaji wa Sekta Binafsi katika sekta ya Nishati;
- 10. Kuhakikisha ushiriki wa wazawa katika shughuli za mafuta na gesi asilia unaimarika;
- 11. Kufufua Shughuli za utafiti na utafutaji wa mafuta na gesi asilia;
- 12. Kuongeza matumizi ya nishati ya gesi kwa kupikia (LPG) na kwenye magari na viwandani (CNG).

Hotuba ya Waziri wa Nishati

145. **Mheshimiwa Spika**, vipaumbele vya Bajeti katika mwaka 2022/23 pamoja na mambo mengine, vimejikita katika kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III), 2021/22 – 2025/26; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020; Maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan aliyojatoa kwa Wizara kwa nyakati tofauti ikiwa ni pamoja na wakati akihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021 pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030 kuhusu Nishati.
146. **Mheshimiwa Spika**, Miradi pamoja na majukumu mengine yaliyopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2022/23 kwa kila Sekta Ndogo ni kama inavyofafanuliwa hapa chini.

SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU

D 1: MIRADI YA KUZALISHA UMEME

D 1.1: MIRADI ILIYOPO KATIKA HATUA ZA UTEKELEZAJI

- (i) *Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Julius Nyerere Hydro Power Project (JNHP) – MW 2,115*
147. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu utakapokamilika utachangia **MW 2,115** katika Gridi ya Taifa na hivyo kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini. Gharama za utekelezaji wa mradi huu ni **Shilingi trilioni 6.55**. Pamoja na kazi nyingine za kiufundi zilizopangwa kufanywa, katika mwaka ujao wa fedha Serikali itaongeza umahiri na weledi kwenye usimamizi wa mradi ili kuhakikisha kwamba unamalizika ukiwa katika usalama na viwango stahili na malengo yake yanatimia. Jumla ya **Shilingi**

trilioni 1.44 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi mbalimbali kwenye mradi.

- (ii) *Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension – MW 185*

148. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu, ambao utagharimu **Dola za Marekani milioni 188** hadi kukamilika kwake, umetengewa **Shilingi bilioni 35** kwa ajili ya kazi za kukamilisha.

- (iii) *Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rusumo – MW 80*

149. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu wa nchi tatu, utaongeza uzalishaji wa umeme nchini kwa megawati 27. Utekelezaji wa mradi huu utakamilika katika mwaka ujao wa fedha ambapo tumetenga **shilingi bilioni 9.94** kwa ajili hiyo..

150. **Mheshimiwa Spika**, Pia ipo miradi iliyopo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:

- (i) *Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Ruhudji – MW 358*

151. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu ambao hadi kukamilika utagharimu **Dola za Marekani milioni 407.4** umezungumzwa kwa muda mrefu. Katika mwaka ujao wa fedha umetengewa **Shilingi bilioni 15** kwa ajili ya kazi mbalimbali kabla ya kuanza ujenzi wa mradi.

- (ii) *Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kakono – MW 87*

152. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu utagharimu **Dola za Marekani milioni 287.6** hadi kukamilika kwake. Katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itakamilisha upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa mradi kutoka kwa washirika wa maendeleo walioonyesha nia. Baada ya hapo, taratibu za ununuzi kwa ajili

- ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi zitaendelea. Jumla ya **Shilingi milioni 150** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.
- (iii) *Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rumakali – MW 222* unaogharimu **Dola za Marekani milioni 388.22** na umetengewa **Shilingi bilioni 8** fedha za ndani kwa ajili ya kukamilisha kazi mbalimbali kabla ya kuanza taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa **mradi**.
 - (iv) *Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Malagarasi – MW 49.5*
 - 153. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu, sio tu kwamba umeme wa Gridi ya Taifa utafika Kigoma, bali pia umeme unaoingia kwenye Gridi ya Taifa utazalishwa Kigoma. Fedha kiasi cha **Dola za Marekani milioni 144.14** za ujenzi wa mradi zinapatikana na taratibu za kuwapata Wakandarasi wa ujenzi wa mradi zimefikia ukingoni. Jumla ya **Shilingi bilioni 13.97** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kazi za awali.
 - (v) *Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kikonge – MW 300*
 - 154. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu una sehemu tatu: umwagiliaji, utalii na uzalishaji wa umeme, na utagarimu **Dola za Marekani milioni 795.4**. Mwaka ujao wa fedha tumetenga **shilingi bilioni 1.45** ili kukamilisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira ili kukamilisha taratibu za kupata fedha za utekelezaji wa mradi.
 - (vi) *Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Mtwara – MW 300*
 - 155. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imedhamiria kuzalisha umeme wa megawati 300 Mtwara kwa kutumia gesi asilia ili kuendeleza uchumi wa mikoa ya Kusini. Gharama za mradi zinakadiriba kuwa **Dola za Marekani milioni 421.1**. Fedha za kutekeleza mradi zimepatikana kutoka Serikali ya Japan. Pia tutajenga njia ya kufikisha umeme Somanga Fungu Lindi. Tumetenga **Shilingi milioni 600** kwa ajili ya kuanza.
 - (vii) *Mradi wa Kuzalisha Umeme Jua wa Shinyanga – MW 150*
 - 156. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka ujao wa fedha Serikali itaanza ujenzi wa mradi huu unaogharimu **Euro Milioni 115.30**. Jumla ya **Shilingi Bilioni 9.55** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme jua MW 50; na kukamilisha taratibu za ufadhili wa awamu ya pili ya MW 100.
 - (viii) *Ukarabati wa Mitambo katika Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Hale*
 - 157. ***Mheshimiwa Spika***, ukarabati utafanyika katika kituo hiki ili kizalishe kwa uwezo wake wa **MW 21** badala ya **MW 10.5** zinazosalishwa kwa sasa. Tumetenga **Shilingi bilioni 10.25** kwa ajili hiyo.
 - 158. ***Mheshimiwa Spika***, kuzalisha umeme ni jambo moja lakini kuusafirisha hadi kwenye maeneo ya watumiaji ni jambo lingine. Katika mwaka 2022/23, Serikali itatekeleza miradi ya usafirishaji umeme ambayo ipo katika hatua mbalimbali kwa sasa. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

Hotuba ya Waziri wa Nishati

D 2: MIRADI YA KUSAFIRISHA NA KUSAMBAZA UMEME

- (i) *Julius Nyerere Hydro Power Plant hadi Chalinze – kV 400*
159. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu ambaa utagharimu **Dola za Marekani milioni 51.4** na **Shilingi bilioni 31.9**, upo katika hatua za utekelezaji ambapo kazi zilizopangwa ni kuendelea na ujenzi wa mradi ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 180.00** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.
- (ii) *Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Singida – Arusha – Namanga*
160. **Mheshimiwa Spika**, kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Arusha hadi Namanga; na kukamilisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Lemugur, Arusha ambapo gharama ya mradi hadi unakamilika ni **Dola za Marekani milioni 258.82**. Katika mwaka 2022/23, jumla ya Shilingi bilioni 7.65 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.
- (iii) *Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 ya Geita – Nyakanazi*
161. **Mheshimiwa Spika**, Gharama ya mradi huu hadi unakamilika ni **Euro milioni 45** ambapo kazi zitakazotekelawa ni: kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Geita hadi Nyakanazi; kukamilisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Geita; na kuendelea na kazi ya usambazaji umeme katika vijiji/mitaa inayopitiwa na mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 6.53** fedha za nje zimetengwa katika mwaka 2022/23 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

- (iv) *Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 Rusumo – Nyakanazi*
162. **Mheshimiwa Spika**, kazi zitakazotekelawa ni: kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Rusumo hadi Nyakanazi ambapo fedha za ndani **Shilingi bilioni 3.30** zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.
- (v) *Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma*
163. **Mheshimiwa Spika**, jumla ya gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 35**. Mradi huu ambaa umepeleka umeme wa Gridi Kigoma upo tayari kwenye utekelezaji. Katika mwaka 2022/23, jumla ya **Shilingi bilioni 7.14** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme; ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kidahwe; upanuzi wa kituo cha Nyakanazi kutoka **kV 220** hadi **kV 400**; na kazi ya usambazaji wa umeme katika vijiji vinavyopitiwa na mradi.
- (vi) *Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 33 kutoka Nyakanazi - Kakonko- Kasulu - Kigoma*
164. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itakamilisha mradi huu ambaa pia utafikisha umeme wa Gridi katika mkoa wa Kigoma kabla ya mwezi Oktoba mwaka huu.
- (vii) *Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Iringa – Mbeya – Tunduma hadi Sumbawanga*
165. **Mheshimiwa Spika**, Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 595** ambapo kazi zitakazofanyika kwa mwaka 2022/23 ni: ulipaji wa fidia wananchi watakaopisha mradi; kukamilisha tathmini ya athari kwa mazingira; kumpata Mtaalam

Mshauri wa kusimamia ujenzi wa mradi na Mkandarasi wa ujenzi wa mradi; na kuanza ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vinne (Kisada, Mbeya, Tunduma na Sumbawanga) vya kupoza umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 34.71** fedha za ndani na nje zimetengwa ili kutekeleza kazi hizo.

(viii) *Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kwa ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (Standard Gauge Railway – SGR*

166. ***Mheshimiwa Spika***, TANESCO kwa kushirikiana na TRC itaendelea kuhakikisha miundombinu ya umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu kwa kilomita 415 inakamilika.

(viii) *Mradi wa Ukarabati na Uboreshaji wa Gridi ya Taifa (Grid Rehabilitation and Upgrading)*

167. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unalenga kuimariswa Gridi ya Taifa kwa kukarabati na kuboresha vituo vya kupoza umeme katika maeneo mbalimbali nchini utaanza kutekelezwa katika mwaka ujao wa fedha ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 8.43** zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

D 2.2: MIRADI ILIYOPO KATIKA HATUA ZA UTAYARISHAJI

(i) *Chalinze – Kinyerezi kV 400*

168. ***Mheshimiwa Spika***, Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 42.882** kwa upande wa njia ya kusafirisha umeme na **Dola za Marekani milioni 71.4** kwa upande wa kituo cha kupoza umeme. Kazi zitakazotekelawa ni pamoja na kukamilisha ulipaji fidia wananchi watakaopisha mradi; na kuanza ujenzi wa mradi ambapo **Shilingi bilioni 40.00** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

(ii) *Chalinze - Dodoma na Chalinze - Segera kV 400*

169. ***Mheshimiwa Spika***, Miradi hii kwa ujumla itagharimu **Dola za Marekani milioni 285.02** ambazo zinajumuisha ujenzi wa njia za kusafirisha umeme na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme. Kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na kukamilisha: Upembuzi Yakinifu; usanifu wa mradi; na taratibu za ufadhili wa mradi ambapo **Shilingi milioni 225.00** fedha za ndani zimetengwa zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

(iii) *Chalinze - Bagamoyo na Segera - Tanga kV 220* utakaogharimu jumla ya **Dola za Marekani milioni 163.21** ambapo jumla ya **Shilingi milioni 50.00** zimetengwa kwa ajili ya kuratibu shughuli za awali za utekelezaji wa mradi.

(iv) *Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Sumbawanga hadi Kigoma kupitia Mpanda, na Kituo cha Kupoza Umeme Mpanda*

170. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu una umahususi kwa sababu pia ni njia nyingine ya kupeleka umeme wa Gridi ya Taifa kwenye mikoa ya Katavi na Kigoma. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa

Hotuba ya Waziri wa Nishati

- Dola za Marekani milioni 200.4 kwa upande wa njia ya kusafirisha umeme, na **Dola za Marekani milioni 50** kwa upande wa kituo cha kupoza umeme. Kazi zitakazofanyika ni: kukamilisha taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kudurusu taarifa ya Upembuzi Yakinifu (*Upgrade of Feasibility Study*). AFDB imeonyesha niā ya kugharamiah mradi huu.
- (v) **Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Somanga Fungu hadi Mkuranga** utakaogharimu **Dola za Marekani milioni 150** ambapo Serikali kupitia TANESCO imetenga jumla ya Shilingi bilioni 4.85 kwa ajili ya kulipa fidia na kumtafuta Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kuhuisha Upembuzi Yakinifu wa mradi.
- (vi) **Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 na Kituo cha Kupoza Umeme katika Mkoa wa Simiyu** unaogharimu **Shilingi bilioni 75** ambao umetengewa **Shilingi milioni 725.00** kwa ajili ya kazi za awali ikiwemo fidia.
- (vii) **Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Benaco hadi Kyaka na Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Benaco na Upanuzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Kyaka**
171. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatekeleza dhamira yetu ya kupeleka umeme wa Gridi ya Taifa Kigoma. Gharama ya mradi inakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 119.4** ambapo katika mwaka 2022/23 kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kukamilisha Tathmini ya Mazingira na Jamii; kuanda zabuni; kufanya usanifu wa mradi; kumpata Mkandarasi wa mradi na kuanza ujenzi wa mradi.
- (viii) **Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 132 kutoka Tabora hadi Urambo na kutoka Urambo Tabora hadi Kidahwe mkoani Kigoma**
172. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu pia una dhamira ya kupeleka umeme wa Gridi mkoani Kigoma na utadharimu **shilingi bilioni 69.7**. Katika awamu ya kwanza, Serikali imetenga **shilingi bilioni 25** kwa ajili ya kupeleka umeme wa uhakika wa msongo mkubwa Urambo, kukamilisha Kituo cha kupohea umeme Urambo na kulipa fidia kwa wananchi waliopitiwa na njia.
- (ix) **Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 132 kutoka Tabora hadi Katavi kupitia Ipole na Inyonga**
173. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu pia utapeleka umeme wa Gridi ya Taifa mkoani Katavi. Utekelezaji wake ambao utahusisha njia na vituo vya kupozea umeme Ipole na Inyonga umeanza na Serikali imetenga **shilingi bilioni 124** kwa ajili ya kukamilisha, ambapo pia fidia kwa wananchi.
- (x) **Mradi wa Kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme katika Jiji la Dodoma**
174. **Mheshimiwa Spika**, kazi zilizopangwa kufanyika katika mradi huu ambao gharama yake ni **Dola za Marekani milioni 167.7** ni pamoja na: kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; kukamilisha taratibu za ufadhili; na kuanza taratibu za kupata Wakandarasi wa ujenzi wa mradi ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 6.57** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.
- (xi) **Mradi wa Kuimarishe Gridi ya Taifa (National Grid Stabilization Project)**
175. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imetafuta mwarubaini wa kadhia ya kukatika katika kwa umeme ambako kwa sehemu kubwa kunatokana na uchakavu na kutotosheleza kwa miundo mbinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme na imekuja na mradi wa kuimarishe Gridi ya Taifa. Mradi huu unahu uimarishejaji wa miundombinu ya ugavi wa umeme katika mikoa mbalimbali

ikiwa ni pamoja na ufungaji wa mitambo na vifaa vya kisasa, ubadilishaji wa nguzo za miti kwa kusimika nguzo za zege, ufungaji wa nyaya zenyne uwezo wa kusafirisha umeme mkubwa pamoja na mashineumba. Utekelezaji wa Mradi huu unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miaka minne na unakadirwa kugharimu **Dola za Marekani bilioni 1.9** sawa na takriban **Shilingi trilioni 4.420**. Katika mwaka ujao wa fedha jumla ya **Shilingi bilioni 500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza kazi hizo. Kielelezo Na. 17 ni mchanganuo wa mradi huo.

Kielelezo Na.17: Mchanganuo wa Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (National Grid Stabilization Projects) kwa Mwaka 2022/23

Na.	Maeneo ya Utekelezaji
1.	Kununua na kufunga mashineumba (transformers) 6,000
2.	Kununua na kusimika nguzo za njia za kusafirisha umeme 380,000
3.	Kununua na kufunga nyaya zenyne urefu wa Kilomita 46,200
4.	Kununua na kufunga Mita za Luku 700,000
5.	Kujenga vituo vya kupooza umeme (grid substations) 14 za 220/33kv na 132/33kv
6.	Kununua na kufunga mashineumba kubwa (power transformers) 27 za size ya 50MVA, 60MVA, 90MVA na 120MVA
7.	Kujenga njia za kusafirisha umeme za urefu wa Kilomita 948 za msongo wa Kv 132 na Kv 220

D 3: MIRADI YA NISHATI VIJJINI

176. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/23, Serikali kuititia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) itaendelea kutekeleza miradi ya kusambaza nishati bora vijijini na kuhamasisha matumizi ya nishati hiyo katika kuwaletaa maendeleo wananchi wa maeneo hayo. Aidha, Serikali imejizatiti kukamilisha kupeleka umeme katika vijiji vyote Tanzania Bara na kutekeleza mradi maalum wa kupeleka umeme katika vitongoji.
177. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha usimamizi wa miradi ya kupeleka umeme vijini na kurahisisha upatikani wa taarifa za maendeleo ya miradi hiyo, kwa mwaka ujao wa fedha, Serikali kuititia REA itaajiri waratibu wa miradi ya umeme vijijini kwa kila jimbo. Waratibu hao watakuwa kiungo cha mawasiliano na taarifa kati ya Wabunge, viongozi wa kisiasa, wakandarasi, REA na wadau wengine. Kwa kushirikiana na TANESCO, waratibu hawa watakuwa na wajibu wa kutoa taarifa za mara kwa mara kwa viongozi ikiwemo wa Wabunge kuhusu maendeleo ya miradi.
178. **Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na kilio cha muda mrefu cha wananchi wanaoishi katika maeneo ya mijini yenye sifa zinazolingana na vijiji huku wakilipa bei ya kuunganishiwa umeme ya mijini. Nataka niwahakikishie kwamba tumeendaa timu inayojumuisha Wizara ya Nishati, TANESCO na REA. Timu hii itazunguka katika miji yote na kuyabaini maeneo hayo kwa kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge wa maeneo husika. Maeneo yatakayobainishwa na timu hiyo yatajumuishwa kwenye bei ya vijiji yaani shilingi 27,000. Zoezi hili litafanyika nchi nzima na kukamilishwa ndani ya miezi sita.

179. **Mheshimiwa Spika**, ilevile, kuanzia mwaka 2022/23, Serikali itanzisha kampeni na kuandaa mikakati ya kuhamasisha matumizi ya nishati bora ya kupikia vijiji ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kwa lengo la kulinda afya za watu wetu (hasa matatizo katika mfumo wa kupumua), kutunza mazingira na kupunguza gharama na muda wa kutafuta nishati hiyo. Ili kutimiza azma hiyo, Serikali itanza mradi wa majaribio wa kusambaza gesi asilia maeneo ya vijiji katika mikoa ya Pwani na Lindi pamoja na kufanya utafiti wa kugundua aina nydingine za nishati na mifumo itakayofaa na kuendana na mazingira yetu katika kuwapatia wananchi wa vijiji nishati bora ya kupikia.

Mradi itakayotekelezwa ni kama ifuatavyo:

- (i) **Mradi wa Kusambaza Umeme Vijiji Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili**
180. **Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unalenga kufikisha miundombinu ya msingi ya umeme katika vijiji vyote ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya kusambaza umeme. Wigo wa awali wa mradi ulikuwa kufikisha umeme katika **vijiji 3,448**. Hata hivyo, baada ya usanifu wa kina, kuna **vijiji 469** vilibainika kutokuwepo katika wigo wa mradi. Ili kuhakikisha vijiji vyote vinafikiwa na huduma ya umeme, Serikali imeelekeza wakandarasi kujumuisha vijiji hivyo katika wigo wa kazi zao na hivyo kufanya jumla ya vijiji vitakavyofikiwa na mradi kuwa **3,917** na kupelekea vijiji vyote 12,345 vya Tanzania Bara kuwa vimefikiwa na huduma za umeme. Kwa sasa wakandarasi wameshaagizwa kufanya tathmini ya kupeleka umeme katika vijiji hivyo.

181. **Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo malalamiko ambayo yana mashiko, kwamba umeme unaofika vijiji unaawafikia wakazi wachache. Serikali imesikia kilio hicho na sasa ipo katika hatua za mwisho za kupata fedha zaidi kwa ajili ya kuongeza kilomita mbili kwa kila kijiji tofauti na wigo wa sasa wa kilomita moja, ili kuwezesha wengi kupata umeme.

182. **Mheshimiwa Spika**, Gharama za mradi ni **Shilingi Bilioni 1,240** na wigo wa awali utekelezwa kwa kipindi cha miezi 18. Katika Mwaka 2022/23, kiasi cha **Shilingi Bilioni 164.54** kitatumika ikiwemo kugharamia nyongeza ya wigo wa mradi.

(ii) **Mradi wa Kusambaza Umeme katika Vitongoji – (Hamlet Electrification Project – HEP)**

183. **Mheshimiwa Spika**, Baada ya kila kijiji sasa kuwa na mradi wa umeme, Serikali imeandaa mradi wa kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote nchini. Tanzania ina jumla ya vitongoji 64,760 na kati ya hivyo 37,610 bado havijafikiwa na miundombinu ya umeme. Gharama ya mradi huu inakadiriwa kuwa **Shilingi trilioni 6.5**. Katika Mwaka 2022/23, Serikali imetenga **Shilingi Bilioni 140.00** kwa ajili ya utambuzi wa wigo halisi wa mradi na kuanza kazi ya utekelezaji wa mradi kwa awamu.

(iii) **Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa 2B**

184. **Mheshimiwa Spika**, Mradi huu utahusisha ujenzi wa njia za usambazaji umeme zenye urefu wa kilomita 4,246 za msongo mdogo, ufungaji wa mashine umba 1,277 na kuunga wateja wa awali 95,334 katika vitongoji 1,686 katika mikoa ya Arusha, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Morogoro, Njombe, Simiyu na Songwe. Gharama za Mradi ni **Shilingi Bilioni 227**. Katika Mwaka 2022/23, kiasi kitakachotumika ni **Shilingi Bilioni 24.08**.

(iv) *Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa 2C*

185. ***Mheshimiwa Spika***, kazi zitakazofanyika ni ujenzi wa njia za kusambaza umeme msongo mdogo wenge urefu wa kilomita 6,562, kufunga mashineumba 1,932 na kuunganisha wateja wa awali 131,719 katika vitongoji 1,752 katika mikoa ya Iringa, Manyara, Mara, Mtwara, Rukwa na Ruvuma. Gharama ya mradi ni **Shilingi Bilioni 100**. Katika Mwaka 2022/23, kiasi kilichotengwa ni **Shilingi Bilioni 31.10**.

(v) *Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme Ifakara (220/33kV, 1 X 20MVA) na Ujenzi wa Miundombinu ya Usambazaji Umeme*

186. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi huu unahusisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Ifakara, ujenzi wa kilomita 299 za njia za msongo wa kati na mdogo, ufungwaji wa mashineumba 26 na kuunganisha vijiji 8 na vitongoji 7 katika Wilaya za Kilombero na Ulanga. Gharama ya mradi ni **Shilingi Bilioni 23.62** na kwa Mwaka 2022/23, kiasi cha **Shilingi Bilioni 2.00** zimetengwa katika kukamilisha mradi huo.

(vi) *Mradi wa Kusambaza Umeme Maeneo ya Vijiji-Miji Awamu ya Pili (Peri-Urban)*

187. ***Mheshimiwa Spika***, kazi zitakazofanyika ni kupeleka umeme katika maeneo 153 pembezoni mwa majiji ya Arusha, Dodoma na Mwanza kwa kujenga njia za kusambaza umeme zenye urefu wa kilomita 751 za msongo wa kati na mdogo, ufungaji mashineumba 143 na kuunga wateja wa awali 16,328 kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 31.33**.

(vii) *Mradi wa Kufunga Mifumo ya Umeme Jua katika Taasisi za Umma katika Wilaya Nane (Sustainable Solar Market Packages Phase II – SSMP)*

188. ***Mheshimiwa Spika***, mradi wa *Sustainable Solar Market Packages* ni mradi unaendelea kutekelezwa ambapo unahusisha ufungaji wa mifumo ya kuzalisha umeme jua katika Taasisi za Umma pamoja na kaya katika Wilaya za Biharamulo, Bukombe, Chato, Kasulu, Kibondo, Namtumbo, Tunduru na Sikonge. Kazi zilizopangwa kufanyika ni kufunga mifumo ya umeme jua katika Wilaya zilozosalia za Bukombe na Biharamulo. Kiasi kitakachotumika katika Mwaka 2022/23 ni **Shilingi Bilioni 1.50** kutoka Serikali ya Tanzania.

(viii) *Mradi wa Kupeleka Umeme kwenye Vijiji katika Visiwa na Maeneo Yaliyo Mbali na Gridi ya Taifa*

189. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unahusisha ujenzi wa miradi midogo midogo (*mini grids*) ili kuzalisha na kusambaza umeme kutokana na vyanzo vya nishati jadidifu kama vile jua, upemo, maporomoko madogo ya maji pamoja na tungamotaka katika maeneo mbalimbali yaliyo mbali na Gridi ya Taifa. Mradi utahusisha ufungaji wa mifumo ya umeme katika vijiji 35 vilivyopo katika visiwa 47 katika Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa na Delta ya Rufiji. Gharama ya mradi ni **Shilingi Bilioni 54.48**. Katika Mwaka 2022/23, kiasi kilichotengwa ni **Shilingi Bilioni 20.00** kutoka Serikali ya Tanzania.

(ix) *Mradi wa Kuwezesha Upatikanaji wa Nishati Bora ya Kupikia Vijijini - Support to Clean Energy for Cooking in Rural Area*

190. ***Mheshimiwa Spika***, Asilimia 89 ya kaya hapa nchini hutumia kuni na mkaa kama chanzo kikuu cha nishati ya kupikia. Jambo hili husababisha uharibifu wa mazingira na afya za watu.

191. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali imepanga kutumia **Shilingi Bilioni 10.00** kutekeleza mradi wa kupeleka na kusambaza gesi asilia katika makazi ya wananchi walio katika mkuza wa bomba kuu la gesi katika mikoa ya Mtwara,

Hotuba ya Waziri wa Nishati

- Lindi na Pwani. Mradi huu kwa maeneo ya vijijini ambao ni wa kwanza hapa nchini utakuwa wa majoribio. Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini itaendelea kutoa ruzuku kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli na wadau wengine ili kupanua huduma hizo katika maeneo mengi zaidi.
192. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/23, Serikali itatekeleza miradi, mipango na mikakati ya matumizi ya nishati safi na salama ya kupikia hasa maeneo ya Vijijini. Kwa ajili hiyo, tumeetenga Shilingi Milioni 500 ili kufanya kampeni kubwa ya kuhamasisha matumizi ya nishati bora ya kupikia pamoja na tafiti za kubaini nishati, mfumo sahihi na vivutio vya kusambaza nishati hiyo kwa maeneo ya vijijini matumizi ya kuni na mkaa ambazo pamoja na athari za kiafya pia zinachangia sana uharibifu wa mazingira.
- (x) **Mradi wa Kuwezesha Ujenzi wa Vituo Vidogo vya Kusambaza Bidhaa za Petroli Vijijini kwa Njia ya Mkopo Nafuu – Credit Line Facility**
193. **Mheshimiwa Spika**, Watanzania wengi vijijini wanalipa fedha nyingi zaidi kununua nishati ya mafuta, ambayo pia sio safi na salama. Kutibu kadhia hiyo, Serikali imebuni mradi uweshehaji wa waendelezaji wa vituo vidogo vya bidhaa za petroli kwa maeneo ya vijijini ambayo hayana vituo vya mafuta kwa njia ya mkopo nafuu. Mradi huu ni mpya na kazi zitakazotekelawa ni pamoja na kuandaa wigo wa mradi, kutangaza zabuni na kuwapata waendelezaji wadogo wadogo wa vituo vya mafuta vijijini ili kuanza ujenzi wa vituo hivyo. Katika Mwaka 2022/23, Serikali imepanga kutumia **Shilingi Biliioni 2.00** kutekeleza mradi huu. Mradi huu ni wa majoribio katika jitihada za kutafuta mbinu bora zaidi za kusambaza nishati ya mafuta salama na kwa bei nafuu vijijini.
- (xi) **Mpango wa Kuimarisha Vyanzo vya Mapato ya Kugharamia Miradi ya Nishati Vijijini**
194. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea na jitihada za kupeleka umeme katika viji ni na vitongoji kwa lengo la kuhakikisha Watanzania wote wanakuwa na nishati safi na ya gharama nafuu na pia kuwasharakishia maendeleo. Pamoja na jitihada hizo, hadi sasa jumla ya vitongoji 37,610 kati ya vitongoji 64,760 nchini, havijafikiwa na umeme na baada ya kufanya tathmini ya mahitaji ya fedha, imebainika kuwa jumla ya **Shilingi trilioni 6.50** zitahitajika kuwezesha kupeleka umeme katika vitongoji hivyo.
195. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia mwenendo wa bajeti ambayo REA inapatiwa kila mwaka kwa ajili ya kupeleka umeme vijijini, itachukua zaidi ya miaka 15 kufikisha umeme katika vitongoji vilivyosalia, jambo ambalo kudumaza maendeleo. Aidha, Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Umeme (PSMP) wa Mwaka 2020 unalenga kuhakikisha maeneo yote nchini yanaunganishwa na umeme ifikapo mwaka 2030. Kwa muktadha huo, hatuna budi kuhakikisha mikakati mbalimbali inatekelezwa ya kuhakikisha rasilimali fedha inapatikana ili kufikisha umeme katika vitongoji vyote.
196. **Mheshimiwa Spika**, ili kufikia azma hiyo, Serikali imeandaa Mpango Maalumu utakaowezesha kuongeza fedha zinazoingia katika Mfuko wa Nishati Vijijini kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa miradi mikubwa ya nishati vijijini kwa muda mfupi. Mpango huo unahusisha kupata vyanzo vypa vya mapato pamoja na kuongeza michango kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, ikiwemo kuongeza idadi ya wachangiaji. Aidha, katika mwaka 2022/23, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, itaangalia uwezekano wa kupata wakandarasi watakaowezesha upatikanaji wa fedha pamoja na utekelezaji wa miradi kwa kutumia mfumo ujulikanao kama "Engineering, Procurement, Construction Plus Financing (EPC+F).

197. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali imepanga kutumia **Shilingi Milioni 500.00** ili kubuni na kuanzisha na kuandaa na kutekeleza mikakati na mipango ya upatikanaji wa fedha za kutosha za kutekeleza miradi mikubwa ya nishati vijijini kwa muda mfupi.

198. **Mheshimiwa Spika**, miradi mingine itakayotekelezwa ni Mradi wa Kuwezesha Waendelezaji Binafsi wa Miradi ya Nishati katika Maeneo ambayo Hayajafikiwa na Gridi ya Taifa; Mradi wa Kupeleka Umeme katika Maeneo ya Wachimbaji Wadogo wa Madini, Viwanda na Kilimo; na Mradi wa Kupeleka Umeme katika Miradi ya Shule Vijijini pamoja na Mahakama za Mwanzo. Kiasi kilichotengwa katika mwaka 2022/23 kwa ajili ya kutekeleza kazi zilizopangwa ni **Shilingi Bilioni 35**.

D 4: UENDELEZAJI WA RASILIMALI YA JOTOARDHI

199. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2022/23, Serikali itaharakisha maandalizi ya uzalishaji wa umeme kwa kutumia rasilimali ya jotoardhi ambapo miradi minne ya Ngozi (Mbeya), Songwe (Songwe), Kiajo-Mbaka (Songwe) na Natron (Arusha), yenyewe uwezo wa kuzalisha takriban Megawati 200, itafanyiwa kazi. Jumla ya shilingi bilioni 5.18 zimetengwa kwa ajili ya kazi mbalimbali za maandalizi

200. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Serikali imetenga kiasi cha **Dola za Marekani milioni 5.04** sawa na takriban **Shilingi bilioni 11.71** kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Nishati (The National Energy Efficiency Action Plan) unaolenga kutoa mwongozo wa utekelezaji wa masuala ya matumizi sahihi ya nishati katika sekta za uzalishaji na matumizi bora ya nishati majumbani na katika taasisi mbalimbali

SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

201. **Mheshimiwa Spika**, kwa miaka mingi, imekuwa ni azma ya nchi yetu kuingia kwenye uchumi wa gesi ambao utakuza mapato ya serikali na kuwanufaisha wananchi. Katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itachukua hatua madhubuti kuharakisha azma hiyo.

D 5: UDHIBITI WA SHUGHULI ZA MKONDO WA JUU WA MAFUTA NA GESI ASILIA

202. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2022/23 Serikali kupitia PURA itasimamia uchorongaji wa visima mbalimbali vyta gesi na mafuta hapa nchini na kufanya ukaguzi katika maeneo yote ya utafutaji na uzalishaji wa gesi asilia nchini. Lengo la kazi hizi ni kuhakikisha sheria na mikataba husika inazingatiwa.

203. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia PURA itashamirisha shughuli za utafiti, utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi. Kwa ajili, hiyo itaanza maandalizi ya kunadi vitalu vilivyo wazi katika maeneo ya nchi kavu na baharini kwa kutumia mikataba maalum. Vilevile, Serikali kupitia PURA itaandaa ramani ya kidijitali yenyewe taarifa za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia nchini (Interactive Digital Petroleum Activities Map) ili kuongeza wigo wa utekelezaji wa shughuli za mkondo wa juu wa petroli nchini. **Shilingi bilioni 1.69** zimetengwa kwa ajili ya kazi hizi.

Hotuba ya Waziri wa Nishati

D 6: MIRADI YA UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA KATIKA VITALU VYA KIMKAKATI

204. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ilitenga vitalu vya mafuta vya gesi vya kimkakati kwa ajili ya kuipatia TPDC kutafuta gesi na mafuta ili kuijengea uwezo na uzoefu. Vitalu hivyo ni Mnazi Bay Kaskazini, Eyasi-Wembere, Songosongo Magharibi. Ziwa Tanganyika na 4/1B na 4/1C. Katika mwaka wa fedha wa 2022/23, Serikali imetenga kiasi cha **shilingi bilioni 102.167** kwa ajili ya kazi mbalimbali za maandalizi ya uchimbaji wa gesi na mafuta kwenye vitalu hivyo. Serikali, kupitia TPDC, pia itaharakisha mchakato wa kuwapata wabia kutoka sekta binafsi ili kushirikiana na TPDC kuendeleza vitalu hivyo.

205. **Mheshimiwa Spika**, pia viro vitalu vinaendeshwa na sekta binafsi ambavyo vinazalisha gesi au vimeonyesha dalili kubwa ya kuwa na gesi. Vitalu hivyo ni Ruvu, Ruvuma, Songosongo, Mnazi Bay, Kilosa-Kilombero na Vitalu Namba 1, 2 na 4. Katika mwaka 2022/23, Serikali kupitia PURA na TPDC itasimamia kuhakikisha kwamba waendeshaji wa vitalu hivi wanafanya kazi kwa mujibu wa ratiba za kwenye mikataba ili kuongeza uzalishaji wa gesi nchini.

D7: KUCHAKATA NA KUSINDIKA GESI ASILIA

(i) **Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (Liquefied Natural Gas – LNG)**

206. **Mheshimiwa Spika**, imekuwa ni ndoto ya nchi yetu kwa miaka zaidi ya kumi sasa kuchakata gesi nyingi iliyogunduliwa kwenye Bahari Kuu, kwa ajili ya mauzo nje ya nchi. Mazungumzo kati ya Serikali na makampuni ya mafuta na Gesi yamekuwa ya kikwama kama mara kwa mara.

(ii) **Mpango wa kufanya Eneo la Mradi wa LNG kuwa Ukanda Maalum wa Kiuchumi (Special Economic Zone)**

206. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na ukubwa pamoja na manufaa yatakayopatikana katika mradi wa LNG, ikiwemo kuchochea ukuaji wa uchumi katika eneo utakapotekelezwa na kitaifa, Serikali ina Mpango wa kuanzisha Ukanda Maalum wa Kiuchumi (Special Economic Zone) katika eneo la mradi ambapo maeneo yatatengwa na kuendelezwa kwa kuzingatia shughuli za kiuchumi na kijamii na kuyatangaza kwa ajili ya wawekezaji. Hatua hii, pamoja na kuimarisha shughuli za kiuchumi wakati wa utekelezaji wa mradi, pia itawezesha manufaa ya mradi kuendelea kupatikana hata baada ya ukomo wake. Katika mwaka 2022/23, Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na wadau itafanya tathmini ya kufikia azma hiyo.

D 8: MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI WA GESI ASILIA

(i) **Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani**

207. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2022/23, Serikali imetenga Shilingi bilioni 3.89 kwa ajili ya shughuli za usambazaji wa gesi asilia katika maeneo mbalimbali ya makazi na viwanda katika Jiji la Dar es Salaam ili kushamirisha matumizi ya nishati hiyo. Kwa upande wa mkoa wa Pwani Serikali kupitia TPDC imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 5.15** kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia viwandani.

(ii) *Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mkoa wa Lindi*

208. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia TPDC itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia yenye urefu wa kilomita 10.04 kutoka matoleo ya gesi katika bomba kubwa la kusafirisha gesi hadi eneo la Mnazi Mmoja ili kuwezesha matumizi ya gesi asilia katika eneo hilo. Kazi za usanifu na ujenzi wa miundombinu hii zinatarajiwaa kuanza mwezi Julai, 2022 na kukamilika mwezi Februari, 2023. Serikali kupitia TPDC imetenga jumla ya Shilingi bilioni 5.49 kwa ajili ya kazi hiyo.

D 9: MRADI WA VITUO VYA CNG KWA AJILI YA MATUMIZI YA NISHATI MBADALA WA PETROLI NA DISELI KATIKA MAGARI NA MATUMIZI MENGINEYO

(i) *Ujenzi wa Vituo vya CNG Katika Bohari za Mafuta za Serikali Dar es Salaam na Dodoma*

209. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia TPDC imepanga kutekeleza mradi wa ujenzi wa vituo vya kujazia gesi asilia iliyoshindiliwa (Compressed Natural Gas - CNG) kwenye magari katika Bohari kuu za mafuta za Serikali za Dar es Salaam na Dodoma. Lengo ni kuwezesha magari mengi zaidi ya Serikali na watu binafsi kutumia gesi asilia inayozalishwa nchini. Kwa kuanzia magari ya Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zilizo chini yake yatawekewa mfumo wa kutumia gesi asilia ikiwa ni azma ya Serikali ya kutaka kuongeza matumizi ya gesi hiyo nchini. Kazi zitakazotekelawa ni kujadiliana na kufikiwa kwa makubaliano kati ya TPDC na GPSA kuhusu matumizi ya ardhi za Bohari za Serikali kwa kujenga miundombinu ya CNG, kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii pamoja na kutayarisha usanifu wa kihandisi wa miundombinu ya CNG. Jumla ya Shilingi bilioni 1 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji kazi za awali za mradi.

(ii) *Ujenzi wa Kituo Mama na Vituo Dada vya CNG Katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani*

210. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia TPDC imepanga kutekeleza mradi wa ujenzi wa Kituo Mama (CNG mother station) cha kusindika gesi asilia katika mgandamizo mkubwa kwa ajili ya kuhudumia wateja wa CNG katika magari na pia kusambaza CNG kwenye vituo dada (CNG Daughter Stations) vitakavyokuwa mbali na miundombinu ya mabomba ya usambazaji wa gesi asilia. Sambamba na hilo, TPDC itajenga vituo dada vya kupokea na kuhifadhi CNG kwa matumizi ya gesi asilia katika magari, nishati ya viwanda na nishati ya kupikia katika taasisi na majumbani. Vituo dada vitatu vya CNG vitajengwa eneo la Kiwanda cha Madawa cha Kairuki, Kibaha; Hospitali ya Taifa Muhimbili na Soko Kuu la Samaki Feri Magogoni. Jumla ya Shilingi bilioni 23.2 zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Vilevile, Serikali inakamilisha makubaliano na makampuni ya sekta binafsi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia.

D 10: MIRADI YA KUSAFIRISHA GESI ASILIA KWENDA NCHI JIRANI

211. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali ina makubaliano ya awali (MOU) na nchi za Uganda na Kenya kwa ajili ya ujenzi wa mabomba ya kusafirishia gesi asilia kutoka Tanzania kwenda kwenye nchi hizo. Miradi yote ipo katika hatua za awali, ikiwemo matayarisho ya kufanya upembuzi yakinifu. Kwa upande wa mradi wa bomba la kwenda Uganda, Serikali imetenga shilingi milioni 635 na update wa bomba la kwenda Kenya shilingi milioni 656.10 kwa ajili ya kazi mbalimbali za awali.

Hotuba ya Waziri wa Nishati

D 11: MIRADI YA KUSAFIRISHA NA KUHIFADHI MAFUTA

- (i) **Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima - Uganda hadi Tanga - Tanzania (East African Crude Oil Pipeline - EACOP)**

212. **Mheshimiwa Spika**, kazi zitakazote-kelezwa ni pamoja na kuendelea kushiriki kwenye uwekezaji wa mtaji katika kampuni; kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi 9,122 wanaopisha mradi; kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu utekelezaji wa mradi na fursa zilizopo hususan katika maeneo yanayopitiwa na mradi; na kuanza shughuli za ujenzi wa mradi. Serikali imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 5.50** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu

- (ii) **Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Safi kutoka Dar es Salaam - Tanzania hadi Ndola – Zambia**

213. **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta safi kutoka Dar es Salaam hadi Zambia lenye urefu wa takribani kilomita 1,710 ambalo litatumia mkuza wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi la TAZAMA. Bomba litamilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zambia. Kazi zitakazofanyika ni: kufanya mapitio ya nyaraka za mradi; kuanza taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya Upembuzi Yakinifu wa mradi pamoja na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii zitokanazo na utekelezaji wa mradi. Jumla ya Shilingi milioni 500.00 zimetengwa na Serikali kugharamia shughuli hizo.

D 12: MRADI WA UANZISHWAJI WA HIFADHI YA KIMKAKATI YA MAFUTA (SPR)

214. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa uanzishwaji wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta (*Strategic Petroleum Reserve - SPR*) unahusisha uratibu wa uagizaji, uhifadhi na usambazaji wa bidhaa za mafuta kwa kipindi mahsus. Uanzishwaji wa SPR ni muhimu ili kuwezesha usalama na uhakika wa usambazaji mafuta nchini wakati wote. Ushiriki wa Serikali katika kuwezesha kuwepo kwa SPR utawezesha nchi kuwa na akiba ya mafuta muda wote na kuwezesha shughuli za uchumi kutoathiriwa na majanga mbalimbali.
215. **Mheshimiwa Spika**, kama sehemu ya maandalizi, Serikali kupitia TPDC inayo maeneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi mafuta (tank farms) katika maeneo ya kimkakati nchini ili kurahisisha usambazaji wa mafuta kwa nyakati zote. Maeneo hayo yapo Kigamboni (Dar es Salaam), Chongoleani (Tanga), Zuzu (Dodoma), Isaka (Shinyanga), Makambako (Njombe), Kibirizi (Kigoma) na Mpanda (Katavi).
216. **Mheshimiwa Spika**, ili kufanikisha ujenzi wa miundombinu ya SPR ikiwemo maghala na mabomba ya kusafirisha mafuta, Serikali imeendelea kuhusisha Sekta binafsi katika hatua hii ili kuharakisha utekelezaji wa mradi huu muhimu kwa uchumi wa nchi. Kwa sasa kazi mbalimbali zinaendelea ikiwemo kupitia na kuboresha hadidu za rejea za kuwapata wabia wa kimkakati, pamoja na kukamilisha usanifu wa kina wa mradi na kupata mahitaji ya mradi kwa ujumla

217. **Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kuiwezesha TPDC kushiriki kwenye uagizaji mafuta kwa jumla, shughuli ambayo iliachaa kuifanya miaka 20 iliyopita. Kupitia Benki Kuu na Wizara ya Fedha na Wizara mama ya Nishati, TPDC itajengewa nguvu ya kimtaji na kitaalam na kupewa kipaumbele kama taasisi ya kimkakati kwa nchi.

D 13: USHIRIKI WA TPDC KATIKA BIASHARA YA MAFUTA KUPITIA TANOIL

218. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TPDC inashiriki katika biashara ya usambazaji mafuta kupitia TANOIL (ambayo ni kampuni tanzu ya TPDC). TANOIL itaendelea na uagizaji wa mafuta kwa ujazo usiopungua tani 20,000 kwa mwezi. Ushiriki wa TANOIL umeimarisha ushiriki wa Serikali na kujenga uwezo wa TPDC na TANOIL katika biashara ya mafuta. Aidha, ili kuimarishe mtandao wa usambazaji, TPDC kupitia TANOIL itajenga na kukarabati vituo vyake vinne (4) vya mafuta vya Segera (Tanga), Makuyuni (Arusha), Tarime na Musoma (Mara) ili kusogeza huduma zake karibu na wananchi. Jumla ya **Shilingi bilioni 2.04** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hiyo.

219. **Mheshimiwa Spika**, TPDC pia inakusudia kuimarishe miundombinu ya uhifadhi mafuta ili kuwa na hifadhi ya mafuta ya kwake na kupunguza gharama za kukodi matenki kutoka makampuni binafsi. Kwa kuanzia, mkakati ni kukarabati Tenki namba 8 lenye uwezo wa tani 45,000 linalomilikiwa na TPDC na lililopo ndani ya hifadhi ya TIPER pamoja na matenki mengine yaliyopo katika eneo la TPDC Kigamboni. Jumla ya **Shilingi bilioni 12.11** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Baada ya ukarabati, Tenki hilo litatumwa na TANOIL.

220. **Mheshimiwa Spika**, katika kutanua wigo wa biashara, TANOIL imepanga kununua maeneo kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya mafuta kwa kushirikiana na Halmashauri za Manispaa na Wilaya, pia kuingia ubia na wawekezaji ambao watawekeza katika ujenzi huo. Kwa mpango huo TANOIL inatarajiwa kuwa na viwanja 50 katika maeneo tofauti nchini. Jumla ya **Shilingi bilioni 2.5** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hiyo.

D 14: KUIMARISHA USHIRIKI WA SEKTA BINAOFI KATIKA SEKTA YA NISHATI

(i) *Ubia kati ya TANOIL na Wawekezaji*

221. **Mheshimiwa Spika**, TPDC kupitia Kampuni yake tanzu ya TANOIL itaendelea kutafuta na kuingia ubia na Kampuni zenye uwezo na uzoefu ili kuwezesha usambazaji wa bidhaa za petroli kwa kasi katika maeneo ya mijini na vijiji hapa nchini. Mkakati huu utaongeza uwezo wa Serikali kuagiza, kuhifadhi na kusambaza bidhaa za petroli na hivyo kuwezesha kuwepo kwa mtandao mkubwa wa biashara ya mafuta nchini. Serikali kupitia TPDC itaandaa utaratibu bora wa upatikanaji wa Wabia ikiwa ni pamoja na kufanya upukuzi wa kina wa Wabia hao na kuandaa makubaliano ya awali (MoU). Jumla ya Shilingi bilioni 1 zimetengwa kwa ajili ya kuratibu shughuli hizo.

Hotuba ya Waziri wa Nishati

(ii) *Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Miradi ya Usambazaji Gesi Asilia*

222. **Mheshimiwa Spika**, ipo miradi ya umeme inayoweza kutekelezwa na sekta binafsi kwa manufaa ya umma. Katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itaongeza jitihada za kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi kwenye uzalishaji wa umeme. Serikali itakamilisha taratibu za kuwapata wawekezaji binafsi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kuzalisha umeme kupitia zabuni kwa miradi ya umeme yenye jumla ya MW 950 kwa kutumia jua, upopo na makaa ya mawe. Hadi sasa kampuni zilizokidhi vigezo baada ya mchujo zimefanyiwa upekuzi na zipo kwenye majadiliano na Serikali kuhusu mikataba ya kuuziana umeme ambapo utekelezaji utaanza mwaka 2022/23.
223. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na TANESCO imeandaa miradi 53 ya umeme yenye sura ya kutekelezwa kupitia Sekta Binafsi na kuiwasilisha kwa wawekezaji mbalimbali wakati wa maonesho ya Dubai Expo 2020. Kupitia maonesho hayo, jumla ya miradi saba (7) ya umeme jua, upopo na maporomoko ya maji yenye uwezo wa kuzalisha **MW 597** ilipata wawekezaji wenye nia ya kuiendeleza ambapo Mkataba wa Makubaliano (MoU) baina ya Serikali na mwekezaji huyo ulisainiwa. Katika mwaka 2022/23, Serikali itaendelea na majadiliano ya kina kuhusu namna ya utekelezaji wa miradi hiyo kupitia mwekezaji huyo. **Kiambatisho Na. 19** ni miradi ya umeme iliyopo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kupitia ushiriki wa Sekta Binafsi.

D 15: KUANDAA NA KUTEKELEZA

MIKAKATI NA MIPANGO MBALIMBALI YA UENDELEZAJI WA SEKTA YA NISHATI

224. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/23 Wizara kwa kushirikiana na Wadau, itaandaa na kutekeleza Mikakati/Mipango mbalimbali ya kuendeleza Sekta ya Nishati. Mikakati hiyo ni pamoja na Mkakati wa Nishati Jadidifu (*Renewable Energy Strategy and Roadmap*), Mkakati wa Matumizi Bora ya Nishati na Mpango wa Utekelezaji (*Energy Efficiency Strategy and Its Implementation Action Plan*) na Mkakati wa Tungamotaka (*Biomass Energy Strategy*). Wizara pia itafanya mapitio ya Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Umeme (*Power System Master Plan*) ili kuhakikisha unaendena na mahitaji ya sasa ya Sekta na pia kutekeleza Mpango Kabambe wa Nishati Vijijini (*Rural Energy Master Plan*) unaohusisha Mpango wa Usambazaji wa Umeme Vijijini pamoja na Mpango wa Nishati Safi ya Kupikia Vijijini.
225. **Mheshimiwa Spika**, Serikali pia inatafakari namna sahihi ya kutekeleza mpango wa kubadilisha deni la TANESCO kwa Serikali kuwa hisa za Serikali ili kuweka vitabu vya mahesabu vya shirikia katika hali nzuri itakayoliwezesha shirika kupata fedha za miradi bila kutegemea Serikali.

D 16: KUIMARISHA UTENDAJI NA UTOAJI WA HUDUMAWA TAASISI NA WIZARA

226. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inasimamia taasisi muhimu zinazotoa huduma moja kwa moja kwa wananchi na zenyet umuhimu katika ufanisi wa shughuli za taasisi na wadau wengine nchini. Utendaji, ufanisi na ueledi wa taasisi hizi ni kipaumbele muhimu cha mipango ya Serikali katika mwaka ujao wa fedha. Kwa upande wa TPDC, kama nilivyozeza hapo awali, Serikali italiimarishe

shirika hili kwa mtaji na utaalalm na kulifanya kuwa Shirika la kimkakati kwa uchumi wa Maendeleo ya nchi yetu. Kwa upande wa EWURA, kwa udhibiti wa sekta nyeti, Serikali itasitisiza kuijengea weledi, utaalalm na uhuru wa kupata nyenzo za kufanya kazi zake bila tofu lakini bila upendeleo.

Kwa upande wa PBPA, Serikali itahakikisha kwa watendaji wa taasisi hii wanakuwa waadilifu na taasisi inajenga uwezo wa kuijua vizuri biashara ya mafuta duniani na kutoa ushauri sahihi kwa serikali kuhusu usalama wa upatikanaji wa mafuta nchini wakati wote. Kwa upande wa PURA, Serikali itaijengea uwezo ili itimize wajibu wake wa kusimamia na kukagua utekelezaji wa mikataba ya mafuta na gesi nchini. Kwa upande wa TANESCO, Serikali itaiwezesha kulipa nafasi shirika kuendelea na mageuzi yanayoendela ya kulii marisha shirika na kuliwezesha kutoa huduma bora zaidi kwa wateja wake. Kwa upande REA, Serikali itaiwezesha kwa rasilimali zaidi, lakin pia tutaijengea uwezo wa kubuni miradi mbalimbali ya nishati vijijini na uwezo wa kuisimamia na kusimamia wazabuni ili miradi ikamilike kwa wakati uliokusudiwa.

227. Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha, TANESCO inategemea kuanza utekelezaji wa mradi wa kubadilisha mita za LUKU kwa kuweka mita janja (*smart meter*) ili kuwezesha wateja kununua umeme utakaoingia moja kwa moja kwenye mita zao na hivyo kuondoa usumbufo kwa wateja na kuongeza mapato ya TANESCO. Hatua nyingine ni kurahisisha taratibu za maombi na uunganishwaji wa umeme ili kupunguza gharama na muda wa kukamilisha taratibu hizo, ikiwemo za kugongewa mihuri kwenye fomu za maombi ya awali na kuhakikisha mfumo wa Nikonekt uliozinduliwa mwezi Aprili, 2022 unatumika nchi nzima kwa lengo la kuondoa usumbufo na gharama kwa wateja kufika Ofisi za TANESCO kwa ajili ya kufanya maombi ya kuunganishiwa umeme. Hatua hii itasaidia pia kuondoa mianya ya rushwa na vishoka.

E. USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

228. **Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa shughuli zake, Wizara ya Nishati inaendelea kushirikiana na Washirika wa Maendeleo, Jumuiya ya nchi wahisani na wadau mbalimbali. Kwa niaba ya Serikali napenda kutoa shukrani kwa nchi na mashirika hayo kama ifuatavyo: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Shirika la Fedha Duniani (IMF); Benki ya Ushirikiano wa Kimataifa ya Japan (JBIC), United Bank for Africa (UBA); na Economic Development Cooperation Fund (EDCF - Korea). Wengine ni Mfuko wa Uendelezaji Jotoardhi (Geothermal Risk Mitigation Facility - GRMF) pamoja na Taasisi na Mashirika ya: JICA (Japan), KfW (Germany), AFD (Ufaransa), DFID (Uingereza), Sida (Sweden), NORAD (Norway); Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Maendeleo la Canada (CIDA) na USAID (Marekani).
229. **Mheshimiwa Spika**, pia natoa shukrani kwa nchi ambazo zinashirikiana na nchi yetu katika kutekeleza miradi ya pamoja na kufadhili Sekta ya Nishati. Nchi hizo ni pamoja na: Kenya, Uganda, Zambia, Malawi, Burundi, Rwanda, DRC Congo, Msumbiji, Misri, Morocco, Algeria, China, Iceland, Japan, Norway, Korea ya Kusini, Uhlanzi, Oman na Umoja wa Falme za Kiarabu. Nazishukuru pia Jumuiya za Kikanda ambazo ni EAC, AU na SADC kwa ushirikiano katika masuala ya kikanda yanayohusu uendelezaji wa Sekta hii.

Hotuba ya Waziri wa Nishati

F. SHUKRANI

230. **Mheshimiwa Spika**, namshukuru Mhe. Stephen Lujwahuka Byabato (Mb.), Naibu Waziri wa Nishati kwa kunisaidia kutekeleza majukumu yangu. Aidha, napenda kumshukuru Katibu Mkuu Mha. Felchesmi Jossen Mramba na Naibu Katibu Mkuu Bw. Kheri Abdul Mahimbali. Ni wazi kuwa katika kipindi kifupi nilichofanya nao kazi wamenipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku na wameonesha ufanisi katika utendaji kazi zao. Napenda pia, niwashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote kwa ujumla kwa ushirikiano na juhudzi zao katika kufanikisha malengo ya Wizara.

G. HITIMISHO

231. **Mheshimiwa Spika**, kama nilivyobainisha awali, katika mwaka 2022/23 Wizara ya Nishati imejipanga kuleta mageuzi makubwa katika Sekta ya Nishati, lengo likiwa ni kuhakikisha rasilimali za mafuta na gesi asilia zilizopo nchini zinachangia ipasavyo katika maendeleo ya taifa letu na watu wake na kuimarisha upatikanaji wa nishati, ikiwemo iliyosafi na rafiki wa mazingira ili kuchocha kasi ya maendeleo ya viwanda, sekta ya huduma na shughuli ndogondogo za kiuchumi za wananchi. Aidha, Wizara itaendelea kutatua kero za wananchi hususan upatikanaji wa nishati ya umeme pamoja na kuimarisha utoaji wa huduma.

232. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liidhinishe Bajeti ya jumla ya **Shilingi 2,705,981,533,000** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:

(i) **Shilingi 2,676,229,576,000** sawa na **asilimia 99** ya Bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,508,756,128,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 167,473,448,000** ni fedha za nje; na

(ii) **Shilingi 29,751,957,000** sawa na asilimia **1** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 15,025,821,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 14,726,136,000** kwa ajili ya Mishahara (PE) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

233. **Mheshimiwa Spika**, naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.nishati.go.tz. Vile vile, Hotuba hii ina vielelezo mbalimbali ambavyo vimeambatishwa kwa ajili ya ufanuzi wa masuala muhimu yanayohusu Sekta ya Nishati.

234. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

VIAMBATISHO

**Kiambatisho Na. 1: Uwezo wa Mitambo ya
Kuzalisha Umeme hadi Kufikia mwezi Mei, 2022**

A: Mfumo wa Gridi ya Taifa		
Na.	Jina la Kituo	Uwezo (MW)
1.	Kidatu	204.00
2.	Kihansi	180.00
3.	Mtera	80.00
4.	New Pangani Falls	68.00
5.	Hale	21.00
6.	Nyumba ya Mungu	8.00
7.	Uwemba	0.84
8.	Mwenga	4.00
9.	Yovi	0.95
10.	Matembwe	0.59
11.	Darakuta	0.32
12.	Luponde	0.9
13.	Andoya	1.00
14.	Tulila	5.00
Jumla Ndogo - Maji		574.60
15.	Songas	189.00
16.	Ubungo I	102.00
17.	Tegeta	45.00
18.	Ubungo II	129.00
19.	Ubungo III	120.00
20.	Kinyerezi I	150.00
21.	Kinyerezi II	248.22
22.	Mtwara	30.60
23.	Somanga	7.50
Jumla Ndogo - Gesi Asilia		1,021.32
24.	Zuzu	7.40
25.	Nyakato	63.00
26.	Biharamulo	4.14
27.	Songea	5.77
28.	Liwale	0.85

Hotuba ya Waziri wa Nishati


29.	Tunduru	1.72
30.	Ludewa	1.27
31.	Mbinga	1.00
32.	Madaba	0.48
33.	Ngara	2.50
Jumla Ndogo - Mafuta		88.13
34.	TANWAT	1.50
35.	TPC	9.00
Jumla Ndogo – Tungamotaka		10.50
Jumla Kuu – Gridi ya Taifa		1,694.55

B: Nje ya Mfumo wa Gridi ya Taifa (Off-Grid)

Na.	Jina la Kituo	Uwezo (MW)
1.	Kigoma	8.75
2.	Mpanda	5.00
3.	Mafia	3.20
4.	Inyonga	0.82
5.	Kasulu	3.75
6.	Kibondo	2.50
7.	Loliondo	2.25
8.	Sumbawanga	5.00
9.	Bukoba	2.56
10.	NexGen Solawazi	5.00
Jumla - Nje ya Gridi		38.83
Jumla Kuu (Gridi na Nje ya Gridi)		1,733.38

Chanzo: **TANESCO**

Kiambatisho Na. 2: Mtando wa Njia za Kusafirisha Umeme Nchini (National Grid Network) hadi Kufikia mwezi Mei, 2022



Chanzo: **TANESCO**

Hotuba ya Waziri wa Nishati

Kiambatisho Na. 3: Taasisi Zilizounganishiwa Umeme hadi Kufikia Mwezi Mei, 2022

Na.	Mradi	Taasisi Zilizounganishiwa Umeme				
		Elimu	Biashara	Pampu za Maji	Afya	Nyumba za Ibada
1.	Miradi ya Awali	1,099	2,648	64	412	813
2.	Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Pili	1,947	4,943	513	1,069	212
3.	Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Kwanza	4,233	8,113	1,879	1,816	2,706
4.	Kusambaza Umeme Kwenye Njia Kuu ya Msongo wa Kilo Volti 400 (BTIP-VEI) Iringa, Dodoma, Singida, Taborana Shinyanga	125	223	11	113	7
5.	Ujazilizi Awamu I (Densification I)	226	3,570	928	507	1,279
6.	Kuzambaza Umeme katika Mkuza wa Njia ya Umeme Kilo Volti 220 (Makambako - Songea)	99	134	5	79	73
7.	Solar za Makontena	6	36		6	27
8.	Kuzambaza Umeme Pembezoni mwa Miji/ Majiji I (Peri Urban I)	26	40	13	7	12
9.	Ujazilizi Awamu II Fungu A (Densification IIA)	31	57	9	5	10
10.	Ufungaji wa Mfumo wa Umeme Jua kwenye Taasisi za Umma II (SSMP II)	82	-	-	195	-
Jumla		7,874	19,764	3,422	4,209	5,139
Jumla ya Taasisi Zote Zilizofikiwa na Umeme						40,408

Chanzo: **REA**

Kiambatisho Na. 4: Ramani ya Maeneo Mbalimbali yenyé Viashiria vya Uwepo wa Rasilimali ya Jotoardhi Nchini



Chanzo: TGDC

Hotuba ya Waziri wa Nishati

Kiambatisho Na. 5: Hali ya Mikataba ya Uzalishaji na Ugawanaji wa Mapato (PSA) kwenye mafuta na gesi asilia

NA.	KITALU	MUENDESHAJI	MKATABA ULIPO	ENEO LA UENDESHAJI
1.	Kitalu namba 1	SHELL Exploration and Production	Utafutaji	Baharini
2.	Kitalu namba 2	Equinor Tanzania	Utafutaji	Baharini
3.	Kitalu namba 4	SHELL Exploration and Production	Utafutaji	Baharini
4.	Ruvuma	ARA Petroleum	Utafutaji	Nchi kavu
5.	Kiliwani Kaskazini	Ndovu Resources	Utafutaji	Nchi kavu
6.	Songo Songo	Pan African Energy	Uzalishaji	Nchi kavu
7.	Mnazi Bay	Maurel et Prom	Uzalishaji	Nchi kavu
8.	Kilosa Kilombero	Swala Oil and Gas Tanzania	Utafutaji	Nchi kavu
9.	Ruvu	Dodsal Tanzania	Utafutaji	Nchi kavu
10.	Nyuni Area	Ndovu Resources	Utafutaji	Nchi kavu
11.	Tanga	Afren Tanzania Limited	Utafutaji	Nchi kavu

Chanzo: **PURA**

Kiambatisho Na. 6: Kiasi cha Gesi Asilia Iliyogunduliwa nchini hadi Kufikia Mwezi Mei, 2022


Kitalu cha Ugunduzi	Visima vya Uzalishaji/ Ugunduzi	Mwaka Ilipogundulika	Hali ya Sasa	Kiasi Kilichogunduliwa (Futi za Ujazo Trilioni - tcf)
Songo Songo	S4, S7,S10 & S11	1974	Imeendelezwa. Uzalishaji unaendelea.	2.5
Mnazi Bay	MB1, MB2, MB3 & MS-x1	1982	Imeendelezwa. Uzalishaji unaendelea.	5
Bigwa Rufiji Mafia	Mkuranga-1	2007	Haijaendelezwa.	0.2
Nyuni	Kiliwani-N	2008	Imeendelezwa. Uzalishaji ulisimama kutoptana na kupungua kwa msukumo wa gesi.	0.07
Ruvuma	Ntorya-1	2012	Haijaendelezwa, Inafanyiwa utafiti wa uendelezaji.	0.466
Ruvuma	Ntorya-2	2017		
Ruvu	Mambakofi-1	2015		2.17
KIWANGO CHA GESI YA NCHI KAVU				10.406

Block 1	Chaza-1	2011		0.47
	Jodari-1	2012		3.53
	Jodari North-1	2012		
	Jodari South-1	2012		
	Mzia-1	2012	Haijaendelezwa, inategemewa kuingizwa kwenye mradi wa LNG.	8.5
	Mzia-2	2013		
	Mzia- 3	2013		
	Mkizi -1	2013		0.6
	Taachui-1	2014		1.10
Block 2	Zafarani-1	2012		6.0
	Zafarani-2	2012		
	Lavani-1	2012		3.6
	Lavani-2	2012		1.4
	Tangawizi-1	2013	Haijaendelezwa, inategemewa kuingizwa kwenye mradi wa LNG.	5.4
	Mronge -1	2013		2.5
	Piri-1	2014		3.0
	Giligiliani-1	Aug-14		1.7
	Mdalasini	Mar-15		1.8
Block 3	Papa-1	2012	Haijaendelezwa.	2.0
Block 4	Chewa-1	2010		1.8
	Pweza-1	2010		1.9
	Ngisi - 1	2013	Haijaendelezwa, inategemewa kuingizwa kwenye mradi wa LNG.	0.8
	Kamba-1	2014		1.03
KIWANGO CHA GESI YA BAHARINI				47.13
JUMLA YA KIWANGO CHA GESI KILICHOGUNDULIWA NCHINI				57.54

Chanzo: **TPDC**

Hotuba ya Waziri wa Nishati

Kiambatisho Na.7: Ramani inayoonesha Shughuli za Utafutaji, Uendelezaji na Uzalishaji wa Gesi Asilia Nchini



Chanzo: **PURA**

Kiambatisho Na. 8: Uwezo wa Uzalishaji wa Gesi Asilia katika Vitalu vya Mnazi Bay na Songo Songo



KITALU	MZALISHAJI	KIASI (Futi za Ujazo Milioni/ Siku)
MNAZI BAY	Maurel & Prom (M&P)	70 – 110
SONGO SONGO	Pan African Energy (PAET)	80 - 110
JUMLA		220



Chanzo: **TPDC**

Hotuba ya Waziri wa Nishati

Kiambatisho Na. 9: Eneo la Mradi wa LNG na Mfano wa Uendelezaji wa Gesi Asilia katika Mradi ikihusisha Miundombinu ya Visima (Baharini) na Kiwanda cha Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika



Chanzo: **TPDC**

**Kiambatisho 10: Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mkoa wa Dar es Salaam
Uunganishaji wa Nyumba 100 na Miundombinu ya Kusambaza gesi Asilia Eneo la Chuo Kikuu
cha Dar es Salaam**



Chanzo: **TPDC**

Hotuba ya Waziri wa Nishati

Uunganishaji wa Nyumba 570 na Miundombinu ya Kusambaza Gesi Asilia Maeneo ya Sinza na Kurasini



Chanzo: **TPDC**

***Kiambatisho Na. 11: Uunganishaji wa Nyumba 209 na Miundombinu ya Usambazaji
Gesi Asilia Kata za Mnazi Mmoja na Mingoyo mkoani Lindi***



Chanzo: **TPDC**

Kiambatisho Na. 12: Urefu wa Miundombinu ya Kusambaza Gesi Asilia Nchini


MKOA	NA.	JINA	UMBALI (km)
Mtwara	1.	Dangote awamu 1	2.70
	2.	Dangote awamu 2	0.10
	3.	Majumbani awamu 1	16.60
	4.	Majumbani awamu 2	8.60
	Jumla Ndogo		28.00
Pwani	1.	Trunk line	7.10
	2.	Goodwill	1.65
	3.	Lodhia	3.70
	4.	Knauf	0.20
	5.	Raddy	0.75
	Jumla Ndogo		13.40
Lindi	1.	Majumbani awamu 1	18.30
	Jumla Ndogo		18.30
Dar es Salaam	1.	Ubungo - Mikocheni	7.20
	2.	NNGI - Ubungo Mikocheni	1.42
	3.	Mitambo ya kuzalisha umeme	6.50
	4.	Coca Cola	0.15
	5.	Majumbani UDSM	10.52
	6.	Majumbani - Mikocheni	4.30
	7.	Majumbani - Sinza	7.50
	8.	Majumbani - Kurasini	4.50
	9.	Viwandani (TPDC & PAET)	53.00
	Jumla Ndogo		95.09
JUMLA KUU		154.79	

Chanzo: **TPDC**

Hotuba ya Waziri wa Nishati

Kiambatisho Na. 13: Ramani ya Njia ya Bomba la Mafuta la Mradi wa EACOP

RAMANI YA BOMBA LA MAFUTA



Tanzania Mikoa (8)

1. Kagera
 2. Geita
 3. Shinyanga
 4. Tabora
 5. Singida
 6. Dodoma
 7. Manyara
 8. Tanga

Wilaya - 24

Kata - 134

Chanzo: ***TPDC***

Kiambatisho Na. 14: Orodha Ya Kanuni Zilizoandaliwa Julai 2021-Machi 2022

Na.	Kanunu	Gazeti la Serikali Na.	Tarehe ya Kutangazwa	Sekta
1.	Kanuni za Umeme (Huduma za Ufungaji Mifumo ya Umeme) Mwaka 2021	GN. 631/2021	13/08/2021	Umeme
2.	Petroleum(Products Price Setting)(Amendment) Rules,2022	GN. 2A/2022	03/01/2022	Mafuta
3.	The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Petroleum Product Price Setting) Rules, 2022	GN. 57/2022	28/01/2022	Mafuta
4.	The Electricity (Licensing and Registration Fees) Rules, 2022	GN. 112/2022	04/03/2022	Umeme
5.	The Electricity (Electrical Installation Services) Rules, 2022	GN. 113/2022	04/03/2022	Umeme
6.	The Petroleum (Liquefied Petroleum Gas Operations) (Amendment) Rules, 2022	GN. 114/2022	04/03/2022	Mafuta
7.	The Petroleum (Lubricants Operations) Rules 2022	GN.115/2022	04/03/2022	Mafuta
8.	The Wholesale, Storage, Retail and Consumer Installation) Rules 2022	GN. 150/2022	25/03/2022	Mafuta

Chanzo: **EWURA**

Kiambatisho Na. 15: Orodha ya Mafundi Wafungaji wa Mifumo ya Umeme Aprili 2022

Madaraja ya Leseni	A	B	C	D	W	S1	S2	S3	Jumla ya Leseni
Uzoefu katika	Msongo Mkubwa	Msongo wa Kati	Msongo Mdogo – Njia Tatu	Msongo Mdogo – Njia Moja	Wanaoanza	Wabobezi hadi kV 400	Wabobezi hadi kV 33	Wabobezi hadi V 400	
Idadi ya Leseni Hai	77	205	1,185	713	101	3	1	3	2,288

Chanzo: **EWURA**

Hotuba ya Waziri wa Nishati

**Kiambatisho Na. 16: Orodha ya Wazalishaji Wadogo wa Umeme wenyewe Leseni/Usajili EWURA
hadi Mwezi Aprili, 2022**

Na.	Mzalishaji Mdogo	Mahali/Wilaya	Chanzo cha Nishati	Uwezo wa kuzalisha na kuuza kwa TANESCO[MW]
1.	TPC	Moshi	Tungamotaka	9.00
2.	Tulila	Songea	Maji	5.00
3.	NextGen Solawazi	Kigoma	Umeme Jua	5.00
4.	Mwenga	Mufindi	Maji	4.00
5.	Mwenga	Mufindi	Upopo	2.40
6.	Madope	Ludewa	Maji	1.70
7.	TANWAT	Njombe	Tungamotaka	1.50
8.	Andoya	Mbinga	Maji	1.00
9.	Yovi	Kilosa	Maji	0.95
10.	Luponde	Njombe	Maji	0.90
11.	Matembwe	Njombe	Maji	0.56
12.	Darakuta	Magugu-Babati	Maji	0.32
Jumla				32.33

Chanzo: **EWURA**

Kiambatisho Na. 17: Mchanganuo wa Leseni Zilizotolewa

Na.	Aina ya Leseni	Mpya	Zilizohuishwa	Jumla
1.	Vituo vya Mafuta	196	124	320
2.	Wauzaji wa Mafuta kwa Jumla	15	10	25
3.	Vituo vya Mafuta kwa ajili ya Matumizi Binafsi	20	0	20
4.	Wasambazaji wa Gesi ya LPG	12	0	12
5.	Maghala ya Kuhifadhi Mafuta	5	0	5
6.	Wauzaji wa Vilainishi kwa Jumla	4	0	4
7.	Viwanda vya Kuzalisha Vilainishi	1	0	1
8.	Usambazaji wa vilainishi (Lubricant dealers)	1	0	1
9.	Huduma ya Kuza Mafuta kwenye Meli (bunkering licence)	0	1	1
10.	Kununua na Kuza condensate kutoka viwanda ya kuchakata gesi asilia nchini	1	0	1
11.	Kuchakata gesi asilia	1	0	1
12.	Kujaza gesi kwenye magari	2	0	2
13.	PBPA	0	1	1
Jumla Kuu		258	136	394

Chanzo: **EWURA**

Hotuba ya Waziri wa Nishati

Kiambatisho Na. 18: Wastani wa Matumizi ya Mafuta na Mauzo kwa Kituo kwa Mwaka 2021

Mkoa	Wastani wa Matumizi ya Mafuta kwa Mwaka (Lita)	Idadi ya Vituo vya Mafuta	Wastani wa Mauzo kwa Kituo kwa Mwaka (Lita)
Arusha	252,822,977	107	2,362,832
Coast	253,296,532	115	2,202,579
Dar es Salaam	1,149,703,994	316	3,638,304
Dodoma	212,146,536	102	2,079,868
Geita	46,729,656	72	649,023
Iringa	116,652,178	45	2,592,271
Kagera	102,042,394	92	1,109,156
Katavi	19,052,570	18	1,058,476
Kigoma	51,651,847	56	922,354
Kilimanjaro	100,899,822	101	999,008
Lindi	31,123,753	45	691,639
Manyara	25,523,817	53	481,581
Mara	69,129,792	69	1,001,881
Mbeya	164,515,387	94	1,750,164
Morogoro	148,359,963	99	1,498,585
Mtewa	79,615,459	56	1,421,705
Mwanza	278,531,014	126	2,210,564
Njombe	70,392,827	46	1,530,279
Rukwa	29,293,995	3	9,764,665
Ruvuma	64,402,211	44	1,463,687
Shinyanga	98,703,902	75	1,316,052
Simiyu	14,078,400	32	439,950
Singida	49,062,067	41	1,196,636
Songwe	31,376,688	42	747,064
Tabora	47,122,056	45	1,047,157
Tanga	135,581,090	83	1,633,507
Total	3,641,810,927	1,977	45,808,986

Chanzo: **EWURA**

Kiambatisho Na. 19: Miradi ya Umeme Iliyopo katika Hatua Mbalimbali za Utekelezaji Kupitia Sekta Binafsi

Na.	Jina la Mradi	Chanzo cha Nishati	Eneo la Mradi	Utaratibu wa Uzalishaji/ Uendeshaji	Hatua za Utekelezaji	Uwezo wa Uzalishaji
1.	Wazalishaji Binafsi (IPPs)-Nishati Jadidifu	Jua	Iringa, Dodoma and Singida	Mzalishaji Binafsi (IPP)	Majadiliano ya Mkataba wa Kuuziana Umeme yanaendelea	150MW
2.	Wazalishaji Binafsi (IPPs)-Nishati Jadidifu	Upepo	Njombe and Singida	Mzalishaji Binafsi (IPP)	Majadiliano ya mkataba wa kuuziana umeme yanaendelea	200MW
3.	Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Zuzu (MASDAR)	Jua	Dodoma	Ubia Bainya ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)	Mikataba ya awali utekelezaji wa Mradi	60MW
4.	Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Manyoni (MASDAR)	Jua	Manyoni - Singida	Ubia Bainya ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)	Mikataba ya awali utekelezaji wa Mradi	100MW
5.	Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Singida (Ikungi) (MASDAR)	Upepo	Singida	Ubia Bainya ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)	Mikataba ya awali utekelezaji wa Mrad	100MW
6.	Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Makambako (MASDAR)	Jua	Njombe	Ubia Bainya ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)	Mikataba ya awali utekelezaji wa Mrad	50MW
7.	Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Same (MASDAR)	Jua	Same-Kilimanjaro	Ubia Bainya ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)	Mikataba ya awali utekelezaji wa Mrad	50MW
8.	Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Jotoardhi wa Ngozi (MASDAR)	Jotoardhi	Mbeya	Ubia Bainya ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)	Mikataba ya awali utekelezaji wa Mrad	100MW

Hotuba ya Waziri wa Nishati

9.	Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Mnyera (MASDAR)	Maji	Kilombero - Morogoro	Ubia Bainya ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)	Mikataba ya awali utekelezaji wa Mrad	137MW
10.	Total Energies Solar Project	Jua	Dodoma	Mzalishaji Binafsi (IPP)	Majadiliano ya Kuingia Mkataba wa Makubaliano (MoU)	100MW
11.	Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Somanga Fungu	Gesi	Somanga - Lindi	Ubia Bainya ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)	Kumpata Mbia wa Kushirikiana na TANESCO	320MW
12.	Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Kibo Mining	Makaa ya Mawe	Mbeya	Mzalishaji Binafsi (IPP)	Majadiliano ya Kuingia Mkataba wa Makubaliano (MoU)	300MW
13.	Total Energies	Upopo	Singida	Mzalishaji Binafsi (IPP)	Majadiliano ya Kuingia Mkataba wa Makubaliano (MoU)	100MW
14.	Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Somanga Fungu (Kilwa Energy Company Ltd)	Gesi	Somanga - Lindi	Mzalishaji Binafsi (IPP)	Utafutaji wa fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji	345MW
16.	Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Geo Wind	Upopo	Singida	Mzalishaji Binafsi (IPP)	Kukamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha	100MW
17.	Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Mpanga (Iringa)	Maji	Morogoro	Mzalishaji Binafsi (IPP)	Majadiliano ya Kuingia Mkataba wa Makubaliano (MoU)	160MW
18	Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Rukwa (Edenville)	Makaa ya Mawe	Rukwa	Mzalishaji Binafsi (IPP)	Concept Note stage	360MW
19.	Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Mchuchuma	Makaa ya Mawe	Njombe	Mzalishaji Binafsi (IPP)	Kuanza Majadiliano ya Mkataba wa Kuuziana Umeme yanaendelea	600MW
JUMLA YA MIRADI MIKUBWA						3,332 MW
20.	Mradi mdogo wa maji Suma	Maji	Mbeya	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mkataba upo hatua ya kusainiana (SPPA)	4MW
21.	Mradi mdogo wa maji Ilundo	maji	Mbeya	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mkataba upo hatua ya kusainiana (SPPA)	0.56MW

22.	Mradi mdogo wa maji Kiwira	Maji	Mbeya	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mkataba upo hatua ya Makubaliano (SPPA)	10MW
23.	Mradi mdogo wa maji Luswisi	Maji	Songwe	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mkataba upo hatua ya kusainiana (SPPA)	4.7MW
24.	Mradi mdogo wa maji Igola	Maji	Njombe	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mkataba upo hatua ya kusainiana (SPPA)	2MW
25.	Mradi mdogo wa maji Lwega	Maji	Katavi	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mkataba upo hatua ya kusainiana (SPPA)	3MW
26.	Mradi mdogo wa maji Nkwilo	Maji	Rukwa	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mkataba upo hatua ya kusainiana (SPPA)	1MW
27.	Mradi mdogo wa maji Ifumbo	Maji	Morogoro	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mkataba upo hatua ya kusainiana (SPPA)	1MW
28.	Mradi mdogo wa maji Nakatuta	Maji	Ruvuma	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mkataba upo hatua ya kusainiana (SPPA)	5MW
29.	Mradi mdogo wa maji Igola	Maji	Njombe	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mkataba upo hatua ya kusainiana (SPPA)	2MW
30.	Mradi mdogo wa maji Kisiwa	Maji	Mafia	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mkataba upo hatua ya kusainiana (SPPA)	1.5MW
31.	Mradi mdogo wa maji Luponde	Maji	Njombe	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mwekezaji ana Mkataba na TANESCO na uzalishaji unaendelea	0.9MW
32.	Mradi mdogo wa Umeme Jua Kigoma	Umeme Jua	Kigoma	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mwekezaji ana Mkataba na TANESCO na uzalishaji unaendelea	5MW
33.	Mradi mdogo wa tungamotaka TANWAT	Tungamo Taka	Njombe	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mwekezaji ana Mkataba na TANESCO na uzalishaji unaendelea	1.5MW
34.	Mradi mdogo wa tungamotaka TPC	Tungamo Taka	Kilimanjaro	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mwekezaji ana Mkataba na TANESCO na uzalishaji unaendelea	9.0MW
35.	Mradi mdogo wa maji MWENGA	Maji	Iringa	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mwekezaji ana Mkataba na TANESCO na uzalishaji unaendelea	4.0MW
36.	Mradi mdogo wa maji ANDOYA	Maji	Ruvuma	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mwekezaji ana Mkataba na TANESCO na uzalishaji unaendelea	0.9MW

Hotuba ya Waziri wa Nishati

37.	Mradi mdogo wa maji MATEMBWE	Maji	Njombe	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mwekezaji ana Mkataba na TANESCO na uzalishaji unaendelea	0.54MW
38.	Mradi mdogo wa maji TULILA	Maji	Ruvuma	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mwekezaji ana Mkataba na TANESCO na uzalishaji unaendelea	5.0MW
39.	Mradi mdogo wa maji DARAKUTA	Maji	Manyara	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mwekezaji ana Mkataba na TANESCO na uzalishaji unaendelea	0.36MW
40.	Mradi mdogo wa maji YOVI	Maji	Morogoro	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mwekezaji ana Mkataba na TANESCO na uzalishaji unaendelea	1MW
41.	Mradi mdogo wa maji Madope	Maji	Njombe	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mkataba umesainiwa. Mradi upo hatua ya Ujenzi	1.7MW
42.	Mradi mdogo wa maji Maguta	Maji	Iringa	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mkataba umesainiwa, Mradi upo hatua ya Ujenzi	1.2MW
43.	Mradi mdogo wa maji Ijangala	Maji	Njombe	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mkataba umesainiwa, Mradi upo hatua ya Ujenzi	0.36MW
44.	Mradi mdogo wa Umeme Jua Kahama	Umeme Jua	Shinyinga	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mkataba umesainiwa na mradi upo katika hatua ya ujenzi	10MW
45.	Mradi mdogo wa maji Diwale	Maji	Morogoro	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mkataba umesainiwa na mradi upo katika hatua ya Ujenzi	5MW
46.	Mradi mdogo wa maji Pinyinyi	Maji	Arusha	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mkataba umesainiwa na mradi upo katika hatua ya ujenzi	1.9MW
47.	Mradi mdogo wa Umeme Jua Lumuma	Umeme Jua	Dodoma	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mkataba upo katika hatua ya kusainiana (SPPA)	2MW
48.	Mradi mdogo wa Umeme Jua Kongwa	Umeme Jua	Dodoma	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mradi umepewa kusudio la Awali (Letter of Intent)	5MW
49.	Mradi mdogo wa Umeme Jua Igunga	Umeme Jua	Tabora	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mradi umepewa Kusudio la Awali (Letter of Intent)	5MW
50.	Mradi mdogo wa Umeme Jua Isangawana	Umeme Jua	Mbeya	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mradi umepewa Kusudio la Awali (Letter of Intent)	8MW

51.	Mradi mdogo wa Umeme Jua Gua	Umeme Jua	Songwe	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mradi umepewa Kusudio la Awali (Letter of Intent)	5MW
52.	Mradi mdogo wa Umeme Jua Mbarali	Umeme Jua	Mbeya	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mradi umepewa kusudio la Awali (Letter of Intent)	6MW
53.	Mradi mdogo wa Umeme Jua Sumbawanga	Umeme Jua	Rukwa	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mkataba upo hatua ya kusainiana (SPPA)	1MW
54.	Mradi mdogo wa umeme Jua Mpanda	Umeme Jua	Katavi	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mkataba upo hatua ya kusainiana (SPPA)	1MW
55.	Mradi mdogo wa Umeme Jua Bugando	Umeme Jua	Mwanza	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mradi umepewa Kusudio la Awali (Letter of Intent)	5MW
56.	Mradi mdogo wa Umeme Jua Chamwino	Umeme Jua	Dodoma	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mradi upo hatua za Kusudio la Awali (Letter of Intent)	5MW
57.	Mradi mdogo wa maji Luengere	Maji	Kigoma	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mradi umepewa Kusudio la Awali (Letter of Intent)	5.34MW
58.	Mradi mdogo wa maji Idete	Maji	Njombe	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mradi upo hatua za Kusudio la Awali (Letter of Intent)	1MW
59.	Mradi mdogo wa Umeme Jua Convivium	Umeme Jua	Mwanza	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mradi upo hatua za Kusudio la Awali (Letter of Intent)	5MW
60.	Mradi mdogo wa maji Kikuletwa II	Maji	Kilimanjaro	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mradi umepewa Kusudio la Awali (Letter of Intent)	8MW
61.	Mradi mdogo wa maji Chimala	Maji	Mbeya	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mradi umepewa Kusudio la Awali (Letter of Intent)	2.5MW
62.	Mradi mdogo wa maji Kamwana	Maji	Kagera	Mzalishaji Mdogo Binafsi (SPP)	Mradi umepewa Kusudio la Awali (Letter of Intent)	2.5MW
JUMLA YA MIRADI MIDOGO(SPPs)						111.62MW
JUMLA KUU YA MIRADI MIKUBWA NA MIDOGO						3,443.62MW



Wizara ya Nishati

Mtaa wa Nishati, Mji wa Serikali Mtumba
S.L.P 404774, Dodoma

+255 26 2322018

ps@nishati.go.tz